**26 JUNI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Hamsini na Nne – Tarehe 26 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na: -

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(Agreement for the Establishment of the Africa Finance Corporation – AFC)*.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Maelezo ya Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(Agreement for the Establishment of the Africa Finance Corporation – AFC)*.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Ester Bulaya.

Na. 690

**Kukamilisha Ujenzi wa Mradi wa *Dege Beach*-Mbweni**

**MHE. ESTER A. BULAYA K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha majengo ya Mradi wa *Dege Beach-NSSF* Mbweni kwa kuwa ni wa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya mradi wa *Dege Eco Village* uliopo Kigamboni Jijini Dar es Salaam na kujiridhisha kuwa itakuwa ni hasara kuendelea na ujenzi wa mradi huo. Hivyo imeamriwa mradi huo uuzwe kwa wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mfuko unaendelea na hatua na taratibu za wawekezaji wenye nia ya kutwaa eneo hili kwa nia ya kununua mradi huo waweze kupewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Kwanza ninatoa pongezi kwa *Dar Young Africans* kwa kuchukua ubingwa bila kipengele chochote na hiyo ndiyo Yanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kumekuwa na malalamiko ya wastaafu fedha zao kutumika kwenye uwekezaji bila kushirikishwa: -

(a) Je, Serikali ina kauli gani katika hili?

(b) Je, kuna miradi mingine aina ya *Dege Beach* ambayo imeiletea Serikali hasara ambayo mmeifanyia tathmini na hatua gani ambayo mmechukua kwa walioruhusu uwekezaji kama huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante na ninaomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kuhusu malalamiko ya wastaafu kuhusiana na fedha zao kuwekezwa hilo hatujalipata rasmi kama ofisi. Kimsingi sababu za uwekezaji zinazofanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, tunafanya baada ya kufanya tathmini na kushauriwa na Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)*. Kuna mwongozo maalum kuhusiana na maeneo ya uwekezaji na namna ya kuwekeza. Tafiti zinafanyika na wanashauri baada ya kuwa mmefanya utafiti huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lengo la kuwekeza ni kwa ajili ya kulinda thamani ya fedha ya mfuko, kwa sababu kuna wakati mwingine inatokea *price fluctuation* au mfumuko wa bei au kushuka kwa shilingi au thamani ya fedha. Sasa fedha hizi zitakapokuwa zimewekwa tu kama kwenye kibubu halafu baadaye fedha ikashuka thamani maana yake unapeleka athari kwa mwanachama mwenyewe kushindwa kuja kupata fedha au mafao mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo zinawekezwa ili ziweze kulinda ile thamani ya fedha yenyewe, lakini pia kutengeneza *stability* ya

mfuko. Kila wakati tunafanya *actuarial valuation* kwa mujibu wa sheria na mwongozo. Kwa hiyo, pia hata hivyo katika hatua hiyo tunaangalia mambo mawili, *cost benefit analysis* na pia tunafanya *profit and loss analysis,* ili kujiridhisha kwamba patakapowekezwa basi kuwe kuna tija na faida kwa mfuko, lakini zaidi kwa wanachama wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili linafanana na la kwanza na swali la pili linasema kwa nini tunaweka miradi ambayo inakuwa na hasara.

Mheshimiwa Spika, miradi yote hii ambayo inafanywa inafanyiwa tafiti na mwongozo wa *BOT* unaelekeza kwamba kabla ya mradi kuwekezwa kwanza ufanyiwe tafiti, kuwe na andiko la mradi na kisha kwenda *BOT* kufanyiwa mapitio na hatimaye kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, sasa kinachojitokeza kwa mfano wa Mradi wa Dege anaueleza Mheshimiwa Mbunge kwenye swali, ni kwamba wakati wa uwekezaji, wakati ule, mazingira yaliruhusu na kulikuwa kuna tija na haja ya mradi huo kuwekwa kwa wakati ule, lakini kadri muda ulivyokwenda mambo yalibadilika. Kwa mfano uamuzi wa kuihamisha Serikali kwa kuitoa Dar es Salaam kuja Jijini Dodoma kuliathiri maeneo mengi ambayo ukiacha tu hata kwenye Mradi wa Dege, lakini pia hata miradi kwenye *private investment* na maeneo mengine yalikuwa na athari.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo kuna mambo ya kimkataba na muda ambayo kimsingi yote haya huwa ni mazingatio ya msingi kuweza kuhakikisha na ndiyo maana hatua nzuri ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilikuwa ni kufanya utafiti na *assessment* kwenye miradi yote…

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** … kuangalia yenye hasara ili kurudisha

faida, kwa maana ya kuweka utaratibu hata huu wa kuuza ili kuweza kulinda ile thamani ya fedha na kuboresha mafao ya wafanyakazi kama jinsi alivyofanya Mheshimiwa Rais kwa sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, Kamati ya Uongozi, Wajumbe wa Kamati ya Uongozi waelekee hapo *lounge* kwa ajili ya kikao, waelekee hapo sasa hivi kwa ajili ya kikao.

Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, sasa aulize swali lake.

Na. 691

**Kukamilisha Maboma ya Zahanati – Sikonge**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza: -

Je, lini Zahanati za Molemlimani, Muungano, Urafiki, Isanjandugu, Iyombakuzova na Kapumpa zitakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujenga vituo vya kutolea huduma na kuvisajili ili vianze kutoa huduma za afya. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 jumla ya zahanati 1,158 zimejengwa na kusajiliwa na zinatoa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge itatenga shilingi milioni 250 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya

Zahanati za Muungano, Urafiki, Isanjandugu, Iyombakuzova, Kapumpa na Molemlimani. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wa Vijiji vya Isanjandugu, Iyombokuzova, Urafiki, Muungano, Kapumpa na Molemlimani wamejitahidi sana kujitolea nguvu zao kwa kushirikiana na mfuko wa jimbo wakajenga maboma hayo.

Je, kwa nini Serikali isiwaunge mkono kwa *block grants* za Serikali Kuu moja kwa moja badala ya kusubiri bajeti ya ndani ya halmashauri ambayo imekuwa haitoshi ni ndogo, hadi mwaka 2026/2027; kwa nini mwaka huu wasisaidiwe?

Je, ni kwa nini Serikali isichukue orodha ya maboma yote ambayo wananchi wamechangia kwa nguvu za wananchi nchi nzima halafu ikaipangia bajeti kukamilisha maboma yote kabla hatujaanzisha ule Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Wote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza natumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Joseph George Kakunda kwa namna ambavyo amekuwa akiwasemea wananchi wa Jimbo la Sikonge na kwa namna ambavyo amefuatilia kuona kwamba Serikali inapeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati hizi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua kwamba wananchi wametoa nguvu zao na

natumia nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Sikonge na yeye Mheshimiwa Mbunge kwa kutoa fedha za Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya ukamilishaji wa baadhi ya maboma.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kutenga fedha kwenye bajeti kila mwaka. Kwa kipindi hiki, katika mwaka huu wa fedha tayari Serikali imeitengea Halmashauri ya Sikonge shilingi 180,000,000 kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati za Ibumba, Mwamaluga na Ipembe.

Mheshimiwa Spika, wakati huo katika mwaka wa fedha 2026/2027 tutakwenda kukamilisha zahanati hizi kwa shilingi 250,000,000. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba zoezi hili ni endelevu na tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakamilisha majengo haya ili yaweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili, tunafahamu kwamba kuna maboma mengi wananchi wamejenga na Serikali tayari imekwishaainisha. Tuna jumla ya maboma ya zahanati 1,614 ambayo yako kote nchini, yanahitaji fedha za ukamilishaji. Hivi karibuni, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwezi mmoja uliopita imetoa zaidi ya shilingi 17,650,000,000 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 346 kati ya hayo 1,614 ambayo yamekwishatambuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kuyatambua maboma, tunaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba yanakamilishwa na kutoa huduma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Venant Daud Protas.

Na. 692

## *TARURA* Kutengeneza Barabara Zisizoharibiwa na Mvua

**MHE. VENANT D. PROTAS K.n.y. MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza: -

Je, lini *TARURA* itaweza kutengeneza barabara zenye viwango zisizoharibika kipindi cha mvua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuimarisha uwezo wa kibajeti na rasilimali watu kwa *TARURA* ili kuwezesha ujenzi wa barabara za kudumu zenye viwango bora zaidi. Lengo ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora ya usafiri wakati wote wa mwaka na pia kuhakikisha barabara zinajengwa kwa viwango vinavyokidhi mahitaji ya kudumu na kwa kufuata usanifu wa kina uliofanyika huku ukizingatia viwango vya ubora vilivyowekwa, hususani katika kukabiliana na athari za hali ya hewa hasa katika nyakati za mvua.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ni muhimu kufahamu kuwa barabara nyingi za vijijini bado ni za udongo na changarawe. Barabara hizi ni rahisi kuathiriwa na mvua nyingi na magari makubwa yanayozidi uwezo wake wa kubeba mizigo. Hali hii husababisha barabara hizi kuharibika haraka kuliko muda uliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha mtandao wa barabara za vijijini na mijini kwa kuzijenga katika viwango vya kudumu kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Venant Daud Protas, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante, mwaka 2023/2024 kutokana na mvua nyingi kunyesha barabara nyingi zilipata hitilafu ikiwemo Barabara ya Goweko – Ndebelwa – Tabora Mjini, Barabara ya Izumba – Mpumbuli na Barabara ya Loya – Mabeshi. Pamoja na udharura wake, tulileta kwa hati ya dharura mpaka leo barabara hizi hazijatengenezwa.

Je, nini mkakati wa Serikali kuweka mikakati madhubuti ili pindi barabara hizi zinapoharibika zinaweza kupitika muda wote ili wananchi wasipate adha kama wanavyopata adha mpaka waakti huu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kuwa barabara ni za udongo na mvua nyingi zikinyesha zinapata hitilafu; je, Wizara hawaoni kama katika fedha mnazoleta za *TARURA* kila halmashauri, basi tuwe tunakata 10% ambayo tunaweka kwenye mfuko maalum ili ikitokea dharura, zile fedha ziwepo ili zikatatue kutokana na udharura wake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali yote mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja kwamba kwanza, Serikali inaweka kipaumbele kikubwa sana katika kuhakikisha kuwa inaimarisha miundombinu ya barabara hizi za wilaya zinazosimamiwa na *TARURA*. Ni dhahiri kwamba mvua nyingi zinazojitokeza kutokana na mabadiliko ya tabianchi zimesababisha barabara zetu ziweze kuharibika na kuleta adha kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua jitihada za makusudi kabisa ili kuhakikisha kwamba inachukua hatua za dharura pindi pale mawasiliano yanapokuwa yamekatika kwenye barabara zetu. Mathalani, Mheshimiwa Mbunge ametaja katika jimbo lake barabara hizi ambazo zimeathirika katika mwaka wa bajeti

2023/2024 ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba inazifikia hizi barabara na kuhakikisha kwamba inachukua hatua za dharura kuzikarabati na kuzijenga na kuleta kuunganisha mawasiliano ambayo yamekatika ili wananchi wetu wasiweze kupata adha.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inatenga bajeti maalum kabisa ya dharura kila mwaka wa bajeti. Mathalani, katika mwaka 2023/2024 Serikali ilitumia zaidi ya shilingi 131,000,000,000 kama fedha ya dharura kwa ajili ya kuhakikisha kuwa inarudisha mawasiliano katika maeneo ambayo mawasiliano yamekatika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa bajeti, Bunge hili lilipitisha nyongeza ya bajeti ya dharura ya *TARURA* shilingi 50,000,000,000; na mpaka sasa katika mwaka wa fedha huu tuliokuwa nao, tuna shilingi 71,000,000,000 ambazo zimetumika kwa ajili ya kuchukua hatua za dharura za kurudisha mawasiliano katika maeneo ambayo mawasiliano yamekatika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuchukua hatua zote za msingi kuhakikisha inaendelea kuimarisha miundombinu ya barabara hizi muhimu kabisa ambazo zinawasaidia wananchi katika shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuchukua hatua zote za msingi kuhakikisha inaendelea kuimarisha miundombinu ya barabara hizi muhimu kabisa ambazo zinawasaidia wananchi katika shughuli zao za kiuchumi na ambazo zinawawezesha kufikia huduma za msingi kabisa za kijamii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi moja kwa moja kwenye swali na majibu vilevile.

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya ya Rungwe ni wilaya yenye mvua nyingi, Serikali italeta lini fedha za ziada kwa ajili ya kutengeneza barabara zinazoharibika mara kwa mara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa ikifanya uwekezaji mkubwa sana kwenye kuimarisha barabara zetu hizi za wilaya zinazosimamiwa na *TARURA*. Utaona katika mwaka wa fedha 2020/2021 bajeti ya *TARURA* ilikuwa ni shilingi bilioni 275 lakini wakati huu tunavyozungumza tunatarajia katika mwaka wa fedha 2025/2026 bajeti ya *TARURA* itakuwa ni shilingi trilioni 1.18. Kwa hiyo, unaona kabisa dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita kuendelea kuwekeza katika kuimarisha barabara hizi za muhimu.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili la bajeti linaonekana katika wilaya. Kila wilaya imepata nyongeza ya bajeti ya *TARURA* kwa ajili ya kuhudumia miundombinu ya barabara hizi za msingi kabisa za *TARURA*. Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Sophia Mwakagenda hata katika Wilaya ya Rungwe na yenyewe inanufaika na ongezeko la bajeti ambalo linalenga kwenda kuimarisha barabara hizi. Serikali itaendelea na jitihada hizi ili kuhakikisha wananchi wanapata barabara bora zaidi ambazo zinawawezesha kufanya shughuli zao za kiuchumi, lakini kufikia huduma za msingi za kijamii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Jimbo la Tarime Vijijini lina mvua nyingi, udongo ni tifutifu. Ni kwa nini Serikali isitoe maelekezo mahususi kwa bajeti hiyo hiyo iliyopo, lakini kule waweke changarawe wasiweke udongo hata kama ni kilometa moja, meta 500 ili mvua ikinyesha watu wasikwame kufanya shughuli za kiuchumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inahakikisha kwamba kila mwaka wa bajeti fedha zinapelekwa kwa ajili ya kuhudumia miundombinu ya barabara hizi muhimu kabisa za wilaya zinazosimamiwa na *TARURA*. Malengo ambayo yamewekwa na *TARURA* ni kuhakikisha kila mwaka kila wilaya inajengewa angalau kilometa moja ya lami, lakini pia kuna matabaka mengine ya barabara zetu hizi kwa maana ya changarawe na udongo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina lengo la kuhakikisha kwamba inaendelea kuongeza mtandao wa barabara za lami ambazo kimsingi zinaishi muda mrefu zaidi kuliko matabaka haya mengine. Vilevile Serikali itaendelea kuhakikisha inapeleka fedha za kutosha kwa ajili ya kuhakikisha tabaka la lami linaongezeka, lakini tabaka la changarawe linaongezeka zaidi kuliko tabaka la udongo kwa maana matabaka haya mawili yanaishi muda mrefu zaidi kuliko tabaka la udongo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mwita Waitara hata Tarime Vijijini lengo la Serikali ni kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara hizi za wilaya na hasa kwa matabaka ambayo yanaishi muda mrefu zaidi, Serikali italeta fedha kuhakikisha inaendelea kuimarisha miundombinu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa barabara nyingi za *TARURA* katika Wilaya ya Kilolo zimekuwa hazipitiki kabisa wakati wa mvua. Je, ni kwa nini Serikali isifanyie upembuzi yakinifu wa yale maeneo machache tu ambayo hayapitiki wakati wote ili zijengwe kwa kiwango cha zege?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikihakikisha inajenga miundombinu imara zaidi katika barabara zetu hizi za *TARURA* na lengo ni kuhakikisha kwamba barabara zinaishi muda mrefu zaidi, lakini zinapitika katika kipindi cha mwaka mzima. Serikali imekuwa ikifanya tathmini na kubaini maeneo ambayo ni korofi na kuweza kuyajengea miundombinu ambayo inaweza kustahimili mazingira ya mvua.

Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwamba huo ndio mpango wa Serikali, kwenye maeneo ambayo ni korofi Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa tabaka la lami na maeneo mengine tabaka la zege na Serikali itaendelea kufanya hivyo hata katika Jimbo la Kilolo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, *junction* ya Mayamaya - Mkondai paliharibika *box culvert* na kuvunja mawasiliano kati ya vijiji hivyo viwili, lakini Serikali tayari imeshapata mkandarasi na mkandarasi yule hajaripoti *site*.

Je, ni lini Serikali inaweza ikafanya aende haraka ili kuondoa huu mkanganyiko ambapo sasa hakuna mawasiliano ya kwenda kijiji kinachofuata?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwagiza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Dodoma akishirikiana na Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Bahi kuhakikisha kwamba mkandarasi huyu ambaye amepewa kazi ya ujenzi wa kazi hii ya dharura aweze kuripoti *site* na aweze kuanza utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii au matengenezo ya barabara hii haraka iwezekanavyo kwa mujibu wa mkataba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, sasa aulize swali lake.

Wewe ndiyo umefika keti, haya Mheshimiwa Condester Sichalwe.

Na. 693

**Hitaji la Bweni la Wasichana na Wavulana – Kimaiga Sekondari**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE K.n.y. MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga bweni la wasichana na wavulana katika Shule ya Sekondari ya Kimaiga, Kata ya Kihanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa shule kuwa na mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia ikiwemo uwepo wa mabweni. Hata hivyo, kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni ujenzi wa shule mpya za kutwa ili kupunguza msongamano wa wanafunzi na watoto kutembea mwendo mrefu na kuongeza nafasi katika shule za kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020/2021 - 2024/2025 Serikali imetumia shilingi bilioni 1.94 kujenga shule mbili za kata na mabweni sita katika Shule za Mgama, Kiponzelo na Weru kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za ujenzi wa miundombuni ya elimu kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kwa Jimbo la Mheshimiwa Jackson Kiswaga. Nina maswali mawili ya nyongeza ninayaelekeza kwenye Jimbo la Momba.

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo la Momba tuna sekondari 16 na sekondari zote hizi kuna changamoto ya mabweni. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuanza kutusaidia kutujengea mabweni angalau kwa kuanzia kwa shule tano kisha kuendelea na shule zingine?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa watoto wengi wanatembea mwendo mrefu na watoto wa kike wengi huahirisha masomo katika Jimbo la Momba kutokana kushindwa kuwatunza kwenye mabweni kwa sababu hakuna mabweni kabisa.

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa haraka na wa dharura angalau kuzisaidia shule kongwe kama Msangano, Chikanamlilo, Kapele, Momba, Uwanda na Ivuna ili zile ambazo zimechukua watoto wengi waweze kusaidika wasiendelee kutoroka kwenye shule? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya uwekezaji mkubwa sana katika sekta yetu hii ya elimu msingi na sekondari na ni dhahiri kutokana na utekelezaji wa Sera ya Elimu bila Malipo udahili wa wanafunzi umeongezeka maradufu na mazingira ya uhitaji miundombinu ya madarasa na shule zetu hizi umeongezeka; na ndio maana katika majibu ya msingi nimeeleza kwamba kipaumbele cha Serikali kwa wakati huu ni ujenzi wa shule mpya za kutwa pia ni ujenzi wa miundombinu itakayowezesha baadhi ya shule zetu hizi za kutwa ziweze kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Condester Sichalwe katika Jimbo lake la Momba anasema kwamba ana shule za

sekondari 16 na kwamba anahitaji shule angalau tano zijengewe mabweni ili ziweze kuwa ni shule za bweni. Sasa mpango wa Serikali kwa sasa shule zenye kuanzia kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne ni shule za kutwa ni shule za kata, kwa hiyo ndiyo maana hazijengewi miundombinu ya mabweni.

Mheshimiwa Spika, kwenye uhitaji kwa kukubaliana na wazazi pamoja na walimu wanakaa pamoja wanajadili na wanaweza kushirikisha wadau kwa ajili ya kujenga hosteli, lakini kipaumbele cha Serikali kwa wakati huu ni kuhakikisha shule za kata nyingi zinajengwa ili ziweze kupokea wanafunzi wengi zaidi ambao wamejitokeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili kwamba anahitaji mabweni kwenye shule hizi ili ziweze kuwasaidia wanafunzi wasichana wasikatize masomo yao kutokana na changamoto mbalimbali; jibu ni lilelile kwamba Serikali inaweka kipaumbele zaidi kujenga miundombinu ya shule ili shule hizi za kata za kutwa ziweze kupokea wanafunzi wengi ambao wamejitokeza, wanataka kupata elimu. Kwa mipango ambayo inakubalika Serikali, shule pamoja na wazazi wanaweza wakakaa wakakubaliana ili waweze kushirikisha wadau kujenga hosteli.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea…

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** ... kufanya uwekezaji mkubwa wa kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanapata miundombinu ya kusomea.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge maswali mafupi na Mheshimiwa Naibu Waziri majibu mafupi.

Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Tarime waliomba fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa bweni na bwalo kwenye Shule ya Msingi Magufuli ambayo ni maalum kwa watoto wenye uhitaji maalum. Je, lini Serikali italeta fedha hizi ili tuweze kujenga bweni hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiendelea kuimarisha miundombinu katika sekta hii muhimu ya elimu ya msingi na sekondari na imekuwa ikifanya uwekezaji maalum kabisa katika shule za watoto wenye mahitaji maalum. Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Esther Matiko kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, lakini kupitia Serikali Kuu kwa ajili ya kuhakikisha na kuja kujenga bweni na bwalo katika shule hii ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Jimbo la Tarime.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru, Shule ya Sekondari ya Mantare katika Jimbo la Sumve ina jiografia ambayo imezungukwa na milima hivyo kusababisha ugumu wa watoto kuwahi shuleni kwa muda muafaka na kusababisha utoro. Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kujenga bweni katika shule hii ili kurahisisha usomaji na ujifunzaji wa watoto hawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha Serikali kwa wakati huu ni kuhakikisha Serikali inaendelea kujenga shule mpya za kutwa ili ziweze kupokea wanafunzi wengi ambao wamejitokeza kwa ajili ya kupata elimu. Shule nyingi hizi za kata ni shule za kutwa, lakini kwa mpango maalum wazazi wakishirikiana na uongozi wa shule wanakaa na kushirikisha wadau

na kuamua kujenga hosteli. Serikali inapeleka fedha katika baadhi ya shule hizi za kata ili ziweze kujengewa miundombinu ikiwemo mabweni kwa ajili sasa ya kuanza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Kasalali katika Jimbo lake hili la Sumve kuwa Serikali kupitia mapato ya ndani pia kupitia utaratibu huu unaofanywa, fedha kutoka Serikali Kuu itaweka kipaumbele katika shule hii uliyoomba ijengewe miundombinu hii ili iweze kuwa na mabweni, hatimaye iweze kupokea wanafunzi pia wa kidato cha tano na sita.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ni lini fedha zitapelekwa Shule ya Bassodesh ambayo ni shule maalum kwa ajili ya watoto wa wafugaji na miundombinu yake imechakaa sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiendelea kuimarisha miundombinu katika sekta hii muhimu kabisa ya elimu msingi na sekondari na Serikali imekuwa ikitumia fedha za mapato ya ndani ikiwemo pia fedha za Serikali Kuu kwa ajili ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya shule zetu.

Mheshimiwa Spika, katika shule hii ya Bassodesh ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Hhayuma kwamba Serikali kupitia mapato ya ndani itafika katika shule hii kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inaikarabati iwe ina miundombinu mizuri ili iweze kuwanufaisha wanafunzi katika jimbo lako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, sasa aulize swali lake.

Na. 694

**Fedha za Kuweka Lami, Taa na Mifereji ya Barabara za Ndani - Dar es Salaam**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kutafuta fedha kama mikopo kuliko kutegemea Bajeti ya Serikali katika kuweka lami, taa na mifereji barabara za ndani Dar es Salaam?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto kubwa ya miundombinu ya barabara za ndani katika Jiji la Dar es Salaam, na kwa kutambua ufinyu wa bajeti ya ndani, Serikali imechukua hatua za makusudi za kutafuta vyanzo mbadala vya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya miji.

Mheshimiwa Spika, moja ya hatua ambazo Serikali imechukua ni utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam Awamu ya Pili *(DMDP II)* unaofadhiliwa kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia. Mradi huu unalenga kuboresha barabara za ndani, mifereji ya maji ya mvua, taa za barabarani na maeneo ya wazi.

Mheshimiwa Spika, katika Manispaa ya Kinondoni kilometa 58.14 zitajengwa kwa kiwango cha lami, pamoja na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua, njia za watembea kwa miguu, taa za barabarani zinazotumia nishati ya jua na kupandwa kwa miti pembezoni mwa barabara ili kuimarisha mazingira. Mradi umekwishaanza na utekelezaji unaendelea. Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kuhakikisha kuwa

miundombinu ya miji inaboreshwa ili kuchochea ukuaji wa kiuchumi, usalama na ustawi wa wananchi wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimesikia majibu ya Serikali ni kwamba pale Dar es Salaam barabara muhimu ambazo zilifanyiwa utafiti kwamba zijengwe ni kilometa 759 na kilometa ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri anazizungumza ni kama ni kama 30% tu na kwangu kwenye jimbo langu tutapata kilometa nne tu katika zote hizo anazozizungumzia.

Mheshimiwa Spika, swali langu, nini mipango ya Serikali kutafuta fedha nje ya Mradi wa *DMDP II* na fedha za bajeti ili kuweza kumaliza ujenzi wa barabara za ndani pale Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wewe ni shahidi kwamba pamoja na kwamba Serikali inajitahidi sana kujenga barabara, suala la ukarabati limekuwa ni sugu, mashimo ni mengi kila mahali na hata wakandarasi waotumika hawafanyi kazi vizuri.

Je, Serikali iko tayari kufanya utafiti ili sasa kubaini jukumu la utengenezaji na ukarabati wa barabara lipelekwe kwa halmashauri za miji yetu ili barabara zetu ziweze kuwa salama wakati wote? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali ya Awamu ya Sita imefanya jitihada za makusudi kabisa kupata mradi mahususi ambao utaendeleza miundombinu ya barabara katika Mkoa wa Dar es Salaam. Mradi huu wa *DMDP II* ni mradi ambao una gharama za jumla ya dola za Kimarekani 438 ikiwa ina lengo la kujenga kilometa 250 za barabara za lami, lakini mifereji ya maji ya mvua kilometa 90, vituo vya mabasi tisa, masoko 18 na ujenzi wa madampo matatu.

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na hoja ya Mheshimiwa Abbas Tarimba ninaomba nimfahamishe kwamba kupitia bajeti ya *TARURA* ambayo inaendelea kuimarika katika kila mwaka wa bajeti ukitazama tu katika kipindi cha miaka minne ya Awamu ya Sita zaidi ya shilingi bilioni 32.2 zimetumika katika Wilaya ya Kinondoni kwa ajili ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara zetu hizi.

Mheshimiwa Spika, mpango uliowekwa na Serikali ni kwamba kila wilaya katika nchi hii kwa maana ya Tanzania Bara kila mwaka wa fedha angalau ijengewe kilometa moja ya lami. Haitoshi hivyo, pia kupitia mapato ya ndani ya halmashauri Serikali imekuwa ikitenga fedha mahsusi kabisa kwa ajili ya kwenda kuimarisha miundombinu ya barabara zetu hizi za wilaya. Mathalani, nitoe pongezi kwa halmashauri hii ya Manispaa ya Kinondoni ambayo kupitia mapato ya ndani imeweza kununua mitambo ya kuchongea barabara. Pongezi kubwa sana kwako Mheshimiwa Mbunge, lakini pongezi kwa Manispaa ya Kinondoni kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, unatazama katika mwaka wa bajeti 2024/2025 ambayo Manispaa ya Kinondoni ina jumla ya mapato ya ndani shilingi bilioni 74; shilingi bilioni 5.6 zimeenda katika ujenzi wa kilometa 5.6 za barabara za lami ambazo tayari zimeshaanza kutekelezwa na zinakaribia kukamilika. Kuna kilometa 2.5 za lami ambazo bado zinaendelea kujengwa na zikikamilika jumla unaona hapo ni zaidi ya kilometa 7.5 ya lami zinakuwa zimejengwa kutokana na mapato ya ndani. Kwa hiyo, Serikali itaendelea na mikakati hii ya kuhakikisha kwamba kupitia miradi mahususi kama hii ya *DMDP,* bajeti ya *TARURA,* lakini mapato ya ndani inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya barabara hizi muhimu za wilaya.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusiana na kutenga fedha…

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri fupisha majibu ya swali la pili tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili la ukarabati wa barabara, Serikali inatenga fedha kila mwaka wa bajeti kupitia bajeti ile ya *TARURA* kuhakikisha inakarabati barabara zetu hizi, lakini kuna maelekezo mahsusi kabisa na hasa kwenye Halmashauri za Manispaa na Majiji kutenga fedha kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kuhakikisha inakarabati barabara hizi za wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niendelee kusisitiza maelekezo haya kuwa Wakurugenzi waweze kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha na wenyewe kwenye mapato ya ndani wanakarabati barabara zetu hizi za wilaya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, kuna mkakati gani kati ya *TARURA* na *TANROADS* kuhakikisha wanashirikiana kufanya hizi barabara za ndani ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam hasa Jimbo la Temeke?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya jukumu la pamoja la kushirikiana kwa maana ya Serikali nzima kama alivyoainisha Mheshimiwa Mbunge kwamba ushirikiano kati ya *TARURA* na *TANROADS,* Serikali imekuwa ikifanya hivyo ikishirikiana kuhakikisha kwamba inaendelea kuimarisha miundombinu ya barabara zetu hizi za wilaya, lakini pia barabara zetu hizi zenye hadhi ya kimkoa. Kwa maana *TANROADS* inahudumia mtandao wa barabara zenye hadhi mkoa na *TARURA* inahudumia barabara zenye hadhi ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha inaimarisha ushirikiano ili kwa pamoja kama Serikali kujenga barabara hizi na kuhakikisha miundombinu ya barabara inakuwa imara, wananchi

wetu waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi, lakini pia waweze kufikia huduma za msingi kabisa za kijamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, je, ni lini taa za barabarani zitafungwa katika Barabara ya Mwaya na ya Kidatu? Naishukuru Serikali kwa taa za Kibaoni Stendi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati maalum kabisa wa kuhakikisha katika barabara zinazojengwa hizi za lami zinajengwa pamoja na mifereji ya kutoa maji ya mvua, lakini pia zinajengwa na taa juu na Serikali imeanza kufanya hivyo katika ujenzi wa barabara zake kwa wakati huu na Serikali itaendelea na jitihada za kufikia barabara zetu hizi na kuhakikisha kwamba zinawekewa taa juu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Abubakari Asenga kwamba kwenye barabara alizozitaja za Mwaya za Kidatu, Serikali itafika kwa ajili ya kuhakikisha inaweka taa ili kuendelea kuboresha miundombinu ya barabara zetu hizi muhimu kabisa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maluum sasa aulize swali lake.

Na. 695

**Kuunganisha Barabara Kutoka Nyamilangano - Ushetu hadi Kaliua Tabora**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuunganisha barabara kutoka Nyamilangano – Ushetu hadi Kaliua Tabora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nyamilangano – Ushetu – Kaliua ni sehemu ya barabara ya Mpanda – Ugalla – Kaliua – Ulyankulu – Kahama yenye urefu wa kilometa 457. Kazi ya upembuzi yakinifu *(feasibility study)* wa barabara hiyo imekamilika na mkataba wa kumpata mhandisi mshauri kwa ajili ya usanifu wa kina umewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya upekuzi *(vetting)*. Kazi ya usanifu wa kina itachukua muda wa miezi 12. Baada ya usanifu wa kina kukamilika Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MH. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa usanifu wa kina utakamilika baada ya miezi 12; je, upatikanaji wa fedha na kuanza ujenzi utachukua miezi mingapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; barabara ya kutoka Kolandoto – Mhunze kwenda Mwangongo imekuwa ni kero kwa wananchi na majibu yamekuwa ni usanifu wa kina kila wakati. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga hii barabara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha usanifu ndipo tunapoweza kujua gharama ya barabara na tukishakamilisha maana yake ni kwamba tutaiweka kwenye mpango wa kuijenga hii barabara baada ya kuwa tumekamilisha usanifu. Kwa hiyo, tuna uhakika tunapofanya usanifu maana yake kinachofuata ni kutafuta fedha kuanza kuijenga hiyo barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Barabara ya Kolandoto – Mwangongo swali hili limejitokeza mara kadhaa na tumeshasema tumekamilisha usanifu na katika mpango wa bajeti wa mwaka huu barabara hiyo imepangiwa fedha kwa ajili ya maandalizi ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Barabara ya Mlongoji kwenda Lulanga, mkandarasi anayejenga amesimama kwa muda mrefu inapata mwaka sasa ambayo inaunganisha Mkoa wa Singida na Tabora.

Je, ni lini Serikali itampa pesa mkandarasi huyu ili arudi barabarani na iweze kupitika vizuri? Maana yake sehemu wanayopita wananchi sasa ni mbaya kuliko kiasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimwelekeze Meneja wa Mkoa wa Singida kuhakikisha kwamba barabara hiyo inapitika kwa sababu ni wajibu wa mkandarasi aliyepo *site* kuhakikisha barabara ambayo anaijenga inapitika, lakini kuhusu upatikanaji wa fedha nimhakikishie

Mbunge tulishapokea hati za madai na tulishaziwakilisha Hazina kwa ajili ya kumlipa huyo mkandarasi ili aweze kuendelea na kazi, ina maana tutakapopata hiyo fedha tutamlipa ili aweze kurejea *site* na kuanza kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA: SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo sasa aulize swali lake.

Na. 696

**Ujenzi wa Barabara ya Laela – Mwimbi hadi Matai**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami barabara kutoka Mji Mdogo wa Laela – Mwimbi hadi Matai kuunganisha na Barabara ya Kasanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, maandalizi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Laela – Mwimbi – Kizombwe (Matai) yenye urefu wa kilometa 92 yameanza ambapo zabuni kwa ajili ya kumpata mhandisi mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni ipo katika hatua ya kufanyiwa upekuzi *(vetting)*.

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinatarajiwa kuchukua kipindi cha mwaka mmoja baada ya mkataba kusainiwa. Usanifu utakapokamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya kututia matumaini ya Serikali naomba nielewe; je, kuna uwezekano wa kufupisha muda ili badala ya kutumika mwaka mzima katika kufanya hicho ambacho kinasemwa na Serikali ikatumika muda mfupi zaidi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri anaijua vizuri barabara ya kutoka Matai kwenda *Kasesha boarder* Zambia mpaka sasa hivi mkandarasi hayupo kwa sababu hajalipwa fedha. Je, Serikali ipo tayari kuhakikisha kwamba inamlipa fedha ili arudi kumalizia kazi ile? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kandege, Mbunge wa Kalambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati wa kufanya usanifu vigezo vyote vimekuwa vimeangaliwa kwamba barabara hii itachukua muda gani. Kwa hiyo, kwa wataalam walivyokadiria itachukua mwaka mmoja labda kutokee mazingira mengine inaweza ikaongezeka ama ikapungua kulingana na mazingira, lakini kwa upande wa watalam ni mwaka mmoja kwa maana ya miezi 12.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Barabara ya Matai – Kasesha tulisema katika bajeti lakini pia Wizara ya Fedha imesema kwamba miradi yote ambayo ilikuwa imesimama fedha itaanza kulipwa ili kazi ziendelee ikiwa ni pamoja na barabara hii ya Matai – Kasesha. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacquline Ngonyani Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona; ni lini Serikali itajenga Barabara ya Kigonsera – Matili – Mbaha yenye urefu wa kilometa 56 ni barabara ambayo

inakwenda nyumba kwa Makamu wa Rais ajaye Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, moja ni kwamba usanifu tumeshafanya wa barabara hii, lakini pia barabara hii inapita kwenye miinuko, maeneo mengi korofi tumeshayajenga kwa kiwango cha zege, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunatafuta fedha ili hiyo barabara iweze kujengwa yote kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Barabara ya Lyazumbi – Kabwe – Poti – Namanyeni – Kipili - Poti lini zitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nimshukuru Mheshimiwa Aida Khenani amekuwa anaulizia barabara hii. Hii barabara tumeshaifanyia usanifu na inaenda kwenye Bandari ya Kabwe, lakini tulichofanya tumekuwa tunasema wakati tunatafuta fedha kuijenga yote ilikuwa kwanza kuimarisha makalavati na madaraja ili yaweze kupitisha magari makubwa yanayokwenda bandarini wakati Serikali inatafuta fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali inatafuta fedha ili tuweze kuijenga hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami kwa sababu tumeshawekeza kwenye Bandari ya Kabwe ili iweze kufanya kazi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, barabara ya kutoka Mwanza Mjini kuelekea Usagara kupitia Kata za Buhongwa – Butimba – Mkuyuni – Igogo inaendelea kuwa finyu sana na tunazo taarifa kwamba mkandarasi alishapatikana. Kutokana na Daraja la JPM kukamilika *traffic* imekuwa kubwa sana na barabara hii inaingiza magari zaidi ya 15,000 kwa siku.

Sasa Serikali haioni umuhimu wa haraka kuhakikisha kwamba mkandarasi anatangazwa ili aanze kazi mara moja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mabula, Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua ni kweli Mji wa Mwanza umepanuka na magari yameongezeka na ndiyo maana Serikali ilishapanga kujenga njia nne kutoka Mwanza – Igogo – Nyegezi – Buhongwa hadi Usagara kwa njia nne na tunavyoongea sasa hivi tuko kwenye majadiliano na mkandarasi ambaye ataijenga hiyo barabara. Kwa hiyo, tunafahamu na hiyo barabara ipo kwenye mpango kuanza kuijenga mara moja na ndiyo maana mkandarasi ameshapatikana tuko kwenye majadiliano naye. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, barabara ambayo inakwenda kwenye visima vya gesi barabara ya uchumi na barabara ya ulinzi lini zitajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara aliyoitaja ni muhimu kiuchumi na tumeshaipangia fedha kwa ajili ya kufanya maandalizi ya kuijenga, lakini kwa maana ya

usanifu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumeshaikamilisha tunatafuta fedha tuanze kuijenga sasa yote kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Kwa majibu… hee!

Naona kuna Wabunge wameamua kusimama baada ya, hamkusimama awali Waheshimiwa kwa hiyo mniwie radhi sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula kwa niaba yake.

**MHE. KABULA E. SHITOBELA:** Mheshimiwa Spika, nipo. Ahsante kwa…

**SPIKA:** Subiri kwanza.

Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 697

**Uhitaji wa Watumishi wa Afya Hospitali ya Bugando na Sekou Toure**

**MHE. KABULA E. SHITOBELA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaongeza wataalam wa afya katika Hospitali ya Bugando na Sekou Toure kwa kuwa kuna upungufu mkubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni, 2025 Serikali imeajiri watumishi wapya 175 katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando na watumishi 79 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekou Toure hivyo kuendelea kupunguza upungufu uliopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa kibali cha ajira za watumishi wa kada mbalimbali 144 kwa Hospitali ya Kanda Bugando ambapo taratibu za ajira zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, swali la nyongeza.

**MHE. KABULA E. SHITOBELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali bado kuna upungufu hasa kwa wagonjwa wa saratani; lini sasa Serikali itatuongezea wataalam zaidi katika hospitali hizo mbili za Sekou Toure na Bungando hasa wataalam wa saratani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kwa sekta ya afya kwa kipindi hiki chote alichokuwepo Bungeni, lakini nimwambie ni kweli kwenye Idara ya Kansa ambayo Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye eneo hilo kwa hospitali tu ya Bugando amewekeza shilingi bilioni 12 na vifaa na sasa rufaa za kutoka Bugando kwenda *Ocean Road* zimepungua, wanaoenda *Ocean Road* ni chini ya asilimia moja, maana yake sasa watu wengi wanabaki kule Kanda ya Ziwa kwa ajili ya uwekezaji uliopo.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge katika nafasi 144 ambazo zimepangwa hapa tutafikiria zaidi na

tutaelekeza kwenye maeneo yale ambayo yana mapungufu kama hilo eneo ambalo umelisema la kansa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Manispaa ya Ilemela ina upungufu wa wauguzi 111 kati ya 205 wanaotakiwa; wa teknolojia 33 kati ya 40 wanaotakiwa pamoja na wataalam wa dawa 11 kati ya 34 wanaotakiwa; je, ni lini manispaa hii itapata wataalam hawa ili waweze kufanya kazi yake vizuri ukizingatia tuna hospitali ya wilaya sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kweli kuna upungufu maeneo mbalimbali hasa inatokana na upungufu halisi, lakini ni kwa sababu wakati mwingine wamesema hospitali ya wilaya inahitaji kiasi hiki, hospitali ya mkoa inahitaji kiasi hiki bila kuangalia *load* yaani namba ya wagonjwa. Nakubalina na wewe kwa Mwanza inawezekana ikawa ni kweli kwa sababu ni mjini na kuna watu wengi upungufu huo ukawepo, lakini nikuhakikishie tu katika ajira ambazo zinapangwa sasa tunatakiwa kwenda kuangalia siyo tu kuangalia hii ni hospitali ya wilaya, hiki ni kituo cha afya hii ni nini tunaenda kuangali je, hawa watu kwa siku wanahudumia wagonjwa wangapi? Wagonjwa ni wangapi wanaolazwa halafu tunaamua kupeleka kwa sababu tumekuja kugundua kuna vituo vya afya vinatibu wagonjwa wengi kwa siku kuliko hata hospitali ya wilaya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, niishukuru Serikali; Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara imejengwa katika Jimbo letu la Babati Mjini na wataalam hao wamekuwa wakifanya vizuri kuwahudumia

wananchi wetu, lakini tatizo kubwa linalolalamikiwa ni gharama kubwa ya matitabu ni gharama kubwa sana. Je, Serikali ipo tayari kwenda kuchunguza ni kwa nini matibabu haya yamekuwa yakilalamikiwa na wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema jana, kwa kweli kwenye hospitali zetu za mikoa gharama za matibabu siyo kubwa kiasi hicho, lakini *specifically* Mheshimiwa Mbunge ninaomba mimi na wewe wiki ijayo ikiwezekana tukapitia pale tuone *specifically* kwa maana ya hospitali yako ya Mkoa wa Manyara ni nini walichokikosea kwenye *formula* ya kupanga bei mpaka sasa tufikie mahali ambapo watu wanalalamika kwamba bei ni ghali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mtakatifu Benedict ya *Ndanda Mission* ndiyo hospitali pekee kwenye Mkoa wa Mtwara na Lindi inayotoa huduma za kansa. Hata hivyo wana upungufu wa vifaa pamoja na wataalam; je, Serikali haioni haja ya kuwashika mkono ili waweze kutoa huduma hizo kwa uhakika wa kupunguza foleni ya watu wanaosafirishwa kuja Dar es Salaam kwa maana ya Muhimbili pamoja na *Ocean Road? (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kwamba tuna Hospitali ya Kanda ambayo iko Mtwara kwa maana ya ukanda huo ambayo Serikali imefanya uwekezaji mkubwa sana na pale sasa hivi kuna ujenzi mkubwa sana wa ghala la kuweka dawa na vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye hiyo hospitali ambayo sasa unaisema Mheshimiwa Mbunge ninakuomba tupitie mikataba yake na Serikali kwamba inasemaje na makubaliano yalikuwa nini, ni maeneo gani ambayo tulitakiwa tushirikiane, baada ya kujua hilo basi tushirikiane kwa mwongozo wa Mheshimiwa Waziri wa Afya ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza kwenda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na majibu ya Mheshimiwa Waziri ya kufuatilia mikataba na vitu vingine, lakini tunayo njia nyepesi ya mkato ambayo tunaweza kuanza nayo na nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kupitia Wizara tutashirikiana na Menejimenti ya Hospitali, tutengeneze mpango mkakati wa *outreach program* tupeleke madaktari wetu bingwa kutoka *Ocean Road* wakaone ni namna gani haraka sana ikiwezekana mwezi wa saba ama wa nane wanaweza kukutana na wataalam wetu pale na wakaweka kambi ya kuanza kufuatilia namna nzuri ya kuweza kuondoa tatizo hilo la matibabu ya kansa hapa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nitaleta tangazo nililonalo hapa kabla hatujaendelea na ratiba yetu.

Tutaanza na wageni wangu; kwanza ni Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk ambaye ni Balozi wetu mteule nchini Italia, karibu sana. Haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Balozi Mbarouk tunakutakia kila la kheri katika utumishi wako nchini Italia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni wengine ambao ni Shirika la *Stoma Care Tanzania* kutoka Jijini Dar es Salaam, yupo Ndugu Khalid Gongoro ambaye ni Mwenyekiti, Ndugu Hassan Kapilima – Katibu, na Ndugu Hussein Waziri - Mhazini. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 27 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hawa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Ruangwa, Mkoani Lindi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, hawa ni wageni 25 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko - Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, hawa ni wazee kutoka Mkoa wa Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ambao ni Dkt. Tausi Kida - Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; ba Dkt. Josephine Kimaro huyu anatoka Taasisi ya Afisi ya Rais, Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini, Zanzibar, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Dkt. Fred Msemwa - Katibu Mtendaji Tume ya Taifa ya Mipango; yupo Dkt. Mursali Milanzi - Naibu Katibu Mtendaji Tume ya Mipango; Dkt. Blandina Kilama - Naibu Katibu Mtendaji; Dkt. Linda Ezekiel - Naibu Katibu Mtendaji; na Ndugu Angela Shayo - Kaimu Mkurugenzi - Idara ya Mipango Kitaifa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wenu Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni 47 wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde - Waziri wa Madini, hawa ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Cosato David Chumi - Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, hawa ni wadogo zake kutoka Mafinga, Mkoani Iringa. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho, huyu ni ndugu yake ambaye ni mtoto wa mdogo wake kutoka Jijini Mwanza anaitwa Ephrahim Chamuriho. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba, na hawa ni ndugu zake kutoka Mkoani Mtwara. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ambaye ni Ndugu Hagai Warioba Komba - Daktari wa Mifugo kutoka Mkoani Mara. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mwandishi wa Habari kutoka Jijini Dar es Salaam ambaye ni Ndugu Kelvin Justine. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Ndugu Rose Mzee rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ambao ni Dkt. Dalaly Kafumu - Mbunge Mstaafu, ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa mtu akiwa ameitwa Mbunge Mstaafu ni kwamba hagombei, sasa kwa sababu sijajua kama anagombea au hagombei basi mimi nitasema Dkt. Dalaly Peter Kafumu ambaye alikuwa Mbunge ili nisijiweke mazingira tatanishi. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Abdula Rashid ambaye anatoka UVCCM Geita, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi ambao ni viongozi wa Halmashauri, Kata na Vijiji kutoka Mlimba, Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ambao ni viongozi wa wachimba madini kutoka Mkoani Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Maganga anao wageni wengine wanne ambao ni watumishi wa Mungu kutoka Mikoa ya Shinyanga na Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 26 wa Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle ambao ni Maafisa Watendaji Kata, wafanyabiashara na Afisa Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoka Halmashauri ya Mkoani Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 26 wa Mheshimiwa Keneth Nollo ambao ni Makatibu wa UVCCM kutoka Bahi Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wengine 15 wa Mheshimiwa Nollo na wao wanatoka Bahi Kata ya Mayamaya, Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau ambao ni viongozi wa CCM kutoka Mkoani Mara. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ambao ni marafiki zake kutoka Mikoa ya Arusha. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Janeth Elias Mahawangwa ambaye ni Ndugu Zahra Mohamed ambaye ni mdogo wake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Ali Juma Mohamed ambao ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Shaurimoyo, Mjini Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Mheshimiwa Amina Bakar Yussuf ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni 14 wa Mheshimiwa Ally Juma Makoa ambao ni wanafunzi Chuo cha Biblia Kondoa Mjini, Mkoani Dodoma, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati ambao ni familia yake kutoka Kilolo, Mkoani Iringa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka ambaye ni Jennifer Kemilembe, mtumishi wa Halmashauri ya Chunya kutoka Mkoa wa Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao Bungeni. Sasa tutaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO YA BUNGE

### Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(Agreement for the Establishment of the Africa Finance Corporation – AFC)*

**na**

### Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote niwapongeze sana timu ya wananchi Yanga kwa kuwa bingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizo za jana ni dhahiri sasa mtoto aliyeanza *form one* mpaka amemaliza *form four* hajaona Simba akiwa bingwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ninaomba kuwasilisha Azimio la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika wa mwaka 2007 *(The Agreement for the Establishment of Africa Finance Corporation)*.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Azimio la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika wa mwaka 2007, Ibara ya 19(3) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika unaozitaka nchi zinazojiunga na shirika hilo baada ya kusainiwa kwa mkataba kuwasilisha hati ya kuridhia masharti ya mkataba huo. *(instrument of ratification)*.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(Africa Finance Corporation - AFC)* ulisainiwa tarehe 28 Mei, 2007. Shirika hili ambalo makao yake makuu yapo nchini Nigeria, linamilikiwa kwa ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma. Sekta ya umma inamiliki 59% ya hisa zote na sekta binafsi inamiliki 41% ya hisa zote.

Mheshimiwa Spika, aidha, umiliki wa sekta binafsi unajumuisha umiliki wa asilimia mbili kwa pamoja wa mashirika ya kimataifa ambayo ni Benki ya Maendeleo ya Afrika na Shirika la Bima la Afrika. Hadi Mei, 2025 nchi 44 za Afrika zimejiunga na shirika hilo na kati ya nchi hizo, nchi 28 zimejiunga kama wanachama pekee na nchi 16 zimejiunga kama nchi wanahisa.

Mheshimiwa Spika, nchi ambazo zinamiliki hisa ni pamoja na Nigeria na mashirika yake kupitia Benki Kuu ya Nigeria yenye hisa za

38.3%, Angola 0.54%, Benin 0.06%, Botswana 0.06%, Cape Verde 0.03%, Cote d'Ivoire 0.31%, DRC 0.16%, Misri 3.73%, Gabon 1.64%, Ghana 1.05%, Guinea 0.03%, Kenya 0.11%, Mauritius 0.61%, Sierra Leone 0.07%, Togo 0.16% na Zimbabwe 0.03%.

Mheshimiwa Spika, nchi ambazo zimejiunga kama wanachama pekee ni Ethiopia, Guinea-Bissau, Burkina Faso, Burundi, Comoros, Congo Brazzaville, Gambia, Liberia, Jamhuri ya Madagascar, Malawi, Mali, Mauritania, Morocco, Namibia, Niger, Rwanda, Sao Tome na Principe, Senegal, Somalia, Jamhuri ya Sudan Kusini, Tunisia, Uganda, Zambia, Chad, Djibouti, Eritrea na Eswatini.

Mheshimiwa Spika, katika vipindi tofauti, Shirika la Afrika limetoa mwaliko kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujiunga na shirika hilo ili kunufaika na fursa mbalimbali za kifedha kwa Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madhumuni ya uanzishwaji wa *AFC* ni kuziwezesha nchi wanachama kupata fedha kwa ajili ya uwekezaji, kuwezesha biashara ndani na nje ya Afrika, kuchangia katika maendeleo ya kisekta, mathalani nishati na uzinduaji, kutoa mikopo ya kibiashara taasisi za kifedha za Afrika pamoja na kujihusisha na shughuli nyingine za kibenki kwa lengo la kukuza uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kigezo kimojawapo cha kunufaika na mikopo na dhamana inayotolewa na *AFC* ni nchi kuwa mwanachama pekee au mwanachama mwenye hisa katika shirika hilo. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapendekeza kujiunga kama mwanachama pekee bila kununua hisa kwa wakati huu.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu una Ibara 21, ninaomba nielezee maudhui ya baadhi ya ibara kwa kifupi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3 ambayo ni Shughuli za Shirika; ibara hii imebanisha shughuli za *AFC* zikiwemo utoaji wa mikopo kwa ajili ya uwekezaji, kuwezesha biashara za ndani na nje ya Afrika,

kuchangia katika maendeleo ya sekta ya nishati na uzinduaji *(extractive industries)*, usafirishaji na ugavi, mawasiliano, viwanda vikubwa, kutoa mikopo kwa taasisi za kifedha za Afrika pamoja na kujihusisha na shughuli nyingine za kibenki kwa lengo la kukuza uwekezaji wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, aidha, ibara hii inatoa fursa kwa sekta ya umma na sekta binafsi kupata mikopo kutoka *AFC*. Uwepo wa fursa hii utaongeza upatikanaji wa mikopo na kuongeza mitaji kwa sekta binafsi, upatikanaji wa fedha za kigeni na ushindani kwa taasisi za fedha nchini.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5 ambayo hii inahusu uanachama imebainisha masharti ya uanachama ambapo nchi inaweza kuwa mwanachama ikiwakilishwa na Benki Kuu katika masuala yote yanayohusiana na mkataba wa *AFC*. Aidha, sekta ya umma au binafsi inaweza kuwa mwanachama na kununua hisa katika shirika hilo. Nchi inayotaka kujiunga na *AFC* itapaswa kuwasilisha hati ya kuridhia masharti ya mkataba wa uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ibara ya 7 inahusu kinga ya misamaha na upendeleo wa kidiplomasia kwamba nchi itakayojiunga na shirika hilo itatakiwa kuipa *AFC* hadhi, kinga, misamaha na upendeleo wa kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 8 inahusu kinga dhidi ya msamaha ya mashtaka na kwamba *AFC* haiwezi kushtakiwa na nchi mwanachama, mwanahisa au mtu yeyote kuhusu masuala ambayo yanasimamiwa na mikataba hususan au masuala binafsi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 inahusu kinga dhidi za upekuzi, ukamataji, utaifishaji wa aina nyingine zote au kukamata, kuchukua au kuzuiliwa kwa mali za *AFC* kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi mwanachama. Kwa upande wa Ibara ya 10 inahusu uhuru wa shughuli za *AFC* ambapo nchi mwanachama anapaswa kuondoa vizuizi vya usimamizi vinavyohusu masuala ya fedha na shughuli za *AFC*.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 11 inahusu kinga ya nyaraka za *AFC* dhidi ya upekuzi na kutolewa, isipokuwa pale nyaraka zinapohitajika na mahakama au mashauri ambayo *AFC* inahusika. Ibara ya 12 inahusu upendeleo wa mawasiliano ya kiofisi ya Shirika la *AFC* ambapo mawasiliano hayo yatachukuliwa kuwa ni mawasiliano ya Taasisi ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13 inahusu kinga, upendeleo na misamaha ya kodi zote kwa watumishi, wawakilishi, wakurugenzi, viongozi na washirika wa *AFC,* wakiwemo Watanzania wakati wakitekeleza yao kwenye *AFC*. Ibara ya 14 inahusu uondoaji wa kinga na upendeleo ambapo Bodi ya Wakurugezi na Mtendaji Mkuu wa *AFC* wanayo mamlaka ya kuondoa kinga na upendeleo kwa Mtendaji Mkuu na watumishi au washauri waelekezi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ibara ya 15 inahusu misamaha ya kodi ambayo imebainisha ulazima wa nchi kutoa msamaha au ushuru wa forodha wa kodi zote za *AFC,* mali, mapato, shughuli zote na uendeshaji wa fedha za *AFC*, ikiwemo mawakala wanaofanya malipo kwa *AFC* kupewa msamaha wa kodi zilizopo katika sheria za nchi au zitakazoainishwa baadaye katika Sheria za Kodi.

Mheshimiwa Spika, misamaha hiyo ni pamoja na msamaha wa kodi kwenye mali, akiba, mtaji, gawio, mikopo wa dhamana, uwekezaji, riba, malipo ya uwakala, faida, ada, mapato, fedha zinazopatikana au mapato yanayotokana na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19(3), hati ya kuridhia mkataba; katika upande huu ibara hii inazitaka nchi wanachama zitakazojiunga baada ya mkataba kusainiwa, ziwasilishe hati ya kuridhia mkataba kwa mujibu wa Katiba au mamlaka ya nchi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matokeo na faida za kuridhia Mkataba wa *AFC* ni kwamba Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa kuridhia mkataba huu itaweza kunufaika katika masuala mbalimbali ikiwemo: -

(a) Kuongezeka kwa wigo wa mikopo kwa ajili ya uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema juzi tunapoongelea mikopo hatumaanishi mikopo ya Serikali, hapa tunamaanisha sekta binafsi zikiwemo benki, kampuni zinazofanya kazi hapa nchini ambayo yanahitaji kukuza mitaji.

(b) Taasisi za fedha za ndani kunufaika na fedha kutoka katika Shirika la *AFC* ambazo zitatumia kutoa mikopo kama ambavyo nimetoka kusema kwa sekta mbalimbali za kiuchumi *(on-lending* na *refinancing facilities);*

(c) Kukuza ajira nchini kwa kuwa taasisi zitakazonufaika na mikopo zitaajiri wafanyakazi katika sekta binafsi na Serikalini na kuipatia Serikali mapato ya kodi.

(d) Kuwezesha upatikanaji wa misaada na ushauri wa kitaalamu katika kuandaa, kufadhili na utekelezaji wa miradi na programu za mbalimbali maendeleo; na

(e) Kuvutia uwekezaji nchini kutokana na taasisi hiyo kuwa na baadhi ya *A3 rated* katika huduma za kimikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mambo ya kuzingatia wakati wa kuridhiwa Mkataba wa Uanzishwaji wa *AFC*, Serikali inapendekeza kuweka mazingatio ambayo tumesema tutakuwa na mazingatio katika baadhi ya maeneo ambayo tumeyabainisha katika kipengele cha 3, 5, 13, na 14. Inapendekezwa kwamba tutakuwa na mazingatio katika maeneo ambayo tumeyaorodhesha.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kuwasilisha Azimio la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la

Fedha la Afrika wa mwaka 2007 *(Agreement for the Establishment of Africa Finance Corporation)* kama ifuatavyo: -

Kwa kuwa Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(Africa Finance Corporation – AFC)* ulisainiwa na kuanza utekelezaji wake tarehe 28 Mei, 2007 na Makao Makuu ni Lagos – Nigeria, shirika hili linamilikiwa kwa ubia baina ya sekta binafsi na umma. Sekta ya umma kupitia Benki Kuu ya Nigeria inamiliki 59% ya hisa zote na sekta binafsi inamiliki 41% ya hisa zote. Aidha, asilimia mbili ya hisa zinazomilikiwa na sekta binafsi zinamilikiwa kwa pamoja na mashirika ya Kimataifa ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* na Shirika la Bima la Afrika *(Africa Re-Insurance Corporation)*.

Kwa kuwa *AFC* ilianzishwa kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya viwanda kwa nchi za Afrika kama Bara na kwa nchi moja moja ambapo hadi Machi, 2025 jumla ya nchi 44 za Afrika zilikuwa zimejiunga na shirika hilo. Kati ya nchi hizo, nchi 28 zimejiunga kama wanachama pekee na nchi 16 zimejiunga kama wanachama wanahisa.

Kwa kuwa hadi Desemba, 2024 shirika lilikuwa na mali *(assets)* zenye thamani ya dola za Kimarekani shilingi bilioni 14.4 na hisa hizo na riba *(equity)* zenye thamani ya dola za Kimarekani shilingi bilioni 3.9, katika miradi mbalimbali Barani Afrika na katika sekta za miundombinu, nishati, uchukuzi, mawasiliano na viwanda. Kwa mujibu wa taarifa ya fedha ya mwezi Septemba 2024, tangu kuanzishwa kwake shirika hilo linagharamia dola za Kimarekani shilingi bilioni 14.79 katika miradi ya nchi wanachama 34.

Kwa kuwa katika vipindi tofauti kutoka mwaka 2021 *AFC* kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imekuwa ikiialika Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kujiunga na *AFC* ambapo pamoja na masuala mengine, maombi haya yametokana na baadhi ya wawekezaji nchini kuwasilisha maombi ya kupata mikopo kutoka katika shirika hilo bila mafanikio, kutokana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokuwa mwanachama.

Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia Mkataba wa Uanzishwajii wa *AFC* na kujiunga kama mwanachama pekee kunaweza kuiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupata manufaa mbalimbali ikiwemo kuvutia uwekezaji mpya.

Kwa kuwa endapo Mkataba wa *AFC* utaridhiwa, Serikali haitawajibika kudhamini mikopo inayotolewa na sekta binafsi nchini. Kwa upande wa mikopo itakayotolewa na *AFC* kwa taasisi za Serikali au miradi ya ubia, Serikali inaweza kudhamini mkopo huo kwa mujibu wa sheria zake.

Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo hazijasaini mkataba huo, inapaswa kuridhia mkataba huo ili iweze kunufaika na kuwezesha utekelezaji wa Mkataba na Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(Agreement for the Establishment of the Africa Finance Corporation – AFC)*.

Kwa kuwa kuridhia kujiunga na *AFC* kutaleta manufaa mbalimbali kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo: -

(a) Kuongezeka kwa wigo wa upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya uwekezaji;

(b) Kuwezesha sekta binafsi na taasisi za fedha za ndani kunufaika na fedha kutoka *AFC* ambazo zinatumika kukopesha sekta mbalimbali za kiuchumi *(on-lending* na *refinancing facilities)*;

(c) Kukuza ajira na mapato nchini kwa kuwa taasisi zitakazonufaika na mikopo hiyo zitaajiri wafanyakazi;

(d) Kuongezeka kwa mzunguko wa fedha katika uchumi, zikiwemo fedha za kigeni, kuwezesha upatikanaji wa ushauri wa kitaalam katika kuandaa, kufadhili na kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maendeleo; na

(e) Kuvutia uwekezaji nchini kutokana na taasisi hiyo kuwa na hadhi ya alama A *(A3 rated)* kufuatia tathmini iliyofanywa na taasisi ya *Moody's Ratings*.

Kwa kuwa matokeo yanayoweza kujitokeza ni pamoja na *AFC* kutoa mikopo kwa masharti ya kibiashara na hivyo kuwa na gharama kubwa ya mikopo ikilinganishwa na mashirika mengine yanayotoa mikopo kwa masharti nafuu, kupunguza wigo wa kodi kutokana na shirika hilo kuomba kusamehewa kodi.

Kwa kuwa Ibara ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Vienna wa mwaka 1969 inaruhusu nchi kuweka maangalizo ama *reservations*.

Kwa kuwa uchambuzi wa kina uliofanywa na Serikali umebaini maeneo hayo Ibara ya tatu pamoja na ibara zingine.

Kwa kuwa Ibara ya tano ya Mkataba wa Uanzishwaji wa *AFC* wa Uanachama *(membership)* Ibara ya 5(3) ya Mkataba inaainisha kuwa nchi inaweza kujiunga na Shirika la *AFC* kwa kununua hisa *(Membership of the corporation shall be acquired upon subscribing to the shares of the corporation in accordance with the provisions of this agreement)*.

Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikilipa gharama kubwa za uanachama katika Mashirika ya Kimataifa, inapendekezwa kuweka angalizo katika ibara hii kuwezesha nchi kujiunga pasipo kununua hisa kwa sasa *(It should not be a requirement to subscribe shares in the AFC organization in order to become a member)*. Angalizo hili limewekwa na nchi ya Liberia, Ethiopia na Somalia wakati zinaridhia mkataba wa kujiunga na shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa *AFC,* kinga binafsi, maendeleo, na misamaha ya kodi (*personal immunities, privileges and exemptions)*, Ibara ya 13(2) Mkataba wa Uanzishwaji wa *AFC* inatoa msamaha wa kodi ya Mtendaji Mkuu,

Mkurugenzi, Maafisa na wafanyakazi wa shirika hilo. Ibara hiyo inakinzana na kifungu cha saba ambacho tumeielezea katika Sura ya 332.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa *AFC,* (uondoaji wa kinga); ibara hii inahusu uondoaji wa kinga na upendeleo ambapo Bodi ya Wakurugezi wa *AFC* ina mamlaka ya kuondoa kinga.

Hivyo basi kwa kuwa na kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata kutokana na kuridhia mkataba huo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Tisa, na kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(An Agreement for the Establishment of the Africa Finance Corporation – AFC)* isipokuwa katika utekelezaji wa maangalizo ambayo tumeyaweka yakiwemo kwa kuanzia kujiunga bila kulipia hisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili Azimio hili na kuliridhia kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA MHE. DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI MAELEZO KUHUSU AZIMIO LA KURIDHIA MKATABA WA UANZISHWAJI WA SHIRIKA LA FEDHA LA AFRIKA WA MWAKA 2007 (AN AGREEMENT FOR THE ESTABLISHMENT OF AFRICA FINANCE CORPORATION OF 2007) - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ninaomba kuwasilisha Azimio la kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika wa mwaka 2007 (An Agreement for the Establishment of Africa Finance Corporation).

**Mheshimiwa Spika,** chimbuko la Azimio la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika wa mwaka 2007 ni Ibara ya 19(3) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika unaozitaka nchi zinazojiunga na Shirika hilo baada ya kusainiwa kwa mkataba kuwasilisha Hati ya kuridhia masharti ya mkataba huo (Instrument of Ratification).

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba wa uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika (Africa Finance Corporation - AFC) ulisainiwa tarehe 28 Mei, 2007. Shirika hili ambalo makao yake makuu yapo nchini Nigeria, linamilikiwa kwa ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma. Sekta ya Umma inamiliki asilimia 59 ya hisa zote na Sekta binafsi inamiliki asilimia 41 ya hisa zote. Aidha umiliki wa Sekta Binafsi unajumuisha umiliki wa asilimia 2 kwa pamoja wa mashirika ya Kimataifa ambayo ni Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Bima la Afrika (Africa Re-insuarance Corporation). Hadi Mei, 2025, nchi 44 za Afrika zimejiunga na Shirika hilo na kati ya nchi hizo, 28 zimejiunga kama wanachama pekee na nchi 16 zimejiunga kama nchi wanahisa.

**Mheshimiwa Spika,** nchi ambazo zinamiliki hisa ni pamoja na Nigeria na mashirika yake kupitia Benki kuu ya Nigeria yenye hisa za asilimia

38.3, Angola asilimia 0.54, Benin asilimia 0.06, Botswana asilimia 0.06, Cape Verde asilimia 0.03, Cote de'Ivoire asilimia 0.31, DR Congo asilimia 0.16, Misri asilimia 3.73, Gabon asilimia 1.64, Ghana asilimia 1.05, Guinea asilimia 0.03, Kenya asilimia 0.11, Mauritius asilimia 0.61, Sierra Leone asilimia 0.07, Togo asilimia 0.16 na Zimbabwe asilimia 0.03. Nchi ambazo zimejiunga kama wanachama pekee ni: Ethiopia, Guinea-Bissau, Burkina Faso, Burundi, Comoros, Congo Brazzaville, Gambia, Liberia, Jamhuri ya Madagascar, Malawi, Mali, Mauritania, Morocco, Namibia, Niger, Rwanda, Sao Tome na Principe, Senegal, Somalia, Jamhuri ya Sudan Kusini, Tunisia, Uganda, Zambia, Chad, Djibouti, Eritrea, na Eswatini.

**Mheshimiwa Spika,** katika vipindi tofauti, Shirika la AFC limetoa mwaliko kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujiunga na Shirika hilo ili kunufaika na fursa mbalimbali za kifedha kwa Serikali na sekta binafsi.

## 2.0 MADHUMUNI YA MKATABA WA UANZISHWAJI WA SHIRIKA LA FEDHA LA AFRIKA (AFC)

**Mheshimiwa Spika**, madhumuni ya uanzishwaji wa AFC ni kuziwezesha nchi wanachama kupata fedha kwa ajili ya uwekezaji, kuwezesha biashara ndani na nje ya Afrika, kuchangia katika maendeleo ya sekta ya nishati na uziduaji (extractive industries), kutoa mikopo ya kibiashara kwa taasisi za kifedha za Afrika pamoja na kujihusisha na shughuli nyingine za kibenki kwa lengo la kukuza uwekezaji. Kigezo kimojawapo cha kunufaika na mikopo na dhamana inayotolewa na AFC ni nchi kuwa Mwanachama pekee au Mwanachama mwenye hisa katika Shirika hilo. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapendekeza kujiunga kama mwanachama pekee bila kununua hisa.

## 3.0 IBARA ZA MKATABA NA MAUDHUI YAKE

**Mheshimiwa Spika**, mkataba huu una Ibara 21 naomba nielezee maudhui ya baadhi ya Ibara kwa ufupi kama ifuatavyo: -

**Ibara ya 3: Shughuli za Shirika**

Ibara hii imebanisha shughuli za AFC zikiwemo utoaji wa mikopo kwa ajili ya uwekezaji, kuwezesha biashara ndani na nje ya Afrika, kuchangia katika maendeleo ya sekta ya nishati na uziduaji (extractive industries); Usafirishaji na Ugavi; Mawasiliano; Viwanda vikubwa; kutoa mikopo kwa taasisi za kifedha za Afrika pamoja na kujihusisha na shughuli nyingine za kibenki kwa lengo la kukuza uwekezaji Afrika.

Aidha, Ibara hii inatoa fursa kwa sekta ya umma na sekta binafsi kupata mikopo kutoka AFC. Uwepo wa fursa hii utaongeza upatikanaji wa mikopo na kuongeza mitaji (equity) kwa sekta binafsi, upatikanaji wa fedha za kigeni na ushindani kwa taasisi za fedha nchini.

**Ibara ya 5: Uanachama**

Ibara hii imebainisha masharti ya uanachama ambapo, nchi inaweza kuwa Mwanachama ikiwakilishwa na Benki Kuu katika masuala yote yanayohusiana na Mkataba wa AFC. Aidha, sekta ya umma au binafsi zinaweza kuwa mwanachama na kununua hisa katika Shirika hilo. Nchi inayotaka kujiunga na AFC itapaswa kuwasilisha Hati ya kuridhia masharti ya mkataba wa uanzishwaji wake.

**Ibara ya 7:** Ibara hii inahusu kinga ya misamaha na upendeleo wa kidiplomasia, na kwamba nchi itakayojiunga na Shirika hilo itatakiwa kuipa AFC hadhi, kinga, misamaha na upendeleo wa kidiplomasia.

**Ibara ya 8:** Ibara hii inahusu kinga dhidi ya mashtaka na kwamba, AFC haiwezi kushtakiwa na nchi mwanachama, mwanahisa au mtu yeyote kuhusu masuala ambayo yanasimamiwa na mikataba ya usuluhishi au masuala binafsi.

**Ibara ya 9**: Ibara hii inahusu kinga dhidi ya upekuzi, ukamataji, utaifishaji na aina nyingine zote za kukamata, kuchukua au kuzuiliwa

kwa mali za AFC kwa mujibu wa taratibu na Sheria za nchi mwanachama;

**Ibara ya 10:** Ibara hii inahusu uhuru wa shughuli za AFC ; ambapo nchi wanachama wanapaswa kuondoa vizuizi vya usimamizi vinavyohusu masuala ya fedha na shughuli za AFC;

**Ibara ya 11**: Ibara hii inahusu kinga ya nyaraka za AFC dhidi ya upekuzi au kutolewa isipokuwa pale nyaraka zinapohitajika na mahakama au mashauri ambayo AFC linahusika.

**Ibara ya 12**: Ibara hii inahusu upendeleo wa mawasiliano ya kiofisi ya Shirika la AFC ambapo mawasiliano hayo yatachukuliwa kuwa ni mawasiliano ya taasisi ya Kimataifa.

**Ibara ya 13**: Ibara hii inahusu kinga, upendeleo na misamaha ya kodi zote kwa watumishi, wawakilishi, wakurugenzi, viongozi na washirika wa AFC wakiwemo watanzania wakati wakitekeleza wajibu wa AFC.

**Ibara ya 14**: Ibara hii inahusu uondoaji wa kinga na upendeleo ambapo Bodi ya Wakurugezi na Mtendaji Mkuu wa AFC wana mamlaka ya kuondoa kinga na upendeleo kwa Mtendaji Mkuu watumishi au Mshauri elekezi mtawalia.

**Ibara ya 15: Msamaha wa Kodi**

Ibara hii imebainisha ulazima wa nchi kutoa msamaha wa ushuru wa forodha na kodi zote kwa AFC, mali, mapato, shughuli zote za uendeshaji na fedha za AFC, ikiwemo mawakala wanaofanya malipo kwa AFC kupewa msamaha wa kodi zote zilizopo katika sheria za nchi au zitakazoainishwa baadaye katika sheria za kodi. Misamaha hiyo ni pamoja na msamaha wa kodi kwenye mali, akiba, mtaji, gawio, mikopo, dhamana, uwekezaji, riba, malipo ya uwakala (commissions), faida, ada, mapato na fedha zozote zitakazopatikana au mapato kutokana na uwekezaji wowote utakaofanywa na AFC. Msamaha wa kodi utakaotolewa utakuwa

sehemu ya gharama za utekelezaji wa Mkataba endapo AFC itapata hadhi ya kidiplomasia.

**Ibara ya 19 (3): Hati ya kuridhia Mkataba**

Ibara hii inazitaka nchi wanachama zitakazojiunga baada ya mkataba kusainiwa, ziwasilishe hati ya kuridhia mkataba kwa mujibu wa Katiba au mamlaka za nchi husika.

## 4.0 MATOKEO NA FAIDA ZA KURIDHIA MKATABA WA AFC

**Mheshimiwa Spika,** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia Mkataba AFC itaweza kunufaika katika masuala mbalimbali ikiwemo:

a) Kuongezeka kwa wigo wa mikopo kwa ajili ya uwekezaji hapa nchini;

b) Taasisi za fedha za ndani kunufaika na fedha kutoka katika Shirika la AFC ambazo zitatumika kutoa mikopo kwa sekta mbalimbali za kiuchumi (on-lending na refinancing facilities);

c) Kukuza ajira nchini kwa kuwa taasisi zitakazonufaika na mikopo zitaajiri wafanyakazi na Serikali itapata mapato kupitia kodi.

d) Kuwezesha upatikanaji wa misaada na ushauri wa kitaalamu katika kuandaa, kufadhili na utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo;

e) Kuvutia uwekezaji nchini kutokana na taasisi hiyo kuwa na hadhi ya A3 rated katika huduma za mikopo ya kibiashara.

## 5.0 MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA KURIDHIA MKATABA

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kuridhiwa kwa Mkataba wa Uanzishwaji wa AFC, Serikali inapendekeza kuweka mazingatio (reservations) katika Ibara ya 3, 5, 13 na 14 kama ifuatavyo: -

**a) Ibara ya 3:** Inapendekezwa kuweka Angalizo (reservation) kuwa mikopo itakayotolewa na AFC iwe kwa ajili ya miradi ya maendeleo na ya muda mrefu kwenye maeneo ya miundombinu, miradi ya kimkakati na viwanda ili kulinda taasisi za ndani zinazotoa mikopo midogo na ya muda wa kati.

**b) Ibara ya 5:** inapendekezwa kuweka Angalizo katika ibara hii ili kuiwezesha nchi kujiunga kama mwanachama pekee ambaye halazimiki kununua hisa.

**c) Ibara ya 13:** Serikali inapendekeza kuweka angalizo (reservation) katika masharti ya ibara ya 13(2) ya Mkataba ili kuiwezesha nchi kutoza kodi kwa wafanyakazi watakaoajiriwa nchini Tanzania na Shirika la AFC au miradi inayofadhiliwa na Shirika hilo au wanahisa ambao ni wakazi (residents).

**d) Ibara ya 14:** Serikali inapendekeza kuweka angalizo katika ibara hii ili kuipa nchi Mamlaka ya kuondoa kinga na upendeleo badala ya mamlaka haya kuwa kwa bodi na mkurugenzi wa AFC.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha Azimio la kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika wa mwaka 2007 (Agreement for the Establishment of Africa Finance Corporation) kama ifuatavyo;

**KWA KUWA**, Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika (Africa Finance Corporation – AFC) ulisainiwa na kuanza utekelezaji tarehe 28 Mei, 2007 na Makao Makuu ni Lagos-Nigeria. Shirika hili linamilikiwa kwa ubia baina ya Sekta Binafsi na Umma. Sekta ya Umma kupitia Benki Kuu ya Nigeria inamiliki asilimia 59 ya hisa zote na Sekta binafsi inamiliki asilimia 41 ya hisa zote. Aidha, asilimia 2 ya

hisa zinazomilikiwa na sekta binafsi zinamilikiwa kwa pamoja na mashirika ya Kimataifa ambayo ni Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Bima la Afrika (Africa Re-insuarance Corparation).

**KWA KUWA,** AFC ilianzishwa kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya viwanda kwa nchi za Afrika kama Bara na kwa nchi moja moja ambapo hadi Machi, 2025 jumla ya nchi 44 za Afrika zilikuwa zimejiunga na Shirika hilo. Kati ya nchi hizo, 28 zimejiunga kama wanachama pekee na nchi 16 zimejiunga kama wanachama wanahisa.

**KWA KUWA**, hadi Desemba, 2024, Shirika lilikuwa na mali (assets) zenye thamani ya Dola za Marekani Bilioni 14.4 na hisa zisizo na riba (equity) zenye thamani ya Dola za Marekani Bilioni 3.9 katika miradi mbalimbali barani Afrika katika sekta za miundombinu, nishati, uchukuzi, mawasiliano na viwanda. Kwa mujibu wa taarifa ya fedha ya mwezi Septemba, 2024, tangu kuanzishwa kwake Shirika hilo limegharamia dola za Marekani bilioni 14.79 katika miradi kwa nchi wanachama 34.

**KWA KUWA**, katika vipindi tofauti kutoka mwaka 2021, AFC kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imekuwa ikiialika Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kujiunga na AFC ambapo pamoja na masuala mengine, maombi haya yametokana na baadhi ya wawekezaji nchini kuwasilisha maombi ya kupata mikopo kutoka katika Shirika hilo bila mafanikio kutokana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokuwa mwanachama wa AFC.

**KWA KUWA**, kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia Mkataba wa Uanzishwajii wa AFC na kujiunga kama mwanachama pekee kunaweza kuiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupata manufaa mbalimbali ikiwemo kuvutia uwekezaji mpya.

**KWA KUWA** endapo Mkataba wa AFC utaridhiwa, Serikali haitawajibika kudhamini mikopo inayotolewa kwa sekta binafsi

nchini. Kwa upande wa mikopo itakayotolewa na AFC kwa taasisi za Serikali au miradi ya ubia, Serikali inaweza kudhamini mkopo huo mujibu wa Sheria zake.

**KWA KUWA**, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo hazijasaini Mkataba huo, inapaswa kuridhia Mkataba huo ili iweze kunufaika na kuwezesha utekelezaji wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika (Agreement for the Establishment of the Africa Finance Corporation - AFC);

**KWA KUWA,** kuridhia kujiunga na AFC kutaleta manufaa mbalimbali kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo-

(a) kuongezeka kwa wigo wa upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya uwekezaji;

(b) kuwezesha sekta binafsi na Taasisi za fedha za ndani kunufaika na fedha kutoka AFC ambazo zitatumika kukopesha sekta mbalimbali za kiuchumi (onlending na refinancing facilities);

(c) kukuza ajira na mapato nchini kwa kuwa taasisi zitakazonufaika na mikopo zitaajiri wafanyakazi;

(d) kuongezeka kwa mzunguko wa fedha katika uchumi, zikiwemo fedha za kigeni; kuwezesha upatikanaji wa ushauri wa kitaalamu katika kuandaa, kufadhili na kutekeleza miradi na programu za maendeleo;

(e) kuvutia uwekezaji nchini kutokana na taasisi hiyo kuwa na hadhi ya alama A (A3 rated) kufuatia tathmini iliyofanywa na taasisi ya Moody's Ratings.

**KWA KUWA** matokeo hasi yanayoweza kujitokeza ni pamoja na:

(a) AFC kutoa mikopo kwa masharti ya kibiashara na hivyo kuwa na gharama kubwa ya mikopo ikilinganishwa na mashirika mengine yanayotoa mikopo kwa masharti nafuu; na

(b) kupunguza wigo wa kodi kutokana na Shirika hilo kuomba kusamehewa kodi zote.

**KWA KUWA,** Ibara ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Vienna wa Mwaka 1969 inaruhusu nchi kuweka angalizo (reservations) wakati wa kusaini au kuridhia mkataba pale ambapo Mkataba husika haujazuia kuwekwa angalizo (reservations). Pamoja na Mkataba wa AFC kutoweka kifungu kinachoruhusu reservations na kwa kuwa haujaweka kifungu kinachozuia, Ibara ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Vienna wa Mwaka 1969 inaweza kutumika kuweka maangalizo (reservations). Baadhi ya nchi zilizoridhia Mkataba wa AFC kwa kuweka maangalizo ni: Ethiopia, Somalia na Liberia.

**NA KWA KUWA,** uchambuzi wa kina uliofanywa na Serikali umebaini kuwa baadhi ya maeneo ya Mkataba huu yanakinzana na Sheria, Kanuni na Taratibu za masuala za kodi, ushindani na hadhi na kinga ya Kibalozi hivyo maeneo hayo yanayopaswa kuwekewa maangalizo (reservations) kama ifuatavyo:

**(a) Ibara ya 3 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa AFC: Majukumu ya AFC**

Ibara ya 3 ya Mkataba inaainisha kuwa Shirika la AFC litakuwa na majukumu ya kutoa mikopo kwa taasisi binafsi na kufanya shughuli zote za kibenki hapa nchini. Kwa kuwa kwa mujibu wa Ibara za 7 hadi 15 za Mkataba huo, Shirika hilo litapata upendeleo (privileges), hadhi ya kidiplomasia na misamaha ya kodi, masharti ya ibara hii yanakinzana na masharti ya ushindani wa kibiashara kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Ushindani, Sura ya 285. Hivyo inapendekewa kuweka angalizo (reservations) kuwa mikopo itatayotolewa na AFC inatakiwa kuwa ya maendeleo na muda mrefu katika miradi ya miundombinu, kimkakati na viwanda.

**"Loan provided by AFC should be developmental and long term in nature and should be directed towards major infrastructure, strategic and industrial projects".**

Angalizo hili pia limewekwa na nchi za Liberia na Ethiopia wakati zinajiunga na Shirika hilo.

**(b) Ibara ya 5 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa AFC: Uanachama (Membership)**

Ibara ya 5(3) ya Mkataba inaainisha kuwa nchi itajiunga uanachama wa Shirika la AFC kwa kununua hisa (Membership of the Corporation shall be acquired upon subscribing to the shares of the Corporation in accordance with the provisions of this Agreement). Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikilipa gharama kubwa za uanachama katika mashirika ya Kimataifa, inapendekezwa kuweka angalizo katika ibara hii ili kuwezesha nchi kujiunga pasipo kununua hisa.

**"It should not be a requirement to subscribe shares in the AFC organisation in order to become a member."**

Angalizo hili pia limewekwa na nchi za Liberia, Ethiopia na Somalia wakati zinaridhia Mkataba wa kujiunga na Shirika hilo.

**(c) Ibara ya 13 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa AFC: Kinga binafsi, upendeleo na misamaha ya kodi (Personal Immunities, Privileges and Exemptions)**

Ibara ya 13(2) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa AFC inatoa msamaha wa kodi kwa Mtendaji Mkuu, Mkurugenzi, Maafisa na wafanyakazi wa Shirika hilo. Ibara hii inakinzana na kifungu cha 7 cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 ambayo inaweka wajibu wa wafanyakazi kulipa kodi ya mapato katika malipo ya ujira isipokuwa kwa wale wenye hadhi ya kibalozi au kidiplomasia kwa mujibu wa aya ya 1(c) ya Jedwali la Kwanza la Sheria hiyo. Serikali inapendekeza kuweka angalizo katika masharti ya ibara ya 13(2) ya Mkataba ili nchi iweze kutoza kodi kwa wafanyakazi wa kitanzania watakaoajiriwa katika Shirika la AFC hapa nchini au miradi

inayofadhiliwa na Shirika hilo au wanahisa ambao ni wakazi wa Tanzania wasio na hadhi ya kibalozi au kidiplomasia.

**"Tanzania should have a right to tax Tanzanian employees of AFC or projects financed by AFC or shareholders who are residents of Tanzania who do not have consular or diplomatic status".**

Angalizo hili limewekwa pia na nchi za Liberia na Somalia wakati wa kuridhia Mkataba huo.

**(d) Ibara ya 14 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa AFC: Uondoaji wa Kinga (Waiver of Immunities)**

Ibara hii inahusu uondoaji wa kinga na upendeleo ambapo Bodi ya Wakurugezi wa AFC ina mamlaka ya kuondoa kinga na upendeleo. Aidha, Mtendaji Mkuu ana mamlaka ya kuondoa kinga na upendeleo kwa watumishi na wataalam elekezi wa AFC. Iwapo Serikali itajiunga, inashauriwa kuweka angalizo katika eneo hili kwa kuwa Ibara hii inakizana na kifungu cha 23 cha Sheria ya Hadhi na Kinga ya Kibalozi, Sura ya 356 ambacho kinampa mamlaka Waziri wa mambo ya nje kuondoa kinga iliyotolewa chini ya Sheria hiyo iwapo kuna sababu za msingi kufanya hivo.

Inapendekezwa kuweka angalizo katika ibara hii ili kuipa Mamlaka ya nchi uwezo wa kuondoa kinga na upendeleo.

**HIVYO BASI**, kwa kuzingatia manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata kutokana na kuridhia Mkataba huo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Tisa, na kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika (an Agreement for the Establishment of the Africa Finance Corporation - AFC) isipokuwa maangalizo katika Ibara ya 3, 5, 13(2) na 14 ya Mkataba huo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo haya naomba Bunge lako tukufu lijadili Azimio hili, na kuliridhia kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB.)**
**WAZIRI WA FEDHA**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, ahsanteni sana.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa niaba yake Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo.

**MHE. BAHATI K. NDINGO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninaomba Taarifa ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(Agreement for Establishment of the Africa Finance Corporation)*, kwa mujibu wa Ibara 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika la Fedha la Afrika *(Africa Finance Corporation)* lilianzishwa tarehe 28 Mei, 2007 kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya viwanda kwa nchi za Afrika. Kwa sasa makao makuu ya shirika hili yapo Lagos, Nigeria na

likiwa linamilikiwa kwa ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa Benki Kuu ya Nigeria inamiliki 59% ya hisa zote na sekta binafsi inamiliki 41% ya hisa hizo. Aidha, mpaka sasa jumla ya nchi 44 za Afrika sawa 81% zimekwishajiunga na shirika hilo. Kati ya nchi hizo, nchi 28 zimejiunga kama wanachama pekee na nchi 16 zimejiunga kama wanachama wanahisa.

Mheshimiwa Spika, katika nyakati tofauti Serikali imekuwa ikipata mwaliko wa kujiunga na shirika hili ili kunufaika na fursa mbalimbali za kifedha kwa Serikali na sekta binafsi. Hivyo, Azimio hili linalenga kuifanya Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kupata fursa hizo kwa sharti la kujiunga.

Mheshimiwa Spika, kulingana na ufafanuzi uliowasilishwa na Serikali kuhusu Azimio hili, Kamati inaunga mkono Azimio hili. Hata hivyo, inapenda kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Bunge lako Tukufu ili kuboresha Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake na kupatiwa maelezo ya Serikali kuhusu dhumuni la *AFC* kuwa ni: -

(i) Kuwezesha nchi ya Tanzania kupata fedha kiushindani kwa ajili ya uwekezaji;

(ii) Kuiwezesha nchi ya Tanzania kuwa na wigo mpana wa mashirikiano na taasisi za kifedha za Kimataifa katika masuala ya kifedha ikiwemo "*Credit Lines*;"

(iii) Kuchangia katika maendeleo ya sekta ya nishati na uziduaji *(extractive industries)*;

(iv) Kutoa mikopo ya kibiashara kwa taasisi za kifedha za Afrika pamoja na shughuli nyingine za kibenki kwa lengo la kukuza uwekezaji; na

(v) Kuwezesha mitaji ya kibiashara ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ili nchi iweze kufaidika na haya inatakiwa kujiunga kama mwanachama pekee au mwanachama mwenye hisa katika shirika hili. Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali, Tanzania inapendekeza kujiunga kama mwanachama pekee.

Mheshimiwa Spika, pamoja na malengo haya mazuri yanayoainishwa, Kamati ilipitia na kuchambua Ibara 21 za Mkataba unaohusika na uanzishwaji wa shirika ambazo zimepelekea kutoa maoni na ushauri ufuatao: -

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kuunga mkono Serikali kwa kuwa mwanachama pekee na sio mwanachama mwenye hisa katika shirika hilo. Hata hivyo, ili kuweza kufaidika zaidi na uanachama huu hapo baadaye, Serikali inatakiwa kuwa mwanachama wa hisa ili iweze kuwa sehemu ya umiliki wa taasisi hii ya fedha na hivyo kupata manufaa zaidi kama vile kushiriki katika vikao vya maamuzi, riba ndogo pamoja na kupata gawio la faida la mwanahisa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uhitaji wa Serikali kujiunga na shirika hili, Kamati inatoa angalizo la Serikali kuhakikisha Ibara za 7 hadi 15 ya Mkataba ambazo zinahusu kinga, upendeleo, na misamaha ya kikodi kwa Shirika la Fedha la Afrika *(Africa Finance Corporation – AFC)* pamoja na watumishi wake zinawekewa maangalizo *(reservation)* ili zisikinzane na sheria, kanuni na utaratibu wa nchi. Ni vema Serikali ikajifunza kwa nchi za Liberia, Ethiopia na Somalia ambazo zimejiunga na shirika hilo kwa kuweka angalizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa nchi ikiwemo sekta binafsi zina uhitaji mkubwa wa fedha za kugharamia miradi

mikubwa ya maendeleo pamoja na uwekezaji. Hivyo, kuwa mwanachama katika shirika hili itakuwa chachu ya kupata fedha za miradi ya maendeleo na ya muda mrefu kwenye maeneo ya msingi kama vile miundombinu ya nishati, pamoja na viwanda vya kimkakati na uwezekezaji katika sekta binafsi. Hata hivyo Kamati imeendelea kutoa angalizo kuwa mikopo itakayochukuliwa na Serikali izingatie sheria ya mikopo, dhamana na misaada ya Serikali *(Government Loans, Guarantees and Grants Act)*.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 16 ya mkataba imeainisha maeneo mengine ambayo nchi mwanachama anatakiwa kutoa upendeleo kwa shirika hili hasa katika masuala yanayohusu msamaha wa kifedha, msamaha katika vifaa vya kifedha na kusamehewa majukumu mengine sawa na inavyotolewa kwa mashirika mengine ya kimataifa na taasisi za fedha zenye hadhi ya kidiplomasia. Kamati inatoa angalizo kuwa ni vyema Serikali ikazingatia aina ya ukubwa wa mashirika au taasisi za kifedha zinazoingia nazo mikataba ili kuweza kupata upendeleo huo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18 inahusu utatuzi wa migogoro baina ya wanachama, shirika na mwanachama wa mkataba huu kuhusu tafsiri au matumizi ya kifungu chochote cha mkataba huu, itawasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Wanahisa wa Shirika na uamuzi wao utakuwa wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii bado Kamati inaona kuwa mwanachama wa kipekee bila kuwa mwanachama wa hisa inapunguza uwezo wa nchi kusimamia haki zake katika mkutano wa maamuzi kuhusu usuluhishi wa migogoro.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; ninapenda nichukue fursa hii kwanza kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika wa Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Umekuwa mlezi wetu mwema, umetuongoza vyema, umetupigania sana Wabunge wako, lakini umekuwa mfano bora wa viongozi wengi. Mimi sina shaka na wananchi wa Uyole, sina shaka, wanajua nini unastahili kwao kwa kuwa umewatumikia

kwa moyo wako wote na kwa akili zako zote na wao watakulipa. Sina mashaka hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu - Naibu Spika, kwa miongozo na hekima na umahiri wake kwenye Bunge letu Tukufu. Ninaamini kabisa Wana-Ilala watamlipa mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge na Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri na ushirikiano mzuri aliotupa kama Kamati. Bila shaka wana Iramba hawatamwangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Hamad Chande, Mbunge na Naibu Waziri; naye tunamshukuru kwa umoja na ushirikiano aliotuonesha Kamati. Naye bila shaka watu wa Kojani watamlipa mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda vilevile kumshukuru Dkt. Natu El-Maamry Mwamba - Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Ndugu Elijah Mwandumbya - Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Makamishna, wataalam wote wa Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa ushirikiano wao waliotupa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu ninapenda kumshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini. Kwa kweli baba huyu ni hazina kubwa kwa Taifa, ni mzalendo wa kweli na amekuwa akituongoza vizuri. Amekuwa ni mwalimu wetu mkubwa, busara zake na hekima zake zimeifanya Kamati hii kuwa ya kipekee na ya mfano kabisa. Ninaamini Mbeya Vijijini watamlipa wema mzee huyu ili tuendelee kuchota busara zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tunashukuru kwa ushirikiano aliotupa pia Makamu Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mheshimiwa Twaha

Mpembenwe kwa miongozo yao kwa kuisaidia Kamati na majukumu yake kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninawapongeza Wajumbe wenzangu wa Kamati. Kamati hii ina wachapakazi kweli kweli, ina wazalendo kweli kweli ambao wao kutoka usiku wa manane si tatizo kwao kwa ajili ya mapenzi na uzalendo mkubwa kwa Taifa lao. Mungu awabariki na ninaomba kuwatambue Wajumbe hao. Kwa kuzingatia muda ninaomba majina yao yote yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa ninaomba nimshukuru Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge, kwa niaba ya watumishi wote wa Bunge kwa kuwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Mbarali kwa namna ambavyo waliniamini wakanichagua na tumeweza kushirikiana vizuri tumefanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kama walivyoniamini kipindi kile wataniamini tena tuje tuendeleze kazi, kama ambavyo zimeanza. Kwa kweli, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, amerejesha tabasamu na matumaini makubwa sana kwa Wana-Mbarali na Wana-Mbarali pamoja na Taifa zima wanasema Oktoba tunakwenda kutiki, ili kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja nakushukuru sana. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA UANZISHWAJI WA SHIRIKA LA FEDHA LA AFRIKA *[AGREEMENT FOR THE ESTABLISHMENT OF THE AFRICA FINANCE CORPORATION – AFC]* – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika. *[Agreement for the Establishment of the Africa Finance CorporationAFC]* kwa mujibu wa Ibara 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**1.1. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Fedha la Afrika *[Africa Finance Corporation – AFC],* lilianzishwa tarehe 28 Mei, 2007 kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya viwanda kwa nchi za Afrika. Kwa sasa Makao Makuu ya Shirika hili yapo Lagos - Nigeria na linamilikiwa kwa ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma.

**1.2. Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonyesha kuwa Benki Kuu ya Nigeria inamiliki **asilimia 59** ya hisa zote na Sekta binafsi inamiliki **asilimia 41** ya hisa zote. Aidha, mpaka sasa jumla ya nchi 44 za Afrika (sawa **asilimia 81)** zimekwishajiunga na Shirika hilo. Kati ya nchi hizo, nchi 28 zimejiunga kama wanachama pekee na nchi 16 zimejiunga kama wanachama wanahisa.

**1.3. Mheshimiwa Spika,** Katika nyakati tofauti, Serikali imekuwa ikipata mwaliko wa kujiunga na Shirika hili ili kunuifaika na fursa mbalimbali za kifedha kwa Serikali na Sekta Binafsi. Hivyo, Azimio hili linalenga kuifanya Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kupata fursa hizo kwa sharti la kujiunga.

**1.4. Mheshimiwa Spika**, kulingana na ufafanuzi uliowasilishwa na Serikali kuhusu Azimio hili, Kamati inaunga mkono Azimio hili. Hata hivyo, inapenda kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Bunge lako Tukufu ili kuboresha Azimio husika.

## 2.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA UANZISHWAJI WA SHIRIKA LA FEDHA LA AFRIKA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake na kupatiwa maelezo ya Serikali kuhusu dhumuni la AFC kuwa ni:-

i) Kuiwezesha Nchi ya Tanzania kupata fedha kiushindani kwa ajili ya uwekezaji;

ii) Kuiwezesha nchi ya Tanzania kuwa na wigo mpana wa mashirikiano na Taasisi za Kifedha za Kimataifa katika masuala ya kifedha ikiwemo '*credit lines*';

iii) Kuchangia katika maendeleo ya sekta ya Nishati na uziduaji *(extractive industries);*

iv) Kutoa mikopo ya kibiashara kwa taasisi za kifedha za Afrika pamoja na shughuli nyingine za kibenki kwa lengo la kukuza uwekezaji; na

v) Kuwezesha mitaji ya kibiashara ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, ili nchi iweze kufaidika na haya inatakiwa kujiunga kama mwanachama pekee au mwanachama mwenye hisa katika Shirika hili. Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali, Tanzania inapendekeza kujiunga kama mwanachama pekee.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na malengo haya mazuri yaliyoainishwa, Kamati ilipitia na kuchambua Ibara 21 za Mkataba

unaohusika wa uanzishwaji wa Shirika ambazo zimepelekea kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

**2.1. Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua na kuunga mkono Serikali kuwa mwanachama pekee na sio mwanachama mwenye hisa katika Shirika hilo. Hata hivyo, ili kuweza kufaidika zaidi na uanachama huu hapo baadae Serikali inatakiwa kuwa mwanachama wa hisa ili iweze kuwa sehemu ya umiliki wa taasisi hii ya fedha na hivyo kupata manufaa zaidi kama vile kushiriki katika vikao vya maamuzi, riba ndogo pamoja na kupata gawio la faida la mwanahisa;

**2.2. Mheshimiwa Spika,** pamoja na uhitaji wa Serikali kujiunga na Shirika hili, Kamati inatoa angalizo la Serikali kuhakikisha kuwa Ibara ya 7 hadi 15 ya Mkataba ambazo zinahusu kinga, upendeleo na misamaha ya kikodi kwa Shirika la Fedha la Afrika *[Africa Finance Corporation – AFC]* pamoja na watumishi wake zinawekewa maangalizo *(reservation)* ili zisikinzane na sheria, kanuni na taratibu za nchi. Ni vema Serikali ikajifunza kwa nchi za Liberia, Ethiopia na Somalia ambazo zimejiunga na Shirika hilo kwa kuweka angalizo.

**2.3. Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa, nchi ikiwemo Sekta Binafsi zina mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kugharamia miradi mikubwa ya maendeleo pamoja na uwekezaji. Hivyo, kuwa mwanachama katika shirika hili itakuwa chachu ya kupata fedha za miradi ya maendeleo na ya muda mrefu kwenye maeneo ya msingi kama vile miundombinu ya nishati pamoja na viwanda vya kimkakati pamoja na uwezekezaji katika sekta binafsi. Hata hivyo Kamati inaendelea kutoa angalizo kuwa mikopo itakayochukuliwa na Serikali izingatie sheria ya mikopo, dhamana na Misaada ya Serikali *(Government Loans Gurantees and Grants Act)*.

**2.4. Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 16 ya mkataba imeainisha maeneo mengine ambayo nchi mwanachama anatakiwa kutoa upendeleo kwa Shirika hili hasa katika masuala yanayohusu msamaha wa kifedha, msamaha katika vifaa vya kifedha na kusamehewa majukumu mengine sawa na inavyotolewa kwa mashirika mengine

ya kimataifa na taasisi za fedha zenye hadhi ya kidiplomasia. Kamati inatoa angalizo kuwa ni vema Serikali ikazingatia aina na ukubwa wa mashirika au taasisi za kifedha inazoingia nazo mikataba ili kuweza kupata upendeleo huo.

**2.5. Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 18 inahusu utatuzi wa migogoro baina ya wanachama, Shirika na mwanachama wa Mkataba huu kuhusu tafsiri au matumizi ya kifungu chochote cha Mkataba huu kuwa itawasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa wanahisa wa Shirika, na uamuzi wao utakuwa wa mwisho. Kwa mantiki hii, bado Kamati inaona; kuwa mwanachama wa kipekee bila kuwa mwanachama wa hisa inapunguza uwezo wa nchi kusimamia haki zake katika mkutano wa maamuzi kuhusu usuluhishi wa migogoro.

**3.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kwanza kukushukuru wewe Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Mb, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), kwa miongozo yako na kunipa fursa kuwasilisha Azimio hili. Aidha, nimshukuru Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb), Naibu Spika, kwa hekima na uongozi wake mahiri katika Bunge letu Tukufu. Vilevile, nawashukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba Madelu (Mb), Waziri wa Fedha na Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha kwa umoja na ushirikiano walio uonyesha kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, napenda kuwashukuru, Dkt. Natu ElMaamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Ndg. Elijah Mwandumbya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Makamishna, na Wataalam wote wa Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa dhati ya moyo wangu napenda kumshukuru Mhe. Twaha Mpembenwe (Mb), Mbunge wa Kibiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa uongozi wake makini. Niwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa uchapakazi na moyo wa kujituma waliouonyesha wakati wa kujadili

Azimio hili. Naomba kuwatambua Wajumbe hao na kwa kuzingatia naomba majina yao yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge:-

1. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Twaha Mpembenwe, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Shally Josepha, Raymond, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Omar Ali Omar, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Yahya Ally Mhata Mb - Mjumbe
21. Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee kabisa naomba nimshukuru Bw. Baraka Ildefonce Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Oran Manase Njeza
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
26 Juni, 2025

**SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, aje awasilishe hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge kuendelea kukushukuru sana Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kutuongoza vyema kabisa katika Bunge letu Tukufu. Pia niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutuongoza vyema katika nchi yetu, hususani katika ajenda ya uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 923 la tarehe 29 Novemba, 2019 ikiwa na ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 30,893 kwa kupandisha hadhi iliyokuwa sehemu ya Pori la Akiba la Selous lililoanzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 275 la mwaka 1974 likiwa na ukubwa wa kilometa za mraba takribani 50,000 na baadhi ya maeneo ya vijiji. Sehemu ya Pori la Akiba la Selous yenye ukubwa wa kilometa za mraba 18,020.54 iliyobaki baada ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, iliendelea kutambulika kama Pori la Akiba la Selous na ilitangazwa rasmi kwa Tangazo la Serikali Na.459 la mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kumega sehemu iliyopandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kutoka sehemu ya Pori la Akiba la Selous mipaka iliyotumika kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Nyerere haikufuata mipaka iliyokuwa ya Pori la Akiba la Selous kwa baadhi ya maeneo na pia mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kutokuendana na Mto Rufiji ambao ndio alama ya asili kati ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na Pori la Akiba la Selous. Hali iliyosababisha malalamiko yanayohusu muingiliano wa mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na maeneo yaliyohifadhiwa ya Pori la Akiba la Selous, Vijiji na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Mbarang'andu, Juhiwangumwa, Iluma, Jukumu, Magingo na Nalika.

Mheshimiwa Spika, kimsingi ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa migogoro ya mpaka baina ya maeneo yaliyohifadhiwa yanapatiwa ufumbuzi wa kudumu ili kuwezesha shughuli nyingine kuendelea katika mazingira rafiki. Kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kwa kumega ukubwa wa kilometa za mraba 195.64 kwenda Pori la Akiba la Selous, kumega kilometa za mraba 259.55 kwenda kwenye vijiji na eneo la *TANESCO*, kumega kilometa za mraba 687.46 kwenda Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori na kumega kilometa za mraba 474.35 kuwa Hifadhi ya Msitu wa Taifa. Kukubalika kwa hoja hii kutatoa fursa za manufaa ya kimazingira, kijamii na kiuchumi kama ifuatavyo: -

(i) Migogoro ya mipaka baina ya Taifa, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, Vijiji, Pori la Akiba la Selous pamoja na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Mbarang'andu, Juhiwangumwa, Iluma, Jukumu, Magingo na Nalika zinazopakana na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

(ii) Kuongezeka Pato la Taifa kwa msingi kuwa kurekebishwa kwa mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kutaendeleza hifadhi hiyo kuwa kivutio cha utalii na kuruhusu shughuli za uwindaji wa kitalii ndani ya Pori la Akiba la Selous na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori zinazozunguka kufanyika katika mazingira rafiki.

(iii) Kulinda mfumo wa ikolojia unaounganisha Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na Pori la Akiba la Selous na kuimarisha mtiririko endelevu wa maji katika Mto Rufiji unaotegemewa kuzalisha umeme wa maji katika Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere, ili kuimarisha upatikanaji wa umeme.

(iv) Kuimarisha uhifadhi wa maliasili, hususani wanyamapori, mimea, mazalia ya wanyamapori na makuzio ya samaki na viumbe wengine kwenye maji.

(v) Kuwezesha upatikanaji wa maji, kwa ajili ya wakulima, wafugaji na wavuvi.

(vi) Kuwezesha shughuli mbalimbali za maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau katika usimamizi wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kwa kufanya yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kuendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya eneo la Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, pamoja na matumizi ya maji na kuweka miundombinu inayofaa na yenye viwango vinavyokubalika ndani na nje ya hifadhi, kwa ajili ya kuendeleza Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo Wizara imefanya uamuzi wa kumega eneo lenye kilometa za mraba 1,617 na kuwarejeshea wananchi Pori la Akiba la Selous, kwa ajili ya shughuli nyingine za maendeleo. Hivyo mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere utasomeka kwa ukubwa wa kilometa za mraba 29,276 kutoka kilometa za mraba 30,893 ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa masharti ya nyongeza ya kifungu cha nne cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amepewa mamlaka ya kurekebisha mipaka ya eneo lolote linalotangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa baada ya kupata idhini ya Bunge na kwa tamko litakalochapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Kufanyika Marekebisho ya Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, lengo la Sera ya Wanyamapori ya mwaka 2007 ni kudumisha uhifadhi endelevu, kuanzisha na kuboresha ikolojia wakilishi ya maeneo yaliyohifadhiwa na kulinda baianuai katika mtandao wa Hifadhi za Taifa za Wanyamapori na Mapori Tengefu.

Na Kwa kuwa, Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ilianzishwa kwa Tangazo la Serikalia Na. 923 la tarehe 29 Novemba, 2019 ikiwa na ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 30,893 kwa kuipandisha hadhi iliyokuwa sehemu ya Pori la Akiba la Selous lililoanzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 275 la mwaka 1974 ikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba takribani 50,000 na baadhi ya maeneo ya vijiji.

Na Kwa kuwa, sehemu ya Pori la Akiba la Selous lenye ukubwa wa kilometa za mraba 18,020.54 iliyobakia baada ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere iliendelea kutambulika kama Pori la Akiba la Selous na ilitangazwa rasmi kwa Tangazo la Serikali Na. 459 la mwaka 2021.

Na Kwa kuwa, wakati wa kumega sehemu iliyopandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kutoka sehemu ya Pori la Akiba la Selous mipaka iliyotumika kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Nyerere haikufuata mipaka iliyokuwa ya Pori la Akiba la Selous kwa baadhi ya maeneo na pia mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kutokuendana na Mto Rufiji ambao ndio alama ya asili kati ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na Pori la Akiba la Selous, hali iliyopelekea malalamiko yanayohusu muingiliano wa mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na maeneo yaliyohifadhiwa ya Pori la Akiba la Selous, Vijiji na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Mbarang'andu, Juhiwangumwa, Iluma, Jukumu, Magingo na Nalika.

Na Kwa kuwa, ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa kimsingi migogoro ya mipaka baina ya maeneo yaliyohifadhiwa inapatiwa ufumbuzi wa kudumu, ili kuwezesha shughuli nyingine kuendelea katika mazingira rafiki.

Na Kwa kuwa, kifungu cha tatu cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282, kinampa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kutangaza eneo lolote la ardhi kuwa Hifadhi ya Taifa ya baada ya kupata idhini ya Bunge na kwa tamko litakalochapishwa katika Gazeti la Serikali.

Na Kwa kuwa, kifungu cha nne cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282, kinatoa katazo la kubadili, kurekebisha au kufuta Hifadhi za Taifa isipokuwa kwa Sheria ya Bunge.

Na Kwa kuwa, kifungu cha nne cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282, kinampa Mheshimiwa Rais mamlaka ya kurekebisha mipaka ya eneo lolote linalotangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa kwa mujibu wa kifungu cha tatu cha Sheria ya Hifadhi za Taifa baada ya kupata idhini ya Bunge na kwa tamko litakalochapishwa katika Gazeti la Serikali.

Na Kwa kuwa, kwa kuridhia Azimio hili, ili kurekebisha mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kwa kumega ukubwa wa kilometa za mraba 195.64 kwenda Pori la Akiba la Selous, kumega kilometa za mraba 687.46 kwenda Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori na kumega kilometa za mraba 259.55 kwenda kwenye vijiji na eneo la *TANESCO* na kumega kilometa za mraba 474.35 kuwa Hifadhi ya Msitu wa Taifa, kwa ajili ya shughuli nyingine za maendeleo kutaleta manufaa yafuatayo kwa Taifa: -

(a) Kuondoa migogoro ya mipaka baina ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, Pori la Akiba la Selous, vijiji pamoja na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Mbarang'andu, Juhiwangumwa, Iluma, Jukumu, Magingo na Nalika zinazopakana na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

(b) Kutaleta manufaa ya kuongeza Pato la Taifa kwa msingi kuwa kurekebishwa kwa mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kutaendeleza hifadhi hiyo kuwa kivutio cha utalii na kuruhusu shughuli za uwindaji wa kitalii ndani ya Pori la Akiba la Selous na jumuiya za kuhifadhi za wanyamapori zinazozunguka kufanyika katika mazingira rafiki.

(c) Manufaa ya kulinda mfumo wa ikolojia unaounganisha Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na Pori la Akiba la Selous na kuimarisha mtiririko endelevu wa maji katika mto Rufiji unaotegemewa

kuzalisha umeme wa maji katika Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere, ili kuimarisha upatikanaji wa umeme.

(d) Kuimarisha uhifadhi wa maliasili hususani wanyamapori, mimea, mazalia ya wanyamapori na makuzio ya samaki na viumbe wengine kwenye maji na kuwezesha shughuli mbalimbali za maendeleo.

Hivyo basi kwa kuzingatia manufaa ya kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ninaomba sasa Bunge hili katika Mkutano wake wa 19 na kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha nne cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282, liridhie Azimio la Kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kwa kuondoa kilometa za mraba 1,617. Hivyo mpaka wa Hifadhi ya Nyerere utasomeka kwa ukubwa wa kilometa za mraba 29,276 kutoka kilometa za mraba 30,893 kama ilivyoainishwa katika Kiambatisho cha Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MAELEZO YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII MHESHIMIWA BALOZI DKT. PINDI HAZARA CHANA (MB) KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA KUFANYIKA MAREKEBISHO YA MIPAKA YA HIFADHI YA TAIFA NYERERE YALIYOTOLEWA TAREHE 26 JUNI, 2025 KWENYE KIKAO CHA 19 CHA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika,** Hifadhi ya Taifa Nyerere ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 923 la tarehe 29 Novemba, 2019 ikiwa na ukubwa wa eneo la kilometa za mraba **30,893** kwa kupandisha hadhi iliyokuwa sehemu ya Pori la Akiba Selous lililoanzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 275 la Mwaka 1974 ikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba takriban **50,000** na baadhi ya maeneo ya vijiji.

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya Pori la Akiba Selous yenye ukubwa wa kilometa za mraba **18,020.54** iliyobakia baada ya kuanzishwa

kwa Hifadhi ya Taifa Nyerere iliendelea kutambulika kama Pori la Akiba la Selous na ilitangazwa rasmi kwa Tangazo la Serikali Na. 459 la mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kumega sehemu iliyopandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa Nyerere kutoka sehemu ya Pori la Akiba Selous, mipaka iliyotumika kuanzisha Hifadhi ya Taifa Nyerere haikufuata mipaka iliyokuwa ya Pori la Akiba Selous kwa baadhi ya maeneo na pia mipaka ya Hifadhi ya Taifa Nyerere kutokuendana na Mto Rufiji ambao ndiyo alama ya asili kati ya Hifadhi ya Taifa Nyerere na Pori la Akiba Selous hali iliyopelekea malalamiko yanayohusu muingiliano wa mipaka ya Hifadhi ya Taifa Nyerere na maeneo yaliyohifadhiwa ya Pori la Akiba Selous, vijiji na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za MBARANG'ANDU, JUHIWANGUMWA, ILUMA, JUKUMU, MAGINGO na NALIKA.

**Mheshimiwa Spika,** ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa migogoro ya mpaka baina ya maeneo yaliyohifadhiwa inapatiwa ufumbuzi wa kudumu ili kuwezesha uwekezaji na shughuli zingine kuendelea katika mazingira rafiki.

**Mheshimiwa Spika,** kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa Nyerere kwa kumega ukubwa wa kilometa za mraba **195.64** kwenda Pori la Akiba Selous, kumega kilometa za mraba **259.55** kwenda kwenye vijiji na eneo la TANESCO, kumega kilometa za mraba **687.46** kwenda Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori na kumega kilometa za mraba **474.35** kuwa Hifadhi ya Msitu wa Taifa kwa ajili ya shughuli nyingine za maendeleo na kukubalika kwa hoja hii kutatoa fursa za manufaa ya kimazingira, kijamii na kiuchumi kama ifuatavyo:

i. Kuondoa migogoro ya mpaka baina ya Hifadhi ya Taifa Nyerere, vijiji, Pori la Akiba Selous pamoja na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za MBARANG'ANDU, JUHIWANGUMWA, ILUMA, JUKUMU, MAGINGO na NALIKA zinazopakana na Hifadhi ya Taifa Nyerere;

ii. Kuongeza pato la Taifa kwa msingi kuwa kurekebishwa kwa mpaka wa Hifadhi ya Taifa Nyerere kutaendeleza hifadhi hiyo kuwa Kivutio cha Utalii na kuruhusu shughuli za uwindaji wa kitalii ndani ya Pori la Akiba Selous na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori zinazozunguka kufanyika katika mazingira rafiki;

iii. Kulinda mfumo ikolojia unaounganisha Hifadhi ya Taifa Nyerere na Pori ya Akiba Selous na kuimarisha mtiririko endelevu wa maji katika Mto Rufiji unao tegemewa kuzalisha umeme wa maji katika Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Julius Nyerere ili kuimarisha upatikanaji wa umeme;

iv. Kuimarisha uhifadhi wa maliasili, hususan wanyamapori, mimea, mazalia ya wanyamapori na makuzio ya samaki na viumbe wengine kwenye maji;

v. Kuwezesha upatikanaji wa maji kwa ajili ya wakulima, wafugaji na wavuvi; na

vi. Kuwezesha shughuli mbalimbali za maendeleo ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kushirikiana na wadau katika usimamizi wa Hifadhi ya Taifa Nyerere kwa kufanya yafuatayo:

i. Kuendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya eneo la Hifadhi ya Taifa Nyerere pamoja na matumizi ya maji; na

ii. Kuweka miundombinu inayofaa na yenye viwango vinavyokubalika ndani na nje ya Hifadhi kwa ajili ya kuendeleza utalii;

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, Wizara imefanya uamuzi kumega eneo lenye kilomita za mraba **1,617** na kuwarejeshea wananchi, Pori la Akiba Selous na kwa ajili ya shughuli nyingine za maendeleo. Hivyo mpaka wa Hifadhi ya Taifa Nyerere utasomeka kwa ukubwa wa kilometa za mraba **29,276** kutoka kilomita za mraba **30,893** ilivyokuwa awali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa masharti ya nyongeza ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amepewa mamlaka ya kurekebisha mipaka ya eneo lolote lililotangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa baada ya kupata idhini ya Bunge, na kwa Tamko litakaochapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Kufanyika Marekebisho ya Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kama ifuatavyo:

**AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA KUREKEBISHA MPAKA WA HIFADHI YA TAIFA NYERERE**

---

**KWA KUWA,** lengo la Sera ya Wanyamapori ya Mwaka 2007 ni kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha ikolojia wakilishi ya maeneo yaliyohifadhiwa na kulinda bioanuwai katika mtandao wa Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu;

**NA KWA KUWA,** Hifadhi ya Taifa Nyerere ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 923 la tarehe 29 Novemba, 2019 ikiwa na ukubwa wa eneo la kilometa za mraba **30,893** kwa kupandisha hadhi iliyokuwa sehemu ya Pori la Akiba Selous lililoanzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 275 la Mwaka 1974 ikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba takriban **50,000** na baadhi ya maeneo ya vijiji;

**NA KWA KUWA,** sehemu ya Pori la Akiba Selous lenye ukubwa wa kilometa za mraba **18,020.54** iliyobakia baada ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa Nyerere iliendelea kutambulika kama Pori la Akiba Selous na ilitangazwa rasmi kwa Tangazo la Serikali Na. 459 la mwaka 2021;

**NA KWA KUWA,** wakati wa kumega sehemu iliyopandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa Nyerere kutoka sehemu ya Pori la Akiba Selous, mipaka iliyotumika kuanzisha Hifadhi ya Taifa Nyerere haikufuata mipaka iliyokuwa ya Pori la Akiba Selous kwa baadhi ya

maeneo na pia mipaka ya Hifadhi ya Taifa Nyerere kutokuendana na Mto Rufiji ambao ndiyo alama ya asili kati ya Hifadhi ya Taifa Nyerere na Pori la Akiba Selous hali iliyopelekea malalamiko yanayohusu muingiliano wa mipaka ya Hifadhi ya Taifa Nyerere na maeneo yaliyohifadhiwa ya Pori la Akiba Selous, vijiji na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za MBARANG'ANDU, JUHIWANGUMWA, ILUMA, JUKUMU, MAGINGO na NALIKA;

**NA KWA KUWA,** ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa migogoro ya mipaka baina ya maeneo yaliyohifadhiwa inapatiwa ufumbuzi wa kudumu ili kuwezesha uwekezaji na shughuli zingine kuendelea katika mazingira rafiki;

**NA KWA KUWA**, kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282 kinampa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kutangaza eneo lolote la ardhi kuwa Hifadhi ya Taifa baada ya kupata idhini ya Bunge na kwa Tamko litakalochapishwa katika Gazeti la Serikali;

**NA KWA KUWA**, kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282 kinatoa katazo la kubadili, kurekebisha au kufuta hifadhi ya Taifa, isipokuwa kwa Sheria ya Bunge;

**NA KWA KUWA**, kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282 kinampa Rais mamlaka ya kurekebisha mipaka ya eneo lolote lililotangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa baada ya kupata idhini ya Bunge na kwa Tamko litakalochapishwa katika Gazeti la Serikali; na

**NA KWA KUWA**, kwa kuridhia Azimio hili, ili kurekebisha mipaka ya Hifadhi ya Taifa Nyerere kwa kumega ukubwa wa kilometa za mraba 195.64 kwenda Pori la Akiba Selous, kumega kilometa za mraba 687.46 kwenda Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori na kumega kilometa za mraba 259.55 kwenda kwenye vijiji na eneo la TANESCO na kumega kilometa za mraba 474.35 kuwa Hifadhi ya Msitu wa Taifa kwa ajili ya shughuli nyingine za maendeleo kutaleta manufaa yafuatayo kwa Taifa:

a) Kuondoa migogoro ya mipaka baina ya Hifadhi ya Taifa Nyerere, Pori la Akiba Selous, vijiji pamoja na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za MBARANG'ANDU, JUHIWANGUMWA, ILUMA, JUKUMU, MAGINGO na NALIKA zinazopakana na Hifadhi ya Taifa Nyerere;

b) Kuongeza pato la Taifa kwa msingi kuwa kurekebishwa kwa mpaka wa Hifadhi ya Taifa Nyerere kutaendeleza hifadhi hiyo kuwa Kivutio cha Utalii na kuruhusu shughuli za uwindaji wa kitalii ndani ya Pori la Akiba Selous na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori zinazozunguka kufanyika katika mazingira rafiki;

c) Kulinda mfumo ikolojia unaounganisha Hifadhi ya Taifa Nyerere na Pori la Akiba Selous na kuimarisha mtiririko endelevu wa maji katika Mto Rufiji unao tegemewa kuzalisha umeme wa maji katika Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Julius Nyerere ili kuimarisha upatikanaji wa umeme;

d) Kuimarisha uhifadhi wa maliasili, hususan wanyamapori, mimea, mazalia ya wanyamapori na makuzio ya samaki na viumbe wengine kwenye maji; na

e) Kuwezesha shughuli mbalimbali za maendeleo.

**HIVYO BASI,** kwa kuzingatia manufaa ya kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa Nyerere, ninaomba sasa Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Tisa na kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura ya 282 liridhie Azimio la kurekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa Nyerere kwa kuondoa kilometa za mraba **1,617**. Hivyo mpaka wa Hifadhi ya Taifa Nyerere utasomeka kwa ukubwa wa kilometa za mraba **29,276** kutoka kilomita za mraba **30,893** kama inavyoainishwa katika **Kiambatisho cha Azimio hili.**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 60(6)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere la mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mamlaka uliyopewa na Kanuni ya 136(3) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 60(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 uliipa Kamati kazi ya kujadili na kuchambua hoja ya Azimio la Bunge la Kuridhia Kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere la mwaka 2025 kama ilivyowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, namna Kamati ilivyotekeleza majukumu; kama zilivyo Kamati nyingine za kisekta, pamoja na masuala mengine Kamati hii inapewa jukumu mahsusi la kuchambua na kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mujibu wa kifungu 7(1)(d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea ajenda ya kujadili hoja hiyo, Kamati ilikutana na kufanya uchambuzi wa awali wa maudhui yanayopendekezwa na Azimio hilo. Katika hatua hii Kamati ilitathmini maudhui ya mapendekezo ya Serikali kwa maslahi mapana ya Taifa. Baada ya hatua hiyo Kamati ilipata fursa ya kujadili maudhui ya azimio linalopendekezwa na Serikali kwa kupata maelezo ya kina kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii kama yalivyowasilishwa na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa

Dunstan Luka Kitandula, Mbunge. Katika maelezo yake Serikali ilifafanua masuala mbalimbali yanayopatikana katika azimio hilo, ikiwemo malengo yake pamoja na mawanda ya utekelezaji wa azimio hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 136(8) na (9) Kamati ilijiwekea utaratibu na kuamua kusikiliza maoni ya Wabunge wengine ambao siyo Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Wabunge hao ni wale ambao wanawawakilisha wananchi ambao wanatoka katika maeneo yanayozungukwa na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na kwa namana moja au nyingine wanaguswa na mapendekezo yaliyoletwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge hao ambao ni wadau muhimu kwa maoni, ushauri na uzoefu wao wa uhifadhi na changamoto zilizopo katika maeneo yao. Mambo hayo yameisaidia Kamati kuboresha taarifa yake kuhusu azimio hili.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati; Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ilianzishwa rasmi kwa Tangazo la Serikali Na. 923 la tarehe 29 Novemba, 2019. Hifadhi hiyo ina ukubwa wa kilometa za mraba 30,893. Hifadhi hiyo ilianzishwa kwa kupandishwa hadhi iliyokuwa sehemu ya Pori la Akiba la Selous ambalo lilikuwepo kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 275 la mwaka 1977. Pori hilo lilikuwa na ukubwa wa kilometa za mraba zipatazo 50,000. Kwa muktadha huo sehemu ya Pori la Akiba la Selous ilibaki na kilometa za mraba 18,020.54 na kutambulika upya Kisheria kwa Tangazo la Serikali Na. 459 la mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, kwa azimio hili, Serikali inapendekeza kupunguza ukubwa wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kwa kumega eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 10,617. Hivyo basi, baada ya azimio hili hifadhi hiyo sasa itakuwa na ukubwa wa kilometa za mraba 29,276 kutoka kilometa za mraba 30,893 za awali.

Mheshimiwa Spika, katika kilometa za mraba 1,617 zinazomegwa kwa azimio hili mgawanyo wake umependekezwa kama ifuatavyo; kilometa za mraba 195.64 kwenda Pori la Akiba la la Selous *(Selous Game Reserve)*, kilometa za mraba 687.46 kwenda kwenye Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori *(WMAs)*, kilometa za mraba 259.55 kwenda kwenye vijiji na *TANESCO,* kwa maelezo ya Serikali kati ya hizo kilometa za mraba 119.55 zinakwenda kwenye vijiji na kilometa za mraba 140 ni kwa ajili ya mitambo na Ofisi za *TANESCO*. Pia kilometa za mraba 474.35 zitakuwa ni Hifadhi ya Msitu wa Taifa, kwa ajili ya shughuli nyingine za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, malengo ya kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere; katika maelezo yaliyowasilishwa na Serikali, Kamati imebaini kwamba wakati wa kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kwa kumega sehemu iliyopandishwa hadhi kutoka Pori la Akiba la la Selous mipaka iliyotumika haikufuata mipaka ya Pori la Akiba la la Selous. Baadhi ya maeneo ya mipaka hiyo haikuendana na mpaka wa asili wa Mto Rufiji ambao kwa maelezo ya Serikali ndio alama ya asili kati ya Hifadhi ya Nyerere na Pori la Akiba la la Selous. Hali hii ilisababisha kuwepo kwa malalamiko yatokanayo na changamoto ya kuingiliana kwa mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na maeneo yaliyohifadhiwa na Pori la Akiba la la Selous. Muingiliano huo pia unahusisha vijiji na Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori *(WMAs)* za Mbarang'andu, Juhiwangumwa, Nalika, Jukumu, Magingo na Iluma.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho hayo yanalengo la kupata ufumbuzi wa migongano ya mipaka baina ya maeneo yaliyohifadhiwa. Aidha, hatua hii ni sehemu ya jitihada za Serikali kuhakikisha kwamba changamoto mbalimbali katika eneo hilo zinapata ufumbuzi wa kudumu, ili kuwezesha uwekezaji na shughuli nyingine za kuendelea kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa maudhui ya mgawanyo wa matumizi ya eneo linalomegwa; katika uchambuzi wa maudhui ya mgawanyo wa matumizi eneo linalopendekezwa kumegwa, Kamati ilitathmini ili kujiridhisha iwapo maslahi mapana ya nchi

yamezingatiwa kikamilifu kwa mapendekezo yanayoletwa na Serikali. Kwa muktadha huo Kamati ilifanya tathmini katika maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kuhusu umuhimu wa kumega eneo la hifadhi ya Taifa; moja kati ya eneo ambalo Kamati ilitaka kujiridhisha ni iwapo kuna umuhimu wa kumega eneo hilo ambalo hapo awali Bunge liliridhia kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa. Baada ya kutathmini kwa kina suala hilo Kamati imejiridhisha kwamba wakati wa uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere kulikuwepo na malalamiko kwamba hifadhi hiyo ilimeza baadhi ya maeneo ya vijiji na baadhi ya maeneo ya *WMAs*. Kwa kuwa Bunge ni chombo cha uwakilishi lilizingatia masuala hayo, hasa kwa kuwa mustakabali wa wananchi uliguswa kwa sehemu. Kwa muktadha huo, Kamati ina maoni kwamba hatua hiyo ni suala lenye uendelevu na ustawi wa wananchi iwapo tu eneo ambalo litamegwa kwa matumizi ya ardhi ya vijiji linaendana na mahitaji halisi ya sasa na ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ardhi kinachomegwa kinatengwa kwa kulinganishwa na matumizi yanayokusudiwa; kwa kuzingatia masuala yaliyoainishwa hapo juu, Kamati pia ilifanya tathmini ya kupima kiwango cha ardhi kinachotengwa kwa kulinganisha na matumizi yanayokusudiwa. Katika mapendekezo yanayoletwa na Serikali, Kamati ilibaini kwamba eneo linalotengwa kwa ajili ya matumizi ya vijiji linaweza kutafsiriwa kwamba ni dogo ukilinganisha na eneo ambalo linatengwa uhifadhi wa shughuli nyingine za maendeleo. Ili hoja hii iwe na mashiko ni vyema kila Serikali ikawa na majibu kuhusu mahitaji halisi ya wananchi, hususani katika maeneo ambayo yanapakana na maliasili za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati; mipango ya matumizi bora ya ardhi; kwa kuwa suala la matumizi ya ardhi ni suala mtambuka, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Wizara ya Ardhi na taasisi nyingine zote za Serikali zinashirikishwa kuandaa mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi hiyo. Hoja hii imejengwa katika msingi kwamba eneo ambalo linatengwa lina

uhusiano wa moja kwa moja na suala zima la uhifadhi wa maliasili, wanyama pori, mimea, mazalia ya wanyama pori na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirikishwaji wa Kamati za Ardhi za Vijiji; hatua ambayo Serikali inapendekeza kuchukua ni hatua ambayo inatarajiwa kupanua wigo wa fursa za kimaendeleo, shughuli za kiuchumi na uwekezaji. Kwa kuzingatia suala hilo, Kamati inashauri kwamba Serikali ishirikishe kikamilifu Kamati za Ardhi za Vijiji ili kuepuka uwezekano wa kutokea migogoro ya mgawanyo wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuendelea kurekebisha mipaka katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere; katika kushughulikia Azimio hili Kamati imebaini kuwa kuna vijiji na maeneo ya mipaka ya utawala yanayozunguka Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ambayo hayaguswa na Azimio hili, lakini yana mgogoro wa mipaka. Kamati inashauri kuwa Serikali iendelee kufanya tathmini ya kina na kuja na azimio ambalo litashughulikia migogoro yote ya vijiji na maeneo mengine ambayo yanazunguka hifadhi hiyo. Aidha, katika kushughulikia migogoro Serikali ihakikishe kwamba inawashirikisha wananchi na wawakilishi wanaotoka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kurekebisha mipaka katika hifadhi nyingine za Taifa; Kamati imebaini kuwa katika baadhi ya maeneo yanayozunguka hifadhi nyingine za Taifa yana migogoro ya mipaka kati yake na vijiji na maeneo mengine ya utawala. Kwa mfano, katika Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusu mipaka ya vijiji vinavyozunguka maeneo haya. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inafanya tathmini ya kina na kuandaa maazimio ya kurekebisha mipaka katika hifadhi mbalimbali nchini ili kuondoa migogoro ya ardhi katika vijiji na maeneo yanayozunguka hifadhi hizo. Ni maoni ya Kamati kuwa ushauri huu utatekelezwa, utaimarisha uhifadhi endelevu na kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kiuchumi na uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho; ninaomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisawaidiwa na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza vyema Bunge letu hili na kwa namna ambavyo mmeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi na utekelezaji bora wa majukumu ya kila siku ya Kamati yetu. Kwa hakika wewe ni moja kati ya hazina tulizonazo na tunawaomba Wana-Uyole watutunzie hazina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao katika kutekeleza majukumu yao ya Kikatiba walichambua, walijadili na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maadhui ya Azimio hili. Kwa kutambua mchango wao ningependa nitaje majina yao lakini naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama taarifa yetu ilivyowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu naomba nimalize kwa kuwashukuru watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uamuzi kuhusu hoja; baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako sasa lijadili na kuridhia Azimio la Bunge la Kuridhia Kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere la mwaka 2025 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa wasilisho hilo kwa niaba ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali tumepokea maoni yaliyotolewa na Kamati yetu ya Bunge ambayo imezingatia maeneo mahsusi ambayo Serikali tulikuwa tumeyapokea. Kwa muktadha huo, naliomba Bunge lako Tukufu liweze kupitisha Azimio ambalo Serikali imelileta la uanzishwaji wa *African Finance Corporation* ili kuweza kunufaika na manufaa ambayo tumeyabainisha katika katika Azimio.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana na sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(The Agreement for the Establishment of the Africa Finance Corporation – AFC)*.

Waheshimiwa Wabunge, wote mmeafiki, ahsanteni sana. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninayo heshima kuendelea kukushukuru kwa uongozi wako imara. Pia nimshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, kwa kufika kwenye Kamati na kujadiliana pamoja na Kamati. Niendelee kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Timotheo Mnzava kwa maoni na ushauri mzuri wa Kamati ambao wametoa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetuelekeza mambo mengi mazuri kwamba imekubaliana na hoja hii ya kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa. Pamoja na ridhaa ya Kamati, Kamati imetukumbusha pia tuendelee kuangalia maeneo mengine mbalimbali ambayo yanahitaji maboresho ya mipaka kati ya hifadhi na maeneo ya wananchi na sisi tunasema suala hilo tunalichukua na suala hilo ni endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imetutajia baadhi ya maeneo hayo yakiwemo Mto Ugalla na maeneo ya Ruaha. Haya ni maeneo ambayo kimsingi tunayachukua. Pia Kamati imetuelekeza mambo mazuri kabisa kuhusu suala zima la ushirikishwaji wa Kamati za Ardhi za Vijiji. Baada ya kufanya marekebisho na kurudisha eneo hili kwa vijiji ni muhimu Kamati za Ardhi za Vijiji zikashirikishwa kuona namna gani sasa ardhi iliyorejeshwa wanaweza kuiweka vizuri, masuala ya mipango ya ardhi tukishirikiana na Wizara ya Ardhi. Tunakiri kupokea hoja hizi na tunasema kwamba tutaendelea kuzishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kulishukuru Bunge lako kwa kuunga mkono hoja hii na Kamati yetu imeunga mkono. Hivyo baada ya kusema hayo na ufafanuzi huo wa kupokea hoja hizo niendelee kukushukuru na niendelee kuomba Bunge letu liridhie Azimio la Kurekebisha Mpaka wa Hifadhi ya Taifa Nyerere kwa kuondoa kilometa za mraba 1,617 na sasa zitasomeka kilometa za mraba 29,276 kutoka kwenye zile za awali 30,893 kama ilivyoanishwa katika kiambatisho cha Azimio.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi wangu huo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, ahsante sana. Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge,

kuhusu hoja ya Waziri wa Maliasili kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

Waheshimiwa Wabunge wote mmeafiki, ahsanteni sana. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Waheshimiwa Mawaziri wawili hawa kuwasilisha hoja hizi na Kamati zetu kusema yale ambayo wamejadiliana huko na wameyaweka hapa na wametoa ushauri kwa upande wa Serikali na ushauri huo umefanyiwa kazi kwa mujibu wa taarifa hizi ambazo Mawaziri hawa wamezisoma, basi nitangaze rasmi kuwa Bunge leo limepitisha Azimio la la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika *(Agreement for the Establishment of the Africa Finance Corporation – AFC)*. *(Makofi)*

Kwa kupitisha Azimio hili tunaitakia Serikali kila la kheri katika hatua zinazofuata baada ya hapo kwa yale ambayo mmetueleza kwenye maelezo yenu, lakini pia mkataba tuliopitia kwamba inakwenda kuleta tija gani kwa upande wa maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri katika hatua zinazofuata. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati huo huo pia tumepata fursa baada ya Waziri wa Maliasili na Utalii kuleta hoja hii na Kamati yetu kuweza kuitazama hoja hii na wameleta hapa mapendekezo yao ambayo kama mlivyomsikia Waziri wakati akihitimisha, wameyachukua mawazo hayo kwa ajili ya maeneo mengine ambayo bado yana changamoto kwamba wataendelea kuyafanyia kazi kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamati yetu.

Sasa kwa kusema hivyo na tumeshawahoji Waheshimiwa Wabunge na ninyi mmeafiki, nitangaze rasmi basi kwamba leo Bunge limepitisha Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Mpaka wa

Hifadhi ya Taifa ya Nyerere. Kwa hiyo, nanyi tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa jambo hili ambalo Bunge limepitisha; tunaamini litaenda kuondoa hiyo migogoro katika maeneo yanayoguswa na yale ambayo yatakuwa hayajaguswa basi Kamati imewapa ushauri hapo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba anao wageni 42 ambao ni mashemeji zake na watoto wake. Sijui wako upande gani? Haya, ahsanteni sana. Kwa hiyo, huyu ana ukoo mkubwa sana. Karibuni sana, ninawashukuru. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nimeletewa taarifa rasmi kabisa kwamba Klabu ya *Young Africans* wameshinda kombe. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwapongeza. *(Makofi)*

Sasa acheni kwanza kupiga makofi ili yasikike yale ninayosema halafu mtapiga nikimaliza itarahishisha.

Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuwapongeza sana Klabu ya *Young Africans* (Yanga) kwa kutwaa ubingwa kwa mfufulizo kwa kweli, kama Waziri amesema ni mara nne au mara tano hivi sasa, mara nne mfululizo kwa kushinda Ligi ya Kuu hapa nchini. Kwa hiyo, tunawapongeza sana Yanga. Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri pia kwa sababu wameshinda hii Ligi Kuu hapa nchini, lakini tunawatarajia pia viwango vizuri walivyoonesha waendelee kutuwakilisha huko kwingine pia. Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri na hongereni sana Yanga. *(Makofi)*

Haya, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kama mjuavyo siku ya kesho tutakuwa na jambo zito hapa Bungeni, kwa sababu hiyo na kwa sababu ya uzito wa jambo hilo huwa tuna utaratibu wa kualika wageni ambao kwa utaratibu wa kawaida wasingeweza kuingia hapa kwenye ukumbi wetu wa Bunge, wanakuwa wanakaa sehemu ambayo wanakaa wageni.

Sasa kwa sababu tuna utaratibu wa kualika baadhi ambao si Wabunge kuingia hapa ndani, kwa maana ya viongozi, basi tunampa nafasi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu ili atuletee hoja ili tuweze kutengua Kanuni tayari kwa ajili kuwapokea wageni ambao kesho tutakuwa nao kwenye Ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge wa Ismani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, karibu kwa ajili ya kuwasilisha hoja. *(Makofi)*

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninakushukuru kwa kutamka vizuri jina langu.

Kwa kuwa kwa mujibu wa Ibara ya 91(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka ya 1977 na Kanuni ya 36(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, kesho tarehe 27 Juni, 2025 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan atalihutubia Bunge na hatimaye kuhitimisha rasmi Shughuli za Bunge la Kumi na Mbili;

Na kwa kuwa wamealikwa viongozi mbalimbali kuja kushirikisha hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati akilihutubia Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Na kwa kuwa Kanuni ya 160(1) na Kanuni ya 164(f) zinaelekeza kwamba wageni wanaoruhusiwa kuingia Bungeni watakaa maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao;

Na kwa kuwa, ili kuruhusu viongozi wa kitaifa walioalikwa na Mheshimiwa Spika kuja kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais kuingia na kukaa ndani ya Ukumbi wa Bunge inabidi Bunge litengue Kanuni;

Kwa hiyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 174(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari, 2023, Bunge linaazimia kwamba Kanuni ya 160(1) na 164(f) ambazo kwa ujumla wake zinaelekeza kuwa wageni wanaoruhusiwa kuingia Bungeni wataketi maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao, zitenguliwe ili viongozi wa kitaifa walioalikwa na Mheshimiwa Spika waruhusiwe kuingia na kukaa sehemu watakazopangiwa ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa ajili ya kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana.

Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge ili kutoa fursa ya wageni kuingia kwenye Ukumbi huu, ahsanteni sana, wote mmeafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, kesho tutapata nafasi ya kushirikiana na viongozi ambao watakuwa wamepata mialiko. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea sana na ratiba yetu, nitoe fursa kwa Wenyeviti wetu wa Bunge ambao walikuwa wananisaidia kazi hapa mbele, kusema maneno machache kisha tuendelee na ratiba yetu.

Mheshimiwa Najma Murtaza Giga. *(Makofi)*

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii adhimu kabisa.

Kwanza kabisa nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye muweza wa kila jambo na yeye ndiye anayetuwezesha kufanya kila kitu katika ulimwengu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nikushukuru wewe mwenyewe Mheshimwa Dkt. Tulia Ackson, kwa namna ambavyo tumeweza kushirikiana na mimi kwa mambo mbalimbali na namna ambavyo umeweza kunisimamia na kunijengea uwezo mkubwa sana katika kipindi chote ambacho umekuwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo nisimsahamu Mheshimiwa Spika ambaye tulianza naye Bunge hili la Kumi na Mbili, Mheshimiwa Job Ndugai kwa namna ambavyo tumeanza kufanya naye kazi pamoja. Ninashukuru sana, wote wawili mmeweza kunisimamia vizuri sana katika nafasi yangu hii ya Uenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee kabisa na kwa heshima ya aina yake, niushukuru uongozi wa Chama Cha Mapinduzi katika nchi yetu, kuanzia Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi Dkt. Samia Suluhu Hassan na pia Makamu Mwenyekiti - Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa namna ambavyo imani yao juu yangu ipo kubwa na kuweza kunipatia nafasi mbalimbali ikiwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kupitia viti 20 vya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ninaamini na kuthamani sana imani yao juu yangu na bado nina nia ya dhati na thabiti kabisa ya kukitumikia Chama Cha Mapinduzi pamoja na kuitumia Jumuiya ya Wazazi kwenye nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na pia natumia fursa hii kabisa adhimu kuushukuru uongozi wa Jumuiya ya Wazazi Tanzania, lakini pia na uongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania, kwa namna ambavyo wanaendelea kuniamini katika kazi zangu hizi za Bunge ya Viti Maalum. Hata hivyo, niwashukuru wanachama wote popote walipo

katika nchi hii, Chama Cha Mapinduzi pamoja na jumuiya zake. Bila ya wao mimi nisingeweza kuwa na nguvu na ujasiri wa kufanya kazi zangu za chama pamoja na Serikali kama ambavyo nafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nitumie fursa hii kuzishukuru Kamati zangu zote mbili ambazo nimehudumia katika Bunge hili la Kumi na Mbili; Kamati ya Katiba na Sheria; na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Ninawashukuru wote ambao tumeshirikiana na namna ambavyo mmenipa upendo wenu na ushirikiano wa kuweza kufanya kazi zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ninawashukuru sana Mawaziri wote kwa namna ambavyo mnashirikiana na mimi katika kazi za hapa Bungeni, lakini hata nje ya Bunge. Pia ninatoa pongezi na shukrani za dhati kwa Wabunge wote ambao nimekaa nao kwa kipindi chote na namna ambavyo mnatumia upendo wenu na uzuri wenu katika kunifanya niweze kufanya kazi zangu kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa siyo kwa kusema kwamba ni muhimu ama ni vipi, lakini kwa heshima ya pekee niwashukuru viongozi wote ama watendaji wote wa Bunge letu la Kumi na Mbili na ninaamini kwamba utendaji wao wa kazi ndiyo umefanikisha na mimi kuweza kufanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninatumia fursa hii kuwaomba Watanzania wote, tunaingia kwenye uchaguzi, twende kufanya uchaguzi wetu kwa amani na utulivu kabisa nikiamini kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja na mgombea mwenza Dkt. John Nchimbi bado wanafaa na wanaweza sana. Kwa hiyo, tukapige kura kuwachagua wote, lakini bila kuwasahau Wabunge wa CCM, chama kwanza mtu baadaye, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kupata fursa hii na nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa neema ambazo tumejaliwa hadi siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Kumi na Mbili litakumbukwa na kizazi hiki na kizazi kijacho kwa kuacha alama kubwa za maendeleo kwenye Taifa letu. Tunapoipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa miradi mikubwa ya maendeleo ambayo imeweza kuifanikisha ikiwemo miradi ya *SGR*, Bwawa la Mwalimu Nyerere, maandalizi ya Dira ya mwaka 2050 pamoja na miradi mikubwa yote ya maendeleo, hatuwezi kusahau mchango mkubwa wa Bunge lako la Kumi na Mbili kwa sababu ndilo ambalo lilipitisha bajeti hizo na ndilo ambalo lilikuwa na jukumu la kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Bunge lako la Kumi na Mbili linaenda kuacha alama ya kudumu kwenye Taifa letu la Tanzania. Kwa sababu hiyo, ninaomba uniruhusu kwa nafasi ya kwanza kuwapongeza sana, kwanza wewe mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge hili la Kumi na Mbili pamoja na Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge, Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge na timu nzima ambayo imeshiriki katika kufanikisha haya masuala yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kukushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge ambao walinipa heshima ya kuwa Mwenyekiti wa Bunge hili Tukufu. Kazi hii imekuwa na mafanikio makubwa sana kwa sababu ya ushirikiano ambao nimeupata kutoka kwako, kwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote. Nitumie fursa hii kusema ninawashukuru sana na fursa hii ikipatikana tena kwa uhakika sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia uniruhusu kwa namna ya kipekee sana kumshukuru Mheshimiwa Florent Kyombo - Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria ambao kwa kipindi chote nikiwa na

majukumu haya ya Uenyekiti wa Bunge wameendelea kusaidia kufanya kazi kwa ufanisi na mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rashid Shangazi, Katibu wa Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi kwa kutusimamia vizuri kwenye utekelezaji wa majukumu yetu. Sambamba na yeye ninamshukuru sana Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee sana uniruhusu nitumie jukwaa hili la Bunge lako Tukufu kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Madaba kwa kunipa heshima ya kuwa mwakilishi wao kwenye Bunge hili Tukufu kwa miaka 10 sasa na kwa ushirikiano ambao wamenipa kwa kipindi chote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Madaba limerekodi maendeleo makubwa sana tangu kuanzishwa kwake miaka 10 iliyopita. Hatua kubwa za maendeleo ambazo Madaba tumepiga zimetokana na ushirikiano mkubwa ambao kila mwananchi wa Madaba ameweza kuutoa kwangu na kwa Serikali yetu, imetokana na dhamira safi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanapata huduma bora na kwa ukaribu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninawashukuru sana wananchi wa Madaba kwa kunipa ushirikiano mkubwa. Ninakishukuru Chama Cha Mapinduzi ngazi zote kuanzia ngazi za ubalozi mpaka ngazi ya Taifa kwa namna ambavyo wamenipa ushirikiano. Wito wangu kwa Wana-Madaba, kazi ya kuijenga Madaba inaendelea, kazi hii itafanikiwa tu iwapo wote kwa pamoja tutaungana kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uchaguzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeonesha dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Madaba na niendelee kuwaomba kwamba kwa vile kazi bado tunazo na huwa wanajua tumefanya kazi kubwa pamoja basi tuendelee kulijenga hili Taifa pamoja.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru sana tena viongozi wangu wa Chama Cha Mapinduzi. Kipekee niishukuru familia yangu, kwanza mke wangu Sophia Augustino Mhagama pamoja na wanangu wote wanne; ndugu, jamaa, marafiki pamoja na wazazi wangu. Ninashukuru sana sana kwa heshima kubwa ambayo tumepata na kwa mafanikio makubwa ambapo Jimbo la Madaba tumeweza kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninashukuru sana kwa kupewa nafasi hii fupi ya kuweza kusema machache ndani ya Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema, lakini kwa namna ya pekee kabisa uwepo wangu ndani ya Bunge hili na kwa nafasi ambayo Bunge iliniamini na kunipatia. Kwa wale wanaofahamu historia yangu fupi mimi ninasema ni kwa neema tu za Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina uhakika kabisa Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ninamshukuru sana vilevile kwa sababu nilihitaji *transformation,* nina uhakika amekuwa sehemu kubwa ya *transformation* yangu kuingia Bungeni, kupewa nafasi na kuweza kuonesha kwamba nina uwezo wa kufanya kitu fulani kuisaidia nchi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe kwa namna ya kipekee sana kwa miongozo mbalimbali ambayo umekuwa ukitupatia hasa mimi toka pale Wabunge wenzangu waliniamini. Ninakushukuru sana kwa sababu umekuwa mwalimu wangu mzuri, kwanza ki-*profession* lakini kama Spika na Kiongozi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilionekana kwa sababu nilikuwa na Kamati ambayo iliniamini. Ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Kilimo ambao waliniamini na kunipa nafasi hii ya kuweza kuwaongoza, ninaamini sijawaangusha. Nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya Maadili ambayo wewe ulinipa hiyo kazi, niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Maadili, tumefanya kazi vizuri na tuliridhia tuwe na kazi nyingi, lakini tulipopata kazi chache tukajua kazi ya maadili ni ngumu. Kwa hiyo, tunashukuru kwa chache tulizozifanya tumezifanya vizuri na kwa weledi, tunamshukuru Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wabunge wenzangu wamenionesha imani kubwa sana kwangu toka siku ambapo walinichagua kwa kura nyingi, ninashukuru Kamati ya Uongozi ambayo ilipeleka jina langu kwa Wabunge kama mmoja ya watu ambao wangefaa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Ninawashukuru sana kwa kipindi chote hiki tumefanya kazi kwa pamoja na kwa kweli nilitoa ahadi moja siku ambapo nilikuwa ninawashukuru kwamba nitajitahidi kufuata Miongozo ya Spika, lakini nitajitahidi kuwa *fair* na nina uhakika nimejitahidi kufanya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miongozo hiyo ninamshukuru sana Naibu Spika - Mheshimiwa Mussa Zungu, amekuwa ni kiongozi ambaye nimefanya naye kazi kwa karibu sana na yeye amekuwa akitupatia miongozo. Ninawashukuru Wenyeviti wenzangu ambao tumefanya nao kazi kwa karibu hasa kipindi hiki cha Bunge refu la Bajeti, kilikuwa kipindi ambacho kimetufanya tuielewe kazi vizuri ya kuwasimamia Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli katika kuifanya kazi hii ninawashukuru Wabunge wote, Mawaziri na Naibu Mawaziri ambao wao katika maongezi waliyoyasema hapa katika ku-*present* bajeti zao walitushukuru sisi Wenyeviti kwamba tumelisimamia Bunge vizuri na mimi ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Vilevile ninamshukuru sana *Chief Whip* pamoja na Waziri Mkuu ambao tumefanya nao kazi kwa karibu sana mimi kama Mwenyekiti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tupo kwenye kipindi ambacho tunakwenda kwenye uchaguzi na sisi tunasema na mimi nimelisema mara nyingi hasa nilipolisema kama Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Rais amefanya uchaguzi wetu kuwa mwepesi kwa mambo makubwa ambayo yamefanyika. Ni suala la sisi sasa kutumia nafasi hiyo kuelezea vizuri yale ambayo tumeyapata, tumeyaona na tumeyafanya katika kipindi hiki ambacho tumepewa dhamana ya kuwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rashid Shangazi kwa ushirikiano mkubwa ambao amenionesha kwa kunitia moyo hata pale ambapo nilitaka kuwa na matatizo ya hapa na pale ya kikazi Mheshimiwa Shangazi alikuwa moja ya watu ambao walinipa nguvu sana. Jambo la siasa siyo wote tumelianza siku nyingi, kwa hiyo, tulihitaji sana kuwa na *counselors* na amekuwa *counselor* mzuri sana kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Katibu wa Bunge na Makatibu Mezani wote ambao kwa kweli wamenisaidia sana niweze kufanya kazi yangu vizuri na kwa ufanisi. Vilevile, niwashukuru wafanyakazi wote wa Bunge kwa ujumla wao; Makatibu Wasaidizi wa Bunge ambao walikuwa kwenye Kamati yangu, Makatibu wa Kamati wale ambao ni wafanyakazi wa Bunge na wafanyakazi mbalimbali wa Bunge ambao wamekuwa msaada mkubwa sana katika utendaji wa kazi hata katika yale mambo ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki nipo hapa kwa sababu wananchi wa Njombe waliniona wakaniamini, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wapigakura wote wa Jimbo la Njombe Mjini ambao mpaka muda huu ni wazi kwamba wameonesha imani kubwa sana kwangu kiasi cha kuonesha kwamba hawahitaji mtu mwingine kwenda kushindana na mimi kule Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba hata msafara wa mamba akiwa mmoja, kenge huwa wanajitokeza kumsikindiza, kwa hiyo ninaamini kwamba kwa mustakabali wa demokrasia bado Wana-Njombe wanakaribisha kugombea, lakini tuna uhakika kabisa watakuwa ni wasindikizaji kwa maana Wana-Njombe wameshaamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache nipende kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii fupi, lakini niishukuru sana familia yangu, mke wangu Bi. Dorothy na watoto wangu watatu wa kike ambao wamekuwa ni *inspiration* kubwa ya mimi kufanya kazi kwa ufanisi. Wamenipa nafasi kwa kutoniuliza maswali kwa nini sionekani nyumbani kwa sababu nipo Bungeni na nipo Njombe nikiwatumikia Wana-Njombe, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati ninahitimisha jambo hili, nipende kusema nimejifunza mengi na nipo tayari kuendelea na kazi, Wabunge wakiona kama ninafaa bado kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nafasi ya Mwenyekiti. Ahsante sana, ninakushukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Wenyeviti.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Spika aliwaaga wiki iliyopita na amesema leo kwa sababu Spika atapata nafasi ya kuzungumza basi yeye asizungumze, lakini pia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa sababu mkubwa wake yupo hapo na atapata nafasi ya kuzungumza basi na yeye hatozungumza, lakini ilikuwa niwape fursa ya kuzungumza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**SPIKA:** Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, ninaomba kutoa taarifa kuwa shughuli zote zilizoko kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge, sasa zimemalizika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na hoja nyingine kuna wageni hapa; wapo wageni waliokaa Jukwaa la Spika.

Tutaanza na wageni wangu wawili, Ndugu Tonny Kabeta, Mkurugenzi wa *Universities Abroad*, yupo pia Ndugu Boka Kabeta, Mkurugenzi Mweza *Universities Abroad,* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine waliokaa Jukwaa la Spika; kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ambaye ni Dkt. Jim Yonaz ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, karibu sana. *(Makofi)*

Hii inafurahisha sana huyu Waziri wake yupo hapa ndani, lakini amealikwa na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, jambo zuri sana hili, haya karibu sana Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii, yupo Dkt. Hassan Abbas ambaye ni Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii, karibu sana, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Kamshina wa Polisi Benedict Wakulyamba, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Alex Lobora, Mkurugenzi wa Wanyapori, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Abdalah Mvungi, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ambao ni wasanii wa *Bongo Movie* kutoka Mbozi, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HOTUBA YA KUKAMILIKA KWA SHUGHULI ZA MKUTANO WA KUMI NA TISA WA BUNGE**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada hotuba hii hutolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aje awasilishe hotuba yake. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa fadhila zake zilizotuwezesha kuiona siku hii muhimu katika historia ya Bunge la 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa fadhila zake zilizotuwezesha kuiona siku hii muhimu katika historia ya Bunge la 12. Kama mnavyofahamu tumekutana leo kwa ajili ya kuhitimisha Mkutano wa 19 ambao ulikuwa mahsusi kwa ajili ya kupokea na kujadili Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nitumie nafasi hii kukushukuru sana wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge wa Mbeya Mjini, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Hakika umekuwa kiongozi shupavu na umeonesha weledi mkubwa katika kuliongoza Bunge hili la 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzoefu wako wakati wote umekuwa na tija kubwa katika utendaji wa shughuli za Serikali Bungeni. Nakushukuru sana kwa namna ulivyoendesha mijadala yote ya bajeti za kisekta katika Mkutano huu wa 19 pamoja na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie nafasi hii kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala na Naibu Spika pamoja na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kwa nafasi zao za Uenyekiti wa Bunge. Wakati wote mmekuwa mkinipa ushirikiano wa kutosha wakati mlipokuwa mkimsaidia Mheshimiwa Spika katika shughuli za kuendesha Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati wa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za Bunge la 12. Waheshimiwa Wabunge, mmefanya kazi kubwa. Hakika mnastahili pongezi. Maoni, ushauri na michango yenu katika Mkutano huu wa Bajeti licha ya kugusa maisha ya wananchi wote imekuwa ikitoa mwelekeo sahihi katika mpango wa utendaji wa shughuli za Serikali. Pia nawapongeza kwa kazi kubwa mliyoifanya tarehe 24 Juni, 2025 ya kupitisha kwa kura ya ndiyo Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2025/2026 ya shilingi trilioni 56.49 kwa 98.7%. Hakika ninyi ni wazalendo, mmevunja *record,* mmeipenda nchi yenu na mnathamini kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano na mshikamano mlionipa wakati wote nilipokuwa nikitekeleza jukumu langu la Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni. Sitawasahau na sitasahau upendo wenu kwangu. *In Shaa Allah,* Mwenyezi Mungu ataajaalia kila lenye heri katika jambo lenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakifanya ufuatiliaji wa miradi kwenye majimbo yenu kwa karibu mno. Kila Mbunge aliwajibika katika kuhakikisha kuna upatikanaji wa maendeleo ya haraka kwa lengo la kuinua ustawi wa wananchi wote umefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, samahani, ahsante sana na poleni.

Mheshimiwa Spika, kama Waswahili wasemavyo; "kila mtenda wema atakumbukwa kwa wema." Niwaombe wananchi wote, endeleeni kuwaunga mkono Waheshimiwa Wabunge wetu huko majimboni. Hakika Waheshimiwa Wabunge mmetenda mema kwa kuwakilisha mema majimbo yenu na mnastahili kukumbukwa kwa wema wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake uliotukuka. Wakati wote amekuwa akinipa maelekezo yenye tija na kuifanya kazi yangu kuwa nyepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina shaka nyote mtakubaliana nami kuwa, hulka yake na ustahimilivu wake umekuwa faraja kwetu sisi wasaidizi wake, watumishi wote wa umma na Watanzania wote kwa ujumla. Isitoshe, Mheshimiwa Rais wakati wote amekuwa nguzo kuimarisha mshikamano na umoja katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa ushirikiano wake alionipatia wakati wote nikitekeleza majukumu yangu. Busara zake na weledi wake umekuwa msaada na mfano wa kuigwa katika utendaji wa kazi Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushirikiano mkubwa alionipa wakati wote. Kadhalika nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais Wa Zanzibar ambaye amekuwa Mwenyekiti Mwenza katika kamati mbalimbali za kitaifa na kufanya kazi pamoja, yeye pamoja na ofisi yake ya Makamu wa Pili wa Rais kule Zanzibar kwa ushirikiano wao wakati tukitekeleza majukumu yetu ya pamoja kama Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niendelee kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa ushirikiano mkubwa katika usimamizi na uratibu wa shughuli za Serikali. Nikiri kwamba Mheshimiwa Biteko amekuwa msaada mkubwa kwangu katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nitumie nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga, Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa kazi nzuri waliyoifanya. Pia ninawashukuru kwa kunisaidia kutekeleza majukumu yangu wanaposimamia dhamana ya Sera, Bunge na Uratibu katika Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Mrisho Kikwete - Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa pamoja na Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi - Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kunisaidia kusimamia dhamana ya kazi, vijana, ajira

na wenye ulemavu. Ushirikiano wao umekuwa chachu ya mafanikio katika shughuli za kila siku za Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa mara nyingine nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana pia Wana-Ruangwa kwa kuniunga mkono na kunipatia ushirikiano katika kipindi chote nilipokuwa nikitekeleza majukumu ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninatambua wakati mwingi nimekuwa nje ya jimbo letu nikitumikia Taifa, lakini Wana-Ruangwa wameendelea kuniunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kusema, ahsanteni sana. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kuimarisha mshikamano uliopo kati yetu sote na naomba kuwajulisha kuwa nakuja kuchukua fomu na kuomba ridhaa yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninaishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu mpendwa Mary Majaliwa na watoto wangu kwa upendo na uvumilivu walioonesha kwangu wakati wote. Hata pale nilipokuwa napitia magumu mliendelea kunionesha upendo wenu. Kwa hakika upendo na mshikamano wenu umekuwa ukinipa nguvu ya kutekeleza majukumu yangu ya kumsaidia kazi Mheshimiwa Rais, kukitumikia chama change; Chama Cha Mapinduzi na kuwatumikia Wana-Ruangwa pamoja na Watanzania wote. Ahsanteni sana, nawashukuru na nawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu salamu za pongezi; wakati Mkutano wa 19 wa Bunge ukiendelea, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanya teuzi mbalimbali. Teuzi hizo zilifanywa kwa lengo la kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi na shughuli mbalimbali za Serikali na mihimili mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 13 Juni, 2025 alimteua Mheshimiwa George Mcheche Masaju aliyekuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania.

Mheshimiwa Masaju amechukua nafasi ya Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma ambaye amestaafu na kwa hakika amefanya kazi kubwa iliyoacha alama katika mhimili wa Mahakama. Ninamtakia kila la kheri Profesa Ibrahim Juma katika maisha yake ya ustaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Jaji Masaju pamoja na viongozi wote wateule katika nafasi mbalimbali. Aidha, nitumie nafasi hii kuwatakia wateule wote kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao ambayo ni mapya na kuwakumbusha wajibu wao wa kutanguliza mbele maslahi ya Taifa letu na wananchi wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa katika Mkutano wa Shirika la Afya Duniani, tarehe 18 Mei, 2025 Geneva, Uswisi pamoja na masuala mengine, ulifanyika uchaguzi wa kumpata Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika. Kwa mara nyingine Tanzania iliendelea kung'ara kimataifa baada ya Profesa Mohamed Yakub Janabi, Mshauri wa Rais wa Masuala ya Tiba na Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika baada ya kuwashinda wagombea kutoka nchi za Ivory Coast, Guinea, Niger na Togo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaungana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu pamoja na Watanzania wote kumpongeza sana Profesa Mohamed Janabi kwa ushindi huo. Nafasi hii imeipa Tanzania heshima kubwa kwani imedhihirisha uwezo wa kuwaandaa viongozi wenye weledi ambao wanaweza kumudu ushindani kwa ngazi ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nikiendelea na Mkutano huu wa 19 wa Bunge lako Tukufu mnamo tarehe 7 Mei, 2025 tuliondokewa na mwanasiasa mashuhuri na mkongwe, Mheshimiwa Cleopa David Msuya. Mheshimiwa Msuya aliwahi kulitumikia Bunge hili akiwakilisha Jimbo la Mwanga, mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, Mheshimiwa Msuya amewahi kuhudumu Serikalini katika nafasi mbalimbali kuanzia mwaka 1964 hadi 1972 alihudumu nafasi ya Katibu Mkuu katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Utamaduni, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Maji, Wizara ya Mambo ya Uchumi na Mipango pamoja na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, vilevile mwaka 1972 hadi 1994 alikuwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Viwanda, Waziri wa Fedha tena, Uchumi na Mipango, Waziri wa Viwanda na Biashara lakini pia amewahi kuwa Waziri Mkuu kwa vipindi viwili tofauti mwaka 1980 hadi 1983 na mwaka 1994 hadi 1995 ambapo alihudumu kama Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mheshimiwa Spika, nami niungane na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki lakini natoa pole nyingi kwa wananchi wa Mwanga, wana CCM na Watanzania wote kwa ujumla. Tuendelee kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa marehemu pumziko la amani, Amina.

Mheshimiwa Spika, wapo Watanzania wenzetu waliokumbwa na majanga mbalimbali zikiwemo ajali za barabarani. Ninatoa pole kwa wananchi waliopoteza wapendwa wao katika ajali hizo. Vilevile natoa pole kwa majeruhi wote na nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awape uponyaji wa haraka. Nitumie nafasi hii pia kutoa pole kwa waathirika wote wa majanga ambayo hatukuyataja hapa, lakini yametokea kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati Bunge la 12 likiendelea kuhitimisha shughuli zake, nimefanikiwa kutekeleza masuala mbalimbali ikiwemo kujibu maswali na hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria ya Serikali, kujadili na kutoa Maazimio mbalimbali, kujadili na kuridhia Mikataba na Itifaki za Kikanda na Kimataifa pamoja na kupokea Kauli za Serikali kuhusu ufafanuzi wa mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa 19, maswali ya msingi 724, maswali ya nyongeza 2,699 na maswali matano ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu yaliulizwa na kupatiwa majibu ya Serikali. Aidha, katika kipindi cha Bunge la 12 linalohitimisha uhai wake, jumla ya maswali ya msingi 5,259 na maswali ya nyongeza 18,075 pamoja na jumla ya maswali 253 ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kupatiwa majibu na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia Bunge lilijadili na kupitisha miswada 58 kwa hatua zake zote. Wakati huo Bunge lako Tukufu lilijadili na kupitisha maazimio 19 ya Bunge ikiwemo ya pongezi manne, kuridhia mikataba ya itifaki 12 na masuala ya maliasili matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Bunge lako Tukufu lilipitisha maazimio 922 yanayotokana na taarifa za Kamati za mwaka yanayohitaji kutekelezwa na Serikali wakati wa uhai wake wa Bunge. Vilevile Serikali imetoa taarifa 15 kupitia kauli za Mawaziri Bungeni kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa mambo mbalimbali yenye maslahi tofauti na mapana kwa Taifa letu. Lengo hapa ni kuweka uwazi katika utendaji wa uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi kupitia wawakilishi wake hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi hii tarehe 26 Juni, Serikali imewasilisha mezani Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025/2050 na dira hiyo itakuwa zana muhimu itakayotoa mwelekeo wa Taifa kwa miaka 25 ijayo. Nitumie fursa hii, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tunaporudi majimboni tukawe mabalozi wazuri kwa wananchi kuwaeleza mazuri yaliyopo kwenye hiyo dira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nieleze utakelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka uliopita wa 2024/2025. Kipekee nataka niendelee kuwapongeza watendaji wote wa Serikali kwa kutekeleza kikamilifu Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mtakumbuka tarehe 12 Juni, 2025 Mheshimiwa Waziri wa

Mipango na Uwekezaji pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha walieleza bayana kwenye hotuba zao mafanikio yaliyopatikana na kwa hakika utekelezaji wake umefanyika kwa ufanisi na kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa pongezi kwa mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu alipoingia madarakani, alibainisha falsafa ya "Kazi Iendelee." Sote tu mashuhuda falsafa hiyo ameitekeleza kwa vitendo kwa kukamilisha miradi iliyokuwepo na kuibua mipya. Wenye macho hawaambiwi tazama, mafanikio makubwa yamepatikana kwenye sekta mbalimbali na siri ya mafanikio hayo ni uongozi thabiti wa Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu nilieleza mafanikio yaliyopatikana katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta mbalimbali kwa upana na uwazi ikiwemo sekta za afya, elimu, maji, kilimo, nishati, ujenzi wa miundombinu, umeme, michezo na uchukuzi. Vilevile Waheshimiwa Mawaziri wakati wakiwasilisha bajeti zao walieleza kwa kina juu ya mafanikio yaliyopatikana kwenye sekta zao. Sikusudii kuyarudia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine tumeshuhudia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla wakimpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya. Nami niungane nanyi kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti uliowezesha nchi yetu kupata mafanikio makubwa ambayo tunayo kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chini ya falsafa ya *4R* na umuhimu wake nchini tumeona namna ambavyo Rais wetu alipoingia madarakani aliitambulisha falsafa ya *4R* yaani *Reconciliation* (Maridhiano), *Resiliency* (Ustahimilivu), *Reform* (Mabadiliko) na *Rebuilding* (Kujenga upya) ikiwa ndiyo dira ya kisera iliyolenga kuijenga upya Tanzania yenye mshikamano, lakini pia nchi yenye haki na maendeleo

endelevu kwa misingi ya demokrasia na ushirikishwaji wa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuendelea kumpongeza Rais wetu kwa kuimarisha uhusiano wa kimataifa na kidiplomasia ya uchumi. Maono yake katika kufikia azma ya kuiunganisha Tanzania na mataifa mengine kiuchumi na kisiasa yamewezesha kupata mafanikio makubwa yakiwemo haya yafuatayo: -

(i) Kushiriki kikamilifu katika mikutano, makongamano na majukwaa mbalimbali yanayolenga kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika kukabiliana na changamoto za kidunia. Mathalani, Tanzania ilishiriki kikamilifu katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi Tajiri Duniani za Kundi la *G20* uliofanyika Rio de Janeiro, Brazil; na Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi *(COP 29)*. *(Makofi)*

(ii) Kuandaa na kuratibu mikutano, makongamano na majukwaa ya kimataifa ikiwemo Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika kuhusu Nishati *(Africa Energy Summit 2025)* na Mkutano wa Jukwaa la Mfumo wa Chakula Afrika *(AGRF – Africa Food Systems Summit 2023)*. *(Makofi)*

(iii) Tumeratibu ziara za kimkakati za viongozi wa kitaifa nje ya nchi pamoja na kupokea viongozi wa kimataifa waliotembelea nchini kwetu. Ziara hizo zimefanikisha kufikiwa kwa makubaliano kadhaa na kusainiwa mikataba ya ushirikiano kwa ajili ya ufadhili wa miradi ya maendeleo katika sekta za kipaumbele. Mikataba hiyo ni pamoja na mkataba kati ya China, Zambia na Tanzania kwa lengo la kufufua reli ya *TAZARA* ili kuboresha huduma za reli hiyo. *(Makofi)*

(iv) Mheshimiwa Rais wetu kupokea Uenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* yenye jukumu la kusimamia masuala ya ulinzi na usalama. Chini ya Uenyekiti wake, pamoja na masuala mengine, tumeweza kusimamia uangalizi wa chaguzi kwenye nchi za Botswana, Mauritius, Msumbiji vilevile Namibia.

(v) Tumeweza kuongeza ushawishi wa Tanzania katika medani za kimataifa uliowezesha kushika nafasi za uongozi katika Mashirika ya Kikanda. Mathalani, Dkt. Ntuli Angyelile Kapologwe aliyechaguliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Jumuiya ya Afya, Nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini pamoja na Profesa Mohamed Yakub Janabi, kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika. Haya yote ni sehemu ya mafanikio makubwa ambayo tumeyafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie tuzo za Kimataifa ambazo zinatambua mchango wa nchi yetu na Rais wetu katika utendaji kazi kwenye maeneo mbalimbali. Kama nilivyoeleza hapo awali yapo mafanikio mbalimbali yamepatikana katika Serikali ya Awamu ya Sita, hii ni kutokana na maono na uongozi thabiti wa Rais wetu, taasisi mbalimbali za kimataifa na kitaifa zimeona na kutambua mchango wa Rais wetu na kutoa tuzo zikiwemo hizi zifuatazo:

Mheshimiwa Spika, kuna zile tuzo za Kimataifa, kwanza, kwenye sekta ya afya; tarehe 4 Februari, 2025 Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokea tuzo ya *Global Gates Goalkeepers*, tuzo hii inatambua uongozi na mchango wake katika kuimarisha afya za uzazi na kupunguza vifo vya mama na mtoto hapa nchini. Aidha, Mheshimiwa Rais ndiye kiongozi wa kwanza kupokea tuzo hiyo Barani Afrika, jambo lililochochea kwa uongozi wake mahiri na kufanya mataifa makubwa duniani yatambue mchango wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili ni katika sekta ya miundombinu; siku ya tarehe 25 Mei, 2022 Mheshimiwa Rais alipokea tuzo ya Babacar Ndiaye kwa mwaka 2022, kuonesha kwamba dunia inatambua jitihada anazozifanya katika ujenzi wa miundombinu bora hapa nchini. Tuzo ya Babacar Ndiaye hutolewa kwa watu mashuhuri duniani walioonesha dhamira ya kuendeleza sekta ya miundombinu ya usafiri kwenye nchi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu ni kwenye sekta ya sanaa; tarehe 19 Novemba, 2022 Mheshimiwa Rais alikabidhiwa tuzo ya Uongozi Kimageuzi Afrika *(African Leaders Award 2022)* kutoka Taasisi ya *AFRIMMA* ya Mjini Dallas, Marekani kwa kutambua mchango wake katika sanaa nchini Tanzania. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia alitumia siku nane nje ya ofisi kuandaa filamu ya Tanzania "*The Royal Tour*" ambayo alikuwa anaongoza watalii akiionesha dunia uzuri wa Tanzania. *(Makofi)*

Vilevile katika kipindi kifupi cha uongozi wake alifanya mageuzi makubwa katika sekta ya sanaa ikiwemo kurejesha tuzo za muziki na kuboresha mifumo ya mirabaha ili kuwainua wasanii hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne ni kwenye sekta ya utalii; siku ya tarehe 10 Septemba 2022, Mheshimiwa Rais alipewa tuzo ya heshima ya *Pyne Africa Awards 2022*, Jijini Lagos, Nigeria akitambuliwa kuwa kiongozi bora, muwajibikaji katika kuendeleza sekta ya utalii Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tano, siku ya tarehe 11 Desemba, 2022, Taasisi ya *International Iconic* ya India, nchi ambayo ni maarufu katika soko la Kimataifa la filamu Duniani, ilimtunuku Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mshindi wa tuzo ya mwongoza watalii bora. Tuzo hii ilitolewa na kutambua na kuthamini mchango wake na kuwa muhusika mkuu kwenye filamu ya "*The Royal Tour.*" Filamu hiyo ilitangaza vivutio vya utalii vya Tanzania, hivyo kuchochea ongezeko la idadi ya watalii hapa nchini na ongezeko la mapato ya sekta hiyo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuzo za ndani ya Taifa; kama wasemavyo wahenga mcheza kwao hutuzwa, hivyo siyo tu taasisi za nje pekee bali hata taasisi za ndani zimetambua mchango wake na kutoa tuzo zikiwemo zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, moja, tarehe 31 Mei, 2025 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilimtunuku Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tuzo maalum ya heshima ya kitambua mchango wake katika kulitumikia Taifa na kuwaletea wananchi maendeleo. Hongera sana Spika, hongera sana Waheshimiwa Wabunge, hongera familia ya Bunge kwa tuzo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, tarehe 19 Juni, 2025 Mradi wa Simiyu Endelevu ulimtunuku Mheshimiwa Rais tuzo maalum ya kutambua dhamira yake thabiti ya kujenga Taifa linalostahimili mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima (Nanenane) ambayo kitaifa yalifanyika Agosti, 2023 kwenye Viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya, Mheshimiwa Rais alipokea tuzo maalum kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Mheshimiwa Makongoro Nyerere aliyeikabidhi kwa niaba ya wananchi wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa kutambua mchango wake katika kuendeleza sekta ya kilimo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, tarehe 1 Februari, 2025, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pia ilimtunuku Mheshimiwa Rais tuzo maalum ya kutambua mchango, maono na uongozi wake katika kuifanya elimu kama nguzo kuu ya maendeleo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tano, 11 Mei, 2024, Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania *(TRCS)* kilimtunuku Tuzo ya Ubinadamu Mheshimiwa Rais ikiwa ni kutambua na kuheshimu mchango wake katika masuala mbalimbali yanayogusa jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, huku kiongozi wetu, Rais wetu akipokea Shahada za Heshima kutoka Vyuo Vikuu mbalimbali. Nianze na shahada zilizotolewa kwa lengo la msukumo wa Wanazuoni katika Vyuo Vikuu vya Ndani na Nje ya Nchi, kumtunuku Shahada za Juu za Udaktari wa Heshima. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kuwa tarehe 30 Novemba, 2022 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilimtunuku Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa Mheshimiwa Rais na kutunukiwa shahada hiyo kutokana na mchango wake katika nyanja za elimu, afya na haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, vyuo vikuu vingine vya nchi za ughaibuni navyo vimetambua mchango wake katika maeneo mengine na kumtunuku Shahada za Udaktari wa Heshima, mnamo tarehe 10 Oktoba, 2023, alitunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa na Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru kilichopo New Dehli nchini India. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 28 Desemba, 2023 Chuo Kikuu cha Zanzibar *(SUZA)* kilimtunukia Mheshimiwa Rais Shahada ya Heshima ya Udaktari katika usimamizi wa utalii wa masoko. *SUZA* ilimtunuku tuzo hiyo kutokana na mchango wake mkubwa katika kuinua uchumi wa nchi kupitia sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Aprili, 2024 Rais wetu alitunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari katika Uchumi na Chuo Kikuu cha Ankara cha nchini Uturuki ikiwa ni ishara ya kutambua mchango wake katika kuboresha maisha ya Watanzania kupitia mageuzi mbalimbali, pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na nchi mbalimbali duniani ikiwemo nchi ya Uturuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 03 Juni, 2024, Rais wetu alitunukiwa Shahada ya Udaktari wa Falsafa ya Heshima kwa sekta ya anga na Rais wa Chuo Kikuu cha Sayansi ya Anga cha Jamhuri ya Korea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuzo hizi mbalimbali ni ushuhuda wa kazi kubwa inayofanywa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan na kutambulisha Taifa letu Kikanda na Kimataifa. Hakika kama nchi tunajivunia lulu hii na tunaendelea kuhakikisha kuwa Taifa na Watanzania kwa ujumla kwamba tunaitunza, tutaienzi na kuitunuku kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nitumie nafasi hii kutambua mchango wa watendaji wote ambao wametekeleza kwa vitendo, maono ya Rais wetu. Leo tunajivunia mafanikio makubwa katika utendaji wa Serikali kwa kila sekta hapa nchini. Mafanikio haya yanatokana na kujitoa kwao katika kuhakikisha mikakati na maono vinatekelezwa kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Naibu Mawaziri na Wakuu wa Wilaya kwa usimamizi wa majukumu yenu kulingana na dhamana mlizopewa. Pia nimpongeze Mheshimiwa Hamza Said Johari – Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kutuongoza vema katika ushauri, miongozo na kutafsiri sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka – Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu wote, Makatibu Tawala wa Mikoa na Naibu Makatibu Wakuu kwa ushirikiano mlioutoa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Waziri Mkuu kama msimamizi wa shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninamshukuru Dkt. Jim James Yonaz, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Bi. Mary Ngelela Maganga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu). Vilevile ninawashukuru Dkt. James Henry Kilabuko, Naibu Katibu Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) na Ndugu Zuhura Abdallah Yunus, Naibu Katibu Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu). Ninazishukuru sana Menejimenti za Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Ahsante sana kwa utumishi wenu uliotukuka. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yake kwetu,

kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu vizuri na kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa pongezi nyingi kwa Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama nikianza na Jenerali Jacob John Mkunda - Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Inspekta Jenerali wa Polisi Camillus Mongoso Wambura - Mkuu wa Jeshi la Polisi, Mkurugenzi Mkuu Suleimani Abubakar Mombo – Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Kamishna Jenerali wa Magereza Jeremiah Yoram Katungu - Mkuu wa Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Spika, vilevile niendelee kuwapongeza Kamishna Jenerali John William Masunga - Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Dkt. Anna Makakala - Mkuu wa Idara ya Uhamiaji, pia Mkurugenzi Mkuu Crispin Francis Chalamila - Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Kamishna Jenerali Aretas James Lyimo - Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa pongezi kwa wakuu wa taasisi na watumishi wote wa umma na sekta binafsi kwa kujituma na kutoa ushirikiano mzuri katika kufanikisha shughuli za Serikali, hakika jitihada zao zimewezesha kufanikisha yote ambayo yalikuwa yamepangwa katika nyanja mbalimbali ikiwemo kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe shukrani za dhati kwa viongozi wa dini kwa utayari wao katika kushirikiana na Serikali, huduma zenu za kiroho zimechangia hali ya utulivu na ustaarabu wa jamii ya Watanzania. Hivyo, ninaendelea kuwasihi viongozi wetu wa dini kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuleta amani, umoja na ushirikiano wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa ninawashukuru sana wananchi wote wa Tanzania kwa kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninakiri kwamba mmeonesha uzalendo, umoja na mshikamano wa

hali ya juu ulioiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana wananchi wote kwa juhudi kubwa katika shughuli za uzalishaji mali, uchumi wa nchi yetu umeendelea kuwa imara wakati wote, sina shaka hata kidogo upendo wenu kwa Serikali ya Awamu ya Sita umekuwa msukumo wa kujitoa kwenu, ninawaomba tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumpa kura nyingi na za kishindo katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu naomba sasa niweke msisitizo katika masuala muhimu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja, juu ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/2026; tarehe 24 Juni, 2025 ndani ya Bunge lako Tukufu sote kwa pamoja tulipitisha kwa kishindo bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Nitumie nafasi hii kusisitiza maeneo yafuatayo: -

(i) Maafisa Masuuli katika ngazi zote za umma wazingatie vipaumbele vilivyoainishwa kwenye bajeti iliyopitishwa na Bunge; na

(ii) Maafisa Masuuli wakamilishe miradi yote ambayo haijakamilishwa sambamba na kutekeleza ahadi za viongozi inayoekelezwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie Uchaguzi Mkuu mwaka huu 2025. Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, 2025. Ninatumia nafasi hii kuwakumbusha wadau mbalimbali kila mmoja kwa nafasi yake, ikiwemo wananchi ambao ni wapiga kura kushiriki kikamilifu katika uchaguzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai kwa kila mmoja wetu kuhakikisha analinda na kuitunza tunu ya amani na utulivu wa nchi yetu kabla, wakati na baada ya uchaguzi. Kwa upande mwingine Serikali itahakikisha inatekeleza wajibu wake wa kusimamia Katiba, sheria na taratibu zilizowekwa ili kila mwananchi mwenye sifa ya kuchagua na kuchaguliwa aweze kutimiza haki yake ya kikatiba bila vikwazo vya aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya michezo; nianze na kukupongeza wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendesha mabonanza ya michezo. Ninafahamu mabonanza haya yameanza kufanyika tangu Januari, 2023 kwa lengo la kuwahamasisha Wabunge na watumishi wa Ofisi ya Bunge kujenga tabia ya kufanya mazoezi kama wanafamilia ya Taasisi ya Bunge. Vilevile, yanalenga kujenga na kuimarisha afya, umoja kama taasisi, na kuongeza tija katika kutekeleza majukumu ya kulitumikia Taifa letu kwa ufanisi. Pia ni fursa kwa wadau mbalimbali kushirikiana na familia ya Bunge pamoja na wananchi katika michezo na burudani kwa pamoja na Wabunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakupongeza sana kwa kutoa fursa hii kwa Waheshimiwa Wabunge kuonesha vipaji vyao katika michezo mbalimbali. Ama kwa hakika, hivi juzi Waheshimiwa Wabunge wameendelea kuonesha vipaji vyao kwa umahiri mkubwa na viwango vya hali ya juu vyenye ubora wa kitaifa na kimataifa. Ninawasihi kwamba wote tuendelee na mazoezi haya, yana nafasi nzuri kiafya na pia yanaimarisha mahusiano. Tumeshuhudia umahiri wa Waheshimiwa Wabunge kwenye michezo ya mipira, mbio, kuvuta kamba, kufukuza kuku, ulaji na unywaji wa kiasi pia na michezo ya ndani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie mwenendo wa mashindano ya Kimataifa ya michezo mbalimbali; katika miaka ya hivi karibuni, Tanzania imeendelea kujipambanua kama nchi yenye vipaji, ari na uwezo mkubwa katika michezo na kuzipeleka timu zetu kimataifa. Timu yetu ya soka ya Taifa ya wanaume - *Taifa Stars,*

imeonesha ushindani wa hali ya juu kwenye mashindano ya kimataifa ikiwemo rekodi za kuvutia kwenye mechi za kufuzu *AFCON* na hata kushinda timu ambazo zamani zilitazamwa kama vigogo wa soka Barani Afrika. Vivyo hivyo, timu ya wanawake, *Twiga Stars*, imeendelea kutoa taswira ya matumaini kwa wasichana wetu, wakionesha kuwa michezo si ya jinsia fulani bali ni ya kila mwanamichezo mwenye ndoto, bidii na moyo wa uzalendo.

Mheshimiwa Spika, vilabu vyetu vya mpira wa miguu nchini vimeendelea kupeperusha bendera ya Taifa letu kwa kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa na kuwa timu tishio Barani Afrika kwa sasa. Hapa nitambue kazi kubwa iliyofanywa na timu yetu ya Yanga kwa kuweza kupiga hatua muhimu kwenye Kombe la Mabingwa Barani Afrika na kufikia hatua ya makundi ya msimu wa mwaka 2024/2025 ambayo ni muhimu sana kwa ustawi na ubora wa ligi yetu.

Mheshimiwa Spika, jana tarehe 25 Juni, 2025 ulichezwa mchezo namba 184 wa Ligi Kuu ya *NBC* maarufu *Kariakoo Derby* kati ya Yanga na Simba katika dimba la Benjamin Mkapa maarufu kama Lupaso, mchezo huo ulimalizika kwa timu ya Yanga kuifunga Simba mabao mawili kwa bila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeombwa nirudie, ninaomba nirudie tena, jana tarehe 25 Juni, 2025 ulichezwa mchezo namba 184 wa Ligi Kuu ya *NBC* maarufu *Kariakoo Derby* kati ya Yanga na Simba katika dimba la Benjamin Mkapa maarufu kama Lupaso. Mchezo huo ulimalizika kwa timu ya Yanga kuifunga Simba mabao mawili kwa bila, yaliyofungwa na nyota Pacome Zouzou na kijana wetu wa Kitanzania Clement Mzize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niungane na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuipongeza timu ya Yanga kwa kutwaa ubingwa wa 31 wa Tanzania Bara, ikiwa ni ubingwa wa nne mfululizo. Aidha, niwatie moyo klabu ya Simba kwa kuendelea kupambana mpaka mechi ya mwisho na kuongeza ladha ya ligi yetu. Pia ninawapongeza wachezaji wote

wa timu zote za ligi hapa nchini, viongozi wa vilabu vya soka, pongezi sana, wadhamini na wafadhili wa michezo, hongera sana na viongozi wa Shirikisho letu la Mpira nchini *(TFF),* hongera sana kwa usimamizi mzuri kwenye mpira huu wa miguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, ninaipongeza sana Klabu ya Simba kwa hatua kubwa ya kutinga fainali katika Kombe la Shirikisho Barani Afrika kwa msimu wa 2024/2025. Timu hiyo ilihitimisha mchezo wake kwa sare ya goli moja kwa moja dhidi timu ya RS Berkane kutoka Morocco katika uwanja wa *New Amaan Zanzibar*, ninazipongeza sana timu zetu za Yanga na Simba kwa hatua kubwa ambazo wamefikia, pia ninaipongeza timu ya *Azam FC* ikifuatia kwa ubora na uwekezaji mzuri wa viwango katika soka la hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie maandalizi ya michezo ya *CHAN* na *AFCON* mwaka 2027. Mwaka huu 2025, Tanzania imepewa heshima ya kipekee kuwa mwenyeji wa michuano ya Ubingwa wa Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ligi za Ndani – *CHAN 2025*.

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali kupitia Wizara husika, kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF),* imeanza maandalizi ya kina ya kuhakikisha viwanja, miundombinu na huduma muhimu zinakidhi viwango vya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshapangiwa timu tano zitakuwa Benjamin Mkapa na timu nne zitakuwa *New Amaan Zanzibar.* Kwa hiyo, tuna timu tisa na vituo viwili hapa Tanzania lakini pia Tanzania itakuwa mwenyeji wa ufunguzi wa michezo ya *CHAN* mara tu itakapoanza mwezi wa nane.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Juni, 2025 ukarabati wa uwanja wa *New Amaan - Zanzibar* umekamilika; ujenzi wa uwanja wa Arusha umefikia 47%; na ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa umefikia 88%. Pamoja na jitihada za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya msingi, vilevile ukarabati wa viwanja vya mazoezi

unaendelea ambapo ukarabati wake umefikia 90%. Viwanja hivyo ni Gymkhana, Uwanja wa Chuo cha Sheria na Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo kule Mbweni.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/2025 wanamichezo na timu mbalimbali wamefanya vizuri katika mashindano ya Kimataifa na kuipeperusha vema Bendera ya Taifa. Baadhi ya timu na wanamichezo waliopeperusha Bendera ya Taifa na kuiletea heshima nchi yetu ni pamoja na hao wafuatao;

(a) Mabingwa wa Mashindano ya Wanawake ya Afrika Mashariki na Kati *(CECAFA Senior Women's Championship 2025)* na yenyewe imetuletea heshima Taifa letu;

(b) Timu ya Taifa ya Kriketi ya Wanaume chini ya miaka 19 ambayo imefuzu kucheza Kombe la Dunia ambalo litafanyika katika nchi za Zimbabwe na Namibia mwaka 2026;

(c) Timu ya Taifa ya Wanawake ya Mchezo wa Futsal ilishika nafasi ya pili katika mashindano ya Afrika na imefuzu kucheza Kombe la Dunia nchini Ufilipino mwezi Novemba, 2025;

(d) Klabu ya Simba ilifika hatua ya Fainali ya Kombe la Shirikisho la *CAF* na kuwa mshindi wa pili baada ya kupoteza mchezo wake na timu ya RS Berkane kutoka nchini Morocco;

(e) Timu ya Taifa ya Wasichana ya Mpira wa Kikapu ya umri chini ya miaka 16 ilikuwa mshindi wa mashindano ya Afrika Mashariki ambayo yalifanyika Kibaha, mkoani Pwani mwaka 2024;

(f) Mwanariadha Alphonce Simbu alishika nafasi ya pili na kupata medali ya fedha katika mashindano ya Marathoni

ya Boston ambayo yalifanyika nchini Marekani mwezi Aprili, 2025.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba kutoa hoja ya shukrani; kwa unyenyekevu mkubwa sana ninamshukuru kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwanza kwa imani yake isiyopimika aliyoionesha kwangu tangu aliposhika hatamu ya kuliongoza Taifa hili. Kwa hakika ni jambo linaloweka historia isiyosahaulika kwangu binafsi, familia yangu na Wana-Ruangwa na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uniruhusu kwa unyenyekevu mkubwa nigusie jambo la kihistoria, lenye hisia na lenye uzito mkubwa kwa Taifa letu. Kama Taifa tuna kumbukumbu ya majonzi na maumivu makubwa tuliyoyapitia kwa tukio la tarehe 17 Machi, 2021 pale ambapo tulimpoteza kiongozi wetu kipenzi, Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Ukweli usiopingika ni kwamba tukio hili lilituacha sote tukiwa na majonzi, taharuki na giza nene.

Mheshimiwa Spika, katika giza hilo nene la huzuni lililogubika Taifa letu, Mwenyezi Mungu alimpa ushupavu, ujasiri na utulivu wa kipekee Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na akawa faraja kubwa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiongozi huyu alisimama imara katika upepo mkali wa historia ya nchi yetu, alichukua hatamu ya uongozi kwa utulivu, kwa busara na kwa ujasiri usioyumba. Katika kipindi hiki alitufundisha kuwa utulivu si udhaifu, bali ni nguvu ya ndani inayotoka kwa Mwenyezi Mungu katika kushughulika na masuala makubwa ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ndani na nje ya mipaka ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho kigumu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alinionesha imani kubwa na hatimaye aliamua niendelee kumsaidia kwa nafasi ya Waziri Mkuu. Hili si jambo

dogo. Ninayakumbuka maneno yake kwangu; ninamnukuu; "Kassim tuendelee kushirikiana kulitumikia Taifa letu, simamia shughuli za Serikali." Ninamshukuru kwa moyo wa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani aliyoionesha kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha uongozi wake, tumeweza kusimama imara kama Taifa, tumesimamia tunu za Taifa za amani na utulivu, tumeendeleza miradi ya maendeleo ya kimkakati ambayo mingine inaendelea kujengwa ikiwemo huduma za jamii, tumeimarisha demokrasia, tumeimarisha diplomasia, tumejenga uchumi na kujenga mshikamano wa kitaifa. Hayo yote yametokana na uongozi imara wenye hekima wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hivyo nimalizie kwa kusema kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa mwalimu wa subira, kielelezo cha ujasiri, ustahimilivu na alama ya matumaini kwa kizazi hiki na kiongozi aliyetoa mfano wa kuwa mwanamke anaweza kuongoza hata kwenye nafasi ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninaomba nimnukuu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne alisema "Hapa Tanzania leo hakuna mwanasiasa maarufu kama Rais Samia iwe ndani ya chama ama nje ya Chama Cha Mapinduzi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, daima nitaendelea kumshukuru na ninamuombea ushindi mkubwa kwenye uchaguzi mkuu ujao. Vilevile ninawaombea ushindi wa kishindo Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Mgombea Mwenza wa nafasi ya Urais na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Mgombea wa Urais Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kutumia nafasi hii pia kukupongeza sana wewe binafsi kwa namna ulivyoendesha Bunge hili kwa weledi, busara na ujasiri wa hali ya juu. Katika kipindi cha uongozi wako katika Bunge hili, sote tumeshuhudia imani kubwa ya dunia kwa nchi yetu kupitia wewe Mheshimiwa Spika wetu pale

ambapo Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)* ulipoamua kukupa dhamana kubwa ya kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Hili si jambo dogo, bali pia kuchaguliwa kwako sio tu kumeliheshimisha Taifa letu pekee, bali kumeliheshimisha Bunge letu ambalo ndilo lilianza kuonesha imani kwako na kujivunia. Vilevile, umewaheshimisha Wana-Mbeya Mjini kama wapiga kura wako ambapo ndiyo jimbo lako kuwa wewe ndiye kiongozi bora na mahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa umefunga mkanda wa kazi na upo tayari katika kuwahudumia wananchi wa jimbo lako jipya la Uyole baada ya kufanya vizuri Jimbo la Mbeya Mjini. Sina shaka kuwa wananchi wanasubiri kwa hamu kubwa kukupa ridhaa ya kuwawakilisha katika chombo hiki na majukumu uliyopewa kwa ngazi ya kimataifa. Niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kukutakia kila la kheri katika uchaguzi mkuu ujao. Ninaomba Wana-Uyole mrudisheni Mheshimiwa Spika wetu Bungeni ili aje kuwakilisha vizuri na aweze kuendesha Bunge letu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niendelee kumpongeza Naibu Spika wa Bunge letu Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala. Naye tunamuombea kila la kheri kwenye mchakato ujao upate ushindi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru na kuwatakia ushindi mnono Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mbunge); Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama (Mbunge); na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika (Mbunge). Tunawaomba wapiga kura wawape kura za kutosha ili warudi tena Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamtakia kila la kheri Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ili wananchi wa Bukombe waweze kukupitisha na kukupa kura za kutosha uweze kushinda. Umekuwa msaada sana kwangu katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hongera sana,

kila la kheri na *In Shaa Allah* Mwenyezi Mungu atakurudisha katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kutambua kazi kubwa iliyofanywa na Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na wasaidizi wote. Kwa Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Naibu Mawaziri ninawaombea ushindi mwema na wa kishindo. *In Shaa Allah* mtashinda kwa ushindi mnono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninaomba nimuombee kibali kwa Mwenyezi Mungu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge wa Ismani. Tunakuombea kila la kheri, Wana-Ismani wakupigie kura nyingi za ndiyo na urudi tena Bungeni. Pia Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete kule Chalinze ninawaombea sana Wana-Chalinze mtende mema kwa Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Mrisho Kikwete ili arudi tena hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Pascal Patrobass Katambi kule Shinyanga Mjini naye pia ninamuombea kila la kheri ili apate kura nyingi na aweze kurudi tena Bungeni pamoja na dada yetu Mheshimiwa Ummy Nderiananga kutoka kundi maalum ili aweze kupata kura za kutosha na aendelee kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Naibu Mawaziri nirudie tena, ninaamini Mwenyezi Mungu ataendelea kuwaongoza katika kuomba, lakini wanajimbo waweze kuwarudisha kwa kura nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nirudie tena kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano mkubwa mlionipa wakati wote nikitekeleza majukumu yangu. Nami ninawatakia ushindi wa kishindo kwenye majimbo yenu kwenye kinyang'anyiro kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kura za maoni mshinde, lakini pili mpigiwe kura nyingi kwenye uchaguzi mkuu muweze kurudi tena

hapa Bungeni muweze kuja kuwakilisha wananchi wenu. *In Shaa Allah* Mwenyezi Mungu mtapigiwa kura wote za ndiyo na za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, ninampongeza Ndugu Baraka Ildephonce Leonard, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa shughuli za Bunge. Ninawapongeza pia watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kazi kubwa na nzuri ya kuandaa, kuratibu na kusimamia mwenendo wa shughuli za Bunge na kutoa huduma stahiki kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninawapongeza wanahabari kwa kazi kubwa ya kuuhabarisha umma kwa uwazi, uaminifu na weledi wa hali ya juu katika kipindi chote cha mkutano na mnaendelea na jukumu hili kuwahabarisha Watanzania nini hasa kinasibu katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawapongeza na kuwashukuru madereva wetu waliofanya kazi nzuri kusimamia uhai wetu na usalama wa Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuja Bungeni Dodoma na kurudi pia kwenye majimbo. Hii ni pamoja na watoa huduma wengine waliotuhudumia katika kipindi chote cha Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwa tunaelekea kuhitimisha Mkutano huu wa 19 wa Bunge la 12, nikiri kuwa Bunge hili limefanya kazi kwa bidii, tumetafakari hoja, tumejadili miswada na tumetoa maazimio yenye tija kwa maendeleo ya nchi yetu. Ni wakati sasa wa kurejea majimboni ili kujiandaa na Uchaguzi Mkuu. Ni matumaini yangu kwamba wananchi watatupa ridhaa kwa mara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninaomba kutoa hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**26 JUNI, 2025**

**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA KUHITIMISHA MKUTANO WA 19 WA BUNGE LA 12 LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TAREHE 26 JUNI, 2025 JIJINI DODOMA KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa fadhili zake zilizotuwezesha kuiona siku hii muhimu katika historia ya Bunge la 12. Kama mnavyofahamu, tumekutana leo kwa ajili ya kuhitimisha mkutano wa 19 ambao ulikuwa mahsusi kwa ajili ya kupokea na kujadili bajeti ya serikali.

**2.** Kipekee nitumie nafasi hii kukushukuru sana wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge wa Mbeya Mjini, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. Hakika umekuwa kiongozi shupavu na umeonesha weledi mkubwa katika kuliongoza Bunge hili la 12.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzoefu wako wakati wote umekuwa na tija kubwa katika utendaji wa shughuli za serikali bungeni. Ninakushukuru sana kwa namna ulivyoendesha mijadala yote ya bajeti za kisekta katika mkutano huu wa 19 pamoja na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2025/2026.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nitumie nafasi hii kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala na Naibu wa Spika pamoja na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mbunge wa Viti Maalum), Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika Mbunge wa Njombe Mjini kwa nafasi zao za Mwenyekiti wa Bunge. Wakati wote mmekuwa mkinipa ushirikiano wa kutosha wakati mlipokuwa mkimsadia Mheshimiwa Spika katika shughuli za kuendesha Bunge. Ahsanteni sana.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Kwa kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za Bunge la 12 Waheshimiwa wabunge mmefanya kazi kubwa, hakika mnastahili pongezi. Maoni, ushauri na michango yenu katika mkutano huu wa bajeti licha ya kugusa maisha ya wananchi wote imekuwa ikitoa mwelekeo sahihi katika mipango na utendaji wa shughuli za Serikali. Pia ninawapongeza kwa kazi kubwa mliyoifanya tarehe 24 Juni, 2025 ya kupitisha kwa kura ya ndiyo Bajeti ya Serikali ya mwaka 2025/2026 ya shilingi trilioni 56.49 kwa asilimia 98.7. Hakika ninyi ni wazalendo, mmevunja rekodi, mnaipenda nchi yenu na mnathamini kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Niendelee kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano, mshikamano mlionipa wakati wote nikiwa natekeleza jukumu langu la Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Sitawasahau na sitasahau upendo wenu kwangu Inshaalah Mwenyezi Mungu atawajaalia kila lenye kheri katika kila jambo lenu.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakifanya ufuatiliaji wa miradi kwenye majimbo yenu kwa karibu mno. Kila mbunge aliwajibika katika kuhakikisha upatikanaji wa maendeleo ya haraka kwa lengo la kuinua ustawi wa wananchi wote.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama Waswahili wasemavyo, "*kila mtenda wema atakumbukwa kwa wema*" niwaombe wananchi wote eendeleni kuwaunga mkono Wabunge wetu huko majimboni. Hakika waheshimiwa wabunge mmetenda mema kwa kuwakilisha vema majimbo yenu na mnastahili kukumbukwa kwa wema wenu.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na taadhima, ninaomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake uliotukuka. Wakati wote amekuwa akinipa maelekezo yenye tija na kuifanya kazi yangu kuwa nyepesi.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** sina shaka nyote mtakubaliana nami kuwa hulka yake na ustahimilivu wake umekuwa faraja kwetu sisi wasaidizi wake, watumishi wote wa umma na Watanzania wote kwa ujumla. Isitoshe, Mheshimiwa Rais wakati wote amekuwa nguzo ya kuimarisha mshikamano na umoja wa kitaifa.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano wake alionipatia wakati wote nikitekeleza majukumu yangu. Busara zake na weledi wake umekuwa msaada na mfano wa kuigwa katika utendaji kazi Serikalini.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushirikiano mkubwa alionipatia wakati wote. Kadhalika, ninatoa shukrani kwa Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar pamoja na Ofisi yote ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ushirikiano wakati nikitekeleza majukumu yangu.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, niendelee kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa ushirikiano mkubwa katika usimamizi na uratibu wa shughuli za Serikali. Nikiri kwamba Mheshimiwa Biteko amekuwa msaada mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ufanisi.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba sasa nitumie nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi (Mb.) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga (Mb.), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa kazi nzuri waliyoifanya. Pia, ninawashukuru kwa kunisaidia kutekeleza majukumu yangu wanaposimamia dhamana ya Sera, Bunge na Uratibu katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, na Mheshimiwa Patrobas Paschal Katambi (Mb.), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, kwa kunisaidia kusimamia dhamana ya Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Ushirikiano wao umekuwa chachu ya mafanikio katika shughuli za kila siku za Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa mara nyingine ninawashukuru sana.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru sana wana Ruangwa kwa kuniunga mkono na kunipatia ushirikiano katika kipindi chote nilipokuwa nikitekeleza majukumu ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninatambua wakati mwingi nimekuwa nje ya jimbo nikilitumikia taifa lakini wana Ruangwa wameendelea kuniunga mkono. Nitumie nafasi hii kusema asanteni sana na ninamuomba Mwenyezi Mungu azidi kuimarisha mshikamano uliopo kati yetu sote. Ninaomba kuwajulisha kuwa ninakuja kuchukua fomu ya kuomba ridhaa yenu tena.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee, ninaishukuru sana familia yangu ikiongozwa na Mke wangu mpendwa, Mama Mary Majaliwa na watoto wangu kwa upendo na uvumilivu waliouonesha kwangu wakati wote hata pale nilipopitia magumu mliendelea kunionesha upendo wenu. Kwa hakika upendo na mshikamano wenu umekuwa ukinipa nguvu ya kutekeleza majukumu yangu ya kumsaidia kazi Mheshimiwa Rais na kuwatumikia Watanzania. Asanteni sana!

## 2.0 SALAMU ZA PONGEZI

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati mkutano wa 19 wa Bunge ukiendelea, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya teuzi mbalimbali. Teuzi hizo zilifanywa kwa lengo la kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi na shughuli mbalimbali za serikali na mihimili mingine.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** mnamo tarehe 13 Juni, 2025 alimteua Mheshimiwa George Mcheche Masaju aliyekuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania. Mheshimiwa Masaju amechukua nafasi ya Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma ambaye amestaafu na kwa hakika amefanya kazi kubwa iliyoacha alama katika muhimili wa mahakama. Ninamtakia kila la heri Prof. Ibrahim Juma katika maisha ya ustaafu.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Jaji Masaju pamoja na viongozi wote wateule na katika nafasi mbalimbali. Aidha, nitumie nafasi hii kuwatakia wateule wote kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya na kuwakumbusha wajibu wao wa kutanguliza mbele maslahi taifa letu na wananchi wote kwa ujumla.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa katika mkutano wa Shirika la Afya Duniani wa Mei 18, 2025 Geneva, Uswisi pamoja na masuala mengine ulifanyika uchaguzi wa kumpata Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika. Kwa mara ya nyingine, Tanzania iliendelea kung'ara kimataifa baada ya Profesa Mohamed Yakubu Janabi, Mshauri wa Rais wa Masuala ya Tiba na Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika baada ya kuwashinda wagombea kutoka Nchi za Ivory Coast, Guinea, Niger na Togo.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaungana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Watanzania wote kumpongeza Profesa Mohamed Janabi, kwa ushindi huo. Nafasi hii imeipa Tanzania heshima kubwa kwani imedhihirisha uwezo wa kuandaa viongozi wenye weledi ambao wanaweza kumudu ushindani wa kimataifa.

## 3.0 SALAMU ZA POLE

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati tukiendelea na mkutano huu wa 19 wa Bunge lako tukufu, mnamo tarehe 7 Mei, 2025 tuliondokewa na mwanasiasa mashuhuri na mkongwe Mheshimiwa Cleopa David

Msuya. Mheshimiwa Msuya aliwahi kulitumikia Bunge hili akiwakilisha Jimbo la Mwanga.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, Mheshimiwa Msuya amewahi kuhudumu serikalini katika nafasi mbalimbali. Kuanzia mwaka 1964 hadi 1972 alihudumu nafasi ya Katibu Mkuu katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Utamaduni, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Maji, Wizara ya Mambo ya Uchumi na Mipango, pamoja na Wizara ya Fedha.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile mwaka 1972 hadi 1994 alikuwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Viwanda, Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango, Waziri wa Viwanda na Biashara. Pia, amewahi kuwa Waziri Mkuu kwa vipindi viwili tofauti mwaka 1980 hadi 1983 na mwaka 1994 hadi 1995 ambapo alihudumu kama Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** nami niungane Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa salamu za pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki. Pia, ninatoa pole nyingi kwa wananchi wa Mwanga, wana CCM na Watanzania wote kwa ujumla. Tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa marehemu pumziko la amani. Amina.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** wapo Watanzania wenzetu waliokumbwa na majanga mbalimbali zikiwemo ajali za barabarani. Ninatoa pole kwa wananchi wote waliopoteza wapendwa wao katika ajali hizo. Vilevile, ninatoa pole kwa majeruhi wote na ninamwomba Mwenyezi Mungu awape uponyaji wa haraka. Nitumie nafasi hii pia, kutoa pole kwa waathirika wa majanga yote yaliyotukia.

## 4.0 SHUGHULI ZA BUNGE

### Maswali na Majibu

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati Bunge la 12 likielekea kuhitimisha shughuli zake, limefanikiwa kutekeleza masuala mbalimbali ikiwemo

kujibu maswali na hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge; kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria ya Serikali; kujadili na kutoa Maazimio mbalimbali; kujadili na kuridhia Mikataba na Itifaki za Kikanda na Kimataifa; pamoja na kupokea kauli za Serikali kuhusu ufafanuzi wa mambo mbalimbali.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mkutano wa 19, maswali ya msingi 724, nyongeza 2,699 na maswali 5 ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu yaliulizwa na kupatiwa majibu ya Serikali. Aidha, katika kipindi cha Bunge la 12 linalohitimisha uhai wake, jumla ya maswali ya msingi 5,057 na Maswali ya nyongeza 15,000 pamoja na jumla ya maswali 260 ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kupatiwa majibu na Serikali.

**Miswada, Maazimio na Taarifa za Serikali**

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Bunge lilijadili na kupitisha Miswada 60 kwa hatua zake zote. Wakati huohuo, Bunge lako tukufu lilijadili na kuridhia Mikataba, Maazimio na Itifaki mbalimbali za Kimataifa kumi na sita (16). Pia, Hoja Binafsi 4 za Wabunge ziliwasilishwa na kujadiliwa.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hayo Bunge lako tukufu lilipitisha Maazimio 922 yanayotokana na taarifa za Kamati za Mwaka yaliyohitaji kutekelezwa na Serikali wakati wa uhai wa Bunge. Vilevile, Serikali imetoa taarifa 15 kupitia kauli za Mawaziri Bungeni kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa mambo tofauti yenye maslahi mapana kwa Taifa. Lengo ni kuwepo kwa uwazi katika utendaji na uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi kupitia wawakilishi wake Bungeni.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** leo asubuhi tarehe 26 Juni, 2025 Serikali imewasilisha mezani Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025 - 2050. Dira hiyo itakuwa zana muhimu itakayotoa mwelekeo wa Taifa kwa miaka ishirini na tano (25) ijayo. Nitumie fursa hii, niwaombe wabunge wenzangu tunaporudi majimboni tukawe mabalozi wazuri kwa wananchi kueleza mazuri yaliyopo kwenye dira hiyo.

## 5.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA 2024/2025

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee niwapongeze watendaji wote wa Serikali kwa kutekeleza kikamilifu Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mtakumbuka tarehe 12 Juni, 2025, Waziri wa Mipango na Uwekezaji na Waziri wa Fedha walielezea bayana kwenye hotuba zao mafanikio yaliyopatikana na kwa hakika utekelezaji wake umefanyika kwa ufanisi na kiwango kikubwa.

## 6.0 PONGEZI KWA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani alibainisha falsafa ya Kazi Iendelee. Sote tu mashuhuda falsafa hiyo ameitekeleza kwa vitendo kwa kukamilisha miradi iliyokuwepo na kuibua mipya. Mwenye macho haambiwi tazama, mafanikio makubwa yamepatikana kwenye sekta mbalimbali. Siri ya mafanikio hayo ni uongozi thabiti wa Mheshimiwa Rais.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu nilieleza mafanikio yaliyopatikana katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta za afya, elimu, maji, kilimo, nishati, michezo, ujenzi na uchukuzi. Vilevile, waheshimiwa mawaziri wakati wakiwasilisha bajeti za wizara zao walieleza kwa kina mafanikio hayo.

**35.** ***Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine tumeshuhudia*** waheshimiwa wabunge na wananchi kwa ujumla wakimpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. Nami niungane nanyi kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti uliowezesha nchi yetu kupata mafanikio makubwa.

### Falsafa ya 4R na umuhimu wake nchini

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani aliitambulisha falsafa ya 4R yaani *Reconciliation* (Maridhiano), *Resiliency* (Ustahimilivu), *Reform* (Mabadiliko) na *Rebuilding* (Kujenga upya) ikiwa ni dira ya kisera iliyolenga kuijenga upya Tanzania yenye mshikamano, haki na maendeleo endelevu kwa misingi ya demokrasia na ushirikishwaji wa wananchi.

**Diplomasia ya Kiuchumi na Ushirikiano wa Kimataifa**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha uhusiano wa kimataifa na diplomasia ya uchumi. Maono yake katika kufikia azma ya kuiunganisha Tanzania na mataifa mengine kiuchumi na kisiasa yamewezesha kupata mafanikio makubwa ikiwemo yafuatayo:

Moja: Kushiriki kikamilifu katika mikutano, makongamano na majukwaa mbalimbali yanayolenga kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika kukabiliana na changamoto za kidunia. Mathalan, Tanzania ilishiriki kikamilifu katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi Tajiri Duniani za Kundi la G20 uliofanyika Rio de Janeiro, Brazil; Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi (COP 29).

Mbili: Kuandaa na kuratibu mikutano, makongamano na majukwaa ya kimataifa ikiwemo Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Afrika kuhusu Nishati (Africa Energy Summit 2025) na Mkutano wa Jukwaa la Mfumo wa Chakula Afrika (AGRF- Africa Food Systems Summit 2023).

Tatu: Kuratibu ziara za kimkakati za viongozi wa kitaifa nje ya nchi pamoja na kupokea viongozi wa kimataifa waliotembelea nchi. Ziara hizo zimefanikisha kufikiwa kwa makubaliano na kusainiwa mikataba ya ushirikiano kwa ajili ya ufadhili wa miradi ya maendeleo katika sekta za kipaumbele. Mikataba hiyo ni pamoja na mkataba kati ya China, Zambia na

Tanzania kwa lengo la kufufua reli ya TAZARA ili kuboresha huduma za reli hiyo.

Nne: Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupokea Uenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC), yenye jukumu la kusimamia masuala ya ulinzi na usalama. Chini ya uenyekiti wake, pamoja na masuala mengine, tumeweza kusimamia uangalizi wa chaguzi kwenye nchi za Botswana, Mauritius, Msumbiji na Namibia.

Tano: Kuongezeka kwa ushawishi wa Tanzania katika medani za kimataifa, uliowezesha kushika nafasi za uongozi katika mashirika ya kikanda. Mathalani Dkt. Ntuli Angyelile Kapologwe aliyechaguliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Jumuiya ya Afya Nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini pamoja na Prof. Mohamed Yakubu Janabi kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika.

**Tuzo za Kimataifa na Kitaifa za Kutambua Mchango wa Mheshimiwa Rais**

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza hapo awali, yapo mafanikio mbalimbali yamepatikana katika Serikali ya Awamu ya Sita kutokana na maono na uongozi thabiti wa Mheshimiwa Rais. Taasisi mbalimbali za kimataifa na kitaifa zimeona na kutambua mchango wa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kutoa tuzo zikiwemo zifuatazo:

**Tuzo za Kimataifa**

Moja: Kwenye Sekta ya Afya, tarehe 4 Februari, 2025 Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokea Tuzo ya *Global Gates Goalkeepers*. Tuzo hii inatambua uongozi na mchango wake katika kuimarisha afya ya uzazi na kupunguza vifo vya mama na mtoto nchini. Aidha, Rais Samia ndiye kiongozi wa kwanza kupokea tuzo hiyo Barani Afrika jambo lililochochewa na

uongozi wake mahiri na kufanya mataifa makubwa duniani yatambue mchango wake.

Mbili: Kwenye Sekta ya Miundombinu, tarehe 25 Mei 2022, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokea Tuzo ya Babacar Ndiaye kwa mwaka 2022 kuonesha kwamba dunia imetambua jitihada anazozifanya katika ujenzi wa miundombinu bora nchini. Tuzo ya Babacar Ndiaye, hutolewa kwa watu mashuhuri duniani walioonesha dhamira ya kuendeleza sekta ya miundombinu ya usafiri.

Tatu: Kwenye sekta ya sanaa, tarehe 19 Novemba 2022, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alikabidhiwa Tuzo ya Uongozi wa Kimageuzi Afrika (*African Leadership Award 2022*), kutoka taasisi ya AFRIMMA ya mjini Dallas, Marekani kwa kutambua mchango wake katika sanaa nchini Tanzania. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia alitumia siku nane nje ya ofisi kuandaa filamu ya Tanzania: "*The Royal Tour*" ambayo alikuwa mwongoza watalii akiionesha dunia uzuri wa Tanzania. Vilevile, katika kipindi kifupi cha uongozi wake, alifanya mageuzi makubwa katika sekta ya sanaa ikiwemo kurejesha tuzo za muziki na kuboresha mifumo ya mirahaba ili kuwainua wasanii nchini.

Nne: Kwenye sekta ya utalii, tarehe 10 Septemba 2022, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipewa Tuzo ya Heshima ya *Pyne Africa Awards* 2022 jijini Lagos, Nigeria akitambuliwa kuwa kiongozi bora, muwajibikaji katika kuendeleza sekta ya utalii barani Afrika.

Tano: Tarehe 11 Desemba, 2022 taasisi ya International Iconic ya India, nchi ambayo ni maarufu katika soko la kimataifa la filamu duniani, ilimtunuku Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mshindi wa Tuzo ya Muongoza Watalii Bora. Tuzo hiyo ilitolewa kwa kutambua na kuthamini mchango wake na kuwa mhusika mkuu kwenye filamu ya "*The Royal Tour*". Filamu hiyo ilitangaza vivutio vya utalii vya Tanzania

hivyo kuchochea ongezeko la idadi ya watalii nchini na ongezeko la mapato kwenye sekta hiyo.

**Tuzo za Kitaifa**

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama wasemavyo Wahenga "*Mcheza kwao hutuzwa*", hivyo siyo tu taasisi za nje pekee, bali hata taasisi za ndani zimetambua mchango wake na kutoa tuzo ikiwemo zifuatazo:-

Moja: Tarehe 31 Mei, 2025, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lilimtunuku Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Tuzo Maalum ya Heshima ya kutambua mchango wake katika kulitumikia Taifa na kuwaletea wananchi maendeleo.

Mbili: Tarehe 19 Juni 2025, Mradi wa Simiyu Endelevu ulimtunuku Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Tuzo Maalum ya kutambua dhamira yake thabiti ya kujenga Taifa linalostahimili Mabadiliko ya Tabianchi.

Tatu: Wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima Nanenane ambayo Kitaifa yalifanyika Agosti, 2023 kwenye Viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya Mheshimiwa Rais alipokea tuzo maalumu kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Mheshimiwa Makongoro Nyerere aliyeikabidhi kwa niaba ya wananchi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa kutambua mchango wake katika kuendeleza sekta ya kilimo nchini.

Nne: Februari Mosi, 2025, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pia, ilimtunuku Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Tuzo Maalumu ya kutambua mchango, maono na uongozi wake katika kuifanya elimu kama nguzo kuu ya maendeleo ya nchi.

Tano: Mei 11, 2024 Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS) kilimtunuku Tuzo ya UBINADAMU Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ikiwa ni kutambua na kuheshimu mchango

wake katika masuala mbalimbali yanayogusa jamii ya Watanzania.

**Shahada za Heshima Kutoka Vyuo Vikuu Mbalimbali**

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada za Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyanja mbalimbali zimetoa msukumo kwa wanazuoni katika vyuo vikuu vya ndani na nje ya Tanzania kumtunuku Shahada ya Juu ya Udaktari wa Heshima. Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kuwa tarehe 30 Novemba 2022, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilimtunuku Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa. Mheshimiwa Rais alitunukiwa shahada hiyo kutokana na mchango wake katika nyanja za elimu, afya na haki za binadamu.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** licha ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, vyuo vikuu vingine vya nchi za ughaibuni navyo vimetambua mchango wake katika maeneo mengine na kumtunuku shahada za udaktari wa heshima. Mnamo tarehe 10 Oktoba, 2023 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa na Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru kilichopo New Delhi nchini India.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 28 Desemba, 2023, Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) kilimtunikia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Shahada ya Heshima ya Udaktari katika Usimamizi wa Utalii na Masoko. SUZA ilimtunuku tuzo hiyo kutokana na mchango wake mkubwa katika kuinua uchumi wa nchi kupitia sekta ya utalii.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 18 Aprili 2024, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu alitunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari katika Uchumi na Chuo Kikuu cha Ankara cha nchini Uturuki, ikiwa ni ishara ya kutambua mchango wake katika kuboresha maisha ya Watanzania kupitia mageuzi mbalimbali pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na nchi mbalimbali duniani ikiwemo Uturuki.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 03 Juni, 2024. Dkt Samia Suluhu alitunukiwa Shahada ya Udaktari wa Falsafa wa Heshima kwenye Sekta ya Anga na Rais wa Chuo Kikuu cha Sayansi ya Anga cha Jamhuri ya Korea.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** tuzo hizi mbalimbali ni ushuhuda wa kazi kubwa iliyofanywa na Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutambulika kitaifa, kikanda na Kimataifa. Hakika kama nchi, tunajivunia Lulu hii na tutaendelea kuhakikisha kama Taifa na Watanzania kwa ujumla kwamba tutaitunza, tutaienzi na kuitumia kikamilifu.

## 7.0 KUPONGEZA VIONGOZI NA WATENDAJI MBALIMBALI WA SERIKALI

**46.** ***Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nitumie nafasi kutambua*** mchango wa watendaji wote ambao wametekeleza kwa vitendo maono ya Mheshimiwa Rais. Leo tunajivunia mafanikio makubwa katika utendaji wa serikali kwa kila sekta hapa nchini. Mafanikio hayo yanatokana na kujitoa kwao katika kuhakikisha mikakati na maono vinatekelezwa kama ilivyokusudiwa.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Naibu Mawaziri na Wakuu wa Wilaya kwa usimamizi wa majukumu yenu kulingana na dhamana mlizopewa. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Hamza Saidi Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutuongoza vema katika ushauri, miongozo na kutafsiri sheria.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza pia Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Naibu Makatibu Wakuu kwa ushirikiano mlionipatia wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Waziri Mkuu.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninawashukuru *Dkt*. Jim James Yonaz, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Bi. Mary Ngelela Maganga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu). Vilevile, ninawashukuru *Dkt*. James

Henry Kilabuko, Naibu Katibu Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) na Bi. Zuhura Abdallah Yunus, Naibu Katibu Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu). Ninazishukuru sana Menejimenti za Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu pamoja na watumishi wote. Ahsanteni sana kwa utumishi wenu uliotukuka.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa pongezi nyingi kwa Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama nikianza na Jenerali Jacob John Mkunda, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi; Inspekta Jenerali wa Polisi Camillus Mongoso Wambura, Mkuu wa Jeshi la Polisi; Mkurugenzi Mkuu Suleimani Abubakar Mombo, Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa; Kamishna Jenerali wa Magereza Jeremiah Yoram Katungu, Mkuu wa Jeshi la Magereza.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, niendelee kuwapongeza Kamishna Jenerali John William Masunga, Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Dkt. Anna Makakala, Mkuu wa Idara ya Uhamiaji; Mkurugenzi Mkuu Crispin Francis Chalamila, Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; Kamishna Jenerali Aretas James Lyimo, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa pongezi kwa Wakuu wa Taasisi na watumishi wote wa umma na sekta binafsi kwa kujituma na kutoa ushirikiano mzuri katika kufanikisha shughuli za serikali. Hakika jitihada zao zimewezesha mafanikio yaliyopatikana katika nyanja mbalimbali ikiwemo kiuchumi na kijamii.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa shukrani za dhati kwa viongozi wa dini kwa utayari wao katika kushirikiana na serikali. Huduma zenu za kiroho zimechangia hali ya utulivu na ustaarabu wa jamii ya Watanzania. Hivyo niendelee kuwasihi viongozi wetu wa dini kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuleta amani, umoja na ushirikiano wa Taifa letu.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa, ninawashukuru sana wananchi wote wa Tanzania kwa kuiunga mkono Serikali ya awamu

ya sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Watanzania wenzangu, nikiri kwamba mmeonesha uzalendo, umoja na mshikamano wa hali ya juu uliowezesha serikali kutimiza majukumu yake.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza sana wananchi wote kwa juhudi kubwa katika shughuli za uzalishaji mali. Uchumi wa nchi yetu umeendelea kuwa imara wakati wote. Sina shaka hata kidogo upendo wenu kwa serikali ya awamu ya sita umekuwa msukumo wa kujitoa kwenu. Ninawaomba tuendelee kumuunga mkono Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumpa kura nyingi na za kishindo katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, 2025.

## 8.0 MAENEO YA MSISITIZO

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu naomba sasa niweke msisitizo katika masuala muhimu kama ifuatavyo:

### Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2025/2026

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 24 Juni, 2025 ndani ya bunge lako tukufu sote kwa pamoja tulipitisha kwa kishindo Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Nitumie nafasi hii kusisitiza maeneo yafuatayo: -

Mosi: Maafisa Masuuli katika ngazi zote wazingatie vipaumbele vilivyoanishwa kwenye bajeti iliyopitishwa na bunge.

Pili: Maafisa Masuuli wakamilishe miradi yote ambayo haijakamilishwa sambamba na kutekeleza ahadi za viongozi inayotekelezwa katika maeneo yao.

### Uchaguzi Mkuu 2025

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi

Oktoba, 2025. Hivyo, nitumie fursa hii kuwakumbusha wadau mbalimbali kila mmoja kwa nafasi yake ikiwemo wananchi ambao ni wapiga kura kushiriki kikamilifu katika uchaguzi huo.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe rai kwa kila mmoja wetu kuhakikisha analinda na kuitunza tunu ya amani na utulivu wa nchi yetu kabla, wakati na baada ya uchaguzi. Kwa upande mwingine, Serikali itahakikisha inatekeleza wajibu wake wa kusimamia Katiba, sheria na taratibu zilizowekwa ili kila mwananchi mwenye sifa ya kuchagua na kuchaguliwa aweze kutimiza haki yake ya kikatiba bila vikwazo vya aina yoyote.

## 9.0 MICHEZO

### Michezo ya Bunge Bonanza

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** nianze kwa kukupongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendesha mabonanza ya michezo. Ninafahamu mabonanza haya yameanza kufanyika tangu Januari Mwaka 2023, kwa lengo la kuwahamasisha Wabunge na Watumishi wa Ofisi ya Bunge kujenga tabia ya kufanya mazoezi kama wanafamilia ya Taasisi ya Bunge.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, yanalenga kujenga na kuimarisha afya, umoja kama Taasisi, na kuongeza tija katika kutekeleza majukumu ya kulitumikia Taifa letu kwa ufanisi. Pia, ni fursa kwa wadau mbalimbali kushirikiana na familia ya Bunge pamoja na wananchi katika michezo na burudani kwa pamoja na Wabunge wao.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninakupongeza sana kwa kutoa fursa hii kwa waheshimiwa wabunge kuonesha vipaji vyao katika michezo mbalimbali. Ama kwa hakika waheshimiwa wabunge wameonesha umahiri mkubwa na viwango vya michezo vya hali ya juu vyenye ubora wa kitaifa na kimataifa na wanastahili pongezi.

**Mwenendo wa Mashindano ya Kimataifa ya Soka:**

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika miaka ya hivi karibuni, Tanzania imeendelea kujipambanua kama nchi yenye vipaji, ari, na uwezo mkubwa katika michezo. Timu yetu ya soka Taifa ya wanaume, Taifa Stars, imeonyesha ushindani wa hali ya juu kwenye mashindano ya kimataifa, ikiweka rekodi za kuvutia kwenye mechi za kufuzu AFCON na hata kushinda timu ambazo zamani zilitazamwa kama vigogo wa soka barani Afrika. Vivyo hivyo, timu ya wanawake, Twiga Stars, imeendelea kutoa taswira ya matumaini kwa wasichana wetu, wakionesha kuwa michezo si ya jinsia fulani bali ni ya kila mwanamichezo mwenye ndoto, bidii na moyo wa uzalendo.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilabu vyetu vya mpira wa miguu nchini vimeendelea kupeperusha vema bendera yetu ya taifa kwa kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa na kuwa timu tishio Barani Afrika kwa sasa. Hapa nitambue kazi kubwa iliyofanywa na Timu yetu ya Yanga kwa kuweza kupiga hatua muhimu kwenye Kombe la Mabingwa Barani Afrika na kufikia hatua ya makundi ya msimu wa 2024/2025 ambayo ni muhimu sana kwa ustawi na ubora wa ligi yetu.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** jana tarehe 25 Juni, 2025 ulichezwa mchezo namba 184 wa Ligi Kuu ya NBC kati ya Yanga na Simba katika dimba la Benjamin Mkapa maarufu kama Lupaso. Mchezo huo ulimalizika kwa Timu ya Yanga kuifunga Simba mabao mawili kwa bila yaliyofungwa na nyota Pacome Zouzou na kijana wetu wa Kitanzania Clement Mzize.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba niungane na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuipongeza timu ya Yanga kwa kutwaa ubingwa wa 31 wa Tanzania Bara ikiwa ni ubingwa wa nne mfululizo. Aidha, niwape moyo klabu ya Simba kwa kupambana mpaka mechi ya mwisho na kuongeza ladha ya ligi yetu. Pia, niwapongeze wachezaji wote wa ligi zote nchini, Viongozi wa vilabu vya soka na Viongozi wa Shirikisho letu la Mpira nchini (TFF).

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, niipongeze sana Klabu ya Simba kwa hatua kubwa ya kutinga fainali katika Kombe la Shirikisho Barani Afrika kwa msimu wa 2024/2025. Timu hiyo ilihitimisha mchezo wake kwa sare ya goli moja kwa moja dhidi timu ya RS Berkane kutoka Morocco katika uwanja wa New Aman Zanzibar. Ninazipongeza sana timu zetu za Yanga na Simba kwa hatua kubwa waliyofikia.

**Maandalizi ya CHAN 2025 na AFCON 2027**

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025, Tanzania imepewa heshima ya kipekee kuwa mwenyeji wa Michuano ya Ubingwa wa Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ligi za Ndani – CHAN 2025. Tayari Serikali kupitia Wizara husika, kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), imeanza maandalizi ya kina ya kuhakikisha viwanja, miundombinu, na huduma muhimu zinakidhi viwango vya kimataifa.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Juni, 2025 ukarabati wa uwanja wa New Amani - Zanzibar umekamilika; ujenzi wa uwanja wa Arusha umefikia asilimia 47; ukarabati wa uwanja wa Benjamin Mkapa umefikia asilimia 88.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na jitihada za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya msingi, vilevile ukarabati wa viwanja vya mazoezi unaendelea ambapo ukarabati wake umefikia asilimia 90. Viwanja hivyo ni Gymkhana, Uwanja wa Chuo cha Sheria na Uwanja wa Meja Generali Isamuhyo.

**Pongezi kwa Washindi wa Michezo Mbalimbali**

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/2025 wanamichezo na timu mbalimbali wamefanya vizuri katika mashindano ya kimataifa na kuipeperusha vema bendera ya Taifa. Baadhi ya timu na wanamichezo hao ni pamoja na:

i. Mabingwa wa Mashindano ya Wanawake ya Afrika Mashariki na Kati (*CECAFA SENIOR WOMEN'S CHAMPIONSHIP 2025*);

ii. Timu ya Taifa ya Kriketi ya wanaume chini ya miaka 19 ambayo imefuzu kucheza kombe la dunia ambalo litafanyika katika nchi za Zimbabwe na Namibia mwaka 2026;

iii. Timu ya taifa ya wanawake ya mchezo wa Futsal ilishika nafasi ya pili katika mashindano ya Afrika na imefuzu kucheza kombe la dunia nchini Ufilipino mwezi Novemba, 2025;

iv. Klabu ya Simba ilifika hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho la CAF na kuwa mshindi wa pili baada ya kupoteza mchezo wake na timu ya RS Berkane kutoka nchini Morocco;

v. Timu ya Taifa ya wasichana ya mpira wa kikapu ya umri chini ya miaka 16 ilikuwa mshindi wa mashindano ya Afrika Mashariki ambayo yalifanyika Kibaha mkoani Pwani mwaka 2024;

vi. Mwanariadha Alphonce Simbu alishika nafasi ya pili na kupata medali ya fedha katika mashindano ya Marathoni ya Boston ambayo yalifanyika nchini Marekani mwezi Aprili, 2025.

## 10.0 HOJA YA SHUKRANI NA KUTOA HOJA

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa ninamshukuru kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwanza kwa imani isiyopimika aliyoionesha kwangu tangu aliposhika hatamu ya kuliongoza Taifa hili. Kwa hakika ni jambo linaloweka historia isiyosahaulika kwangu binafsi, familia yangu, wana-Ruangwa na Watanzania kwa ujumla.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** niruhusu kwa unyenyekevu mkubwa nigusie jambo la kihistoria, lenye hisia na lenye uzito mkubwa kwa Taifa letu. Kama Taifa, tunakumbukumbu ya majonzi na maumivu makubwa tuliyoyapitia kwa tukio la tarehe 17 Machi 2021, pale ambapo

tulimpoteza Kiongozi wetu kipenzi, Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Ukweli usiopingika ni kwamba, tukio hili lilituacha sote tukiwa na majonzi, taharuki na giza nene.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika giza hilo la huzuni iliyogubika taifa letu, Mwenyezi Mungu alimpa ushupavu, ujasiri na utulivu wa kipekee Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na akawa faraja kubwa kwa Watanzania. Kiongozi huyu alisimama imara katika upepo mkali wa historia ya nchi yetu, alichukua hatamu ya uongozi kwa utulivu, kwa busara na kwa ujasiri usioyumba. Katika kipindi hiki alitufundisha kuwa utulivu si udhaifu, bali ni nguvu ya ndani inayotoka kwa Mungu katika kushughulika na masuala makubwa ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ndani na nje ya mipaka ya Nchi.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho kigumu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alinionesha imani kubwa na hatimaye aliamua niendelee kumsaidia kwa nafasi ya Waziri Mkuu. Hili si jambo dogo. Ninayakumbuka maneno yake kwangu: *"Kassim Tuendelee kushirikiana kulitumikia Taifa letu, simamia shughuli za Serikali"*. Ninamshukuru kwa moyo wa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani aliyoionesha kwangu.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha uongozi wake, tumeweza kusimama imara kama Taifa, tumesimamia tunu za taifa za amani na utulivu, tumeendeleza miradi ya maendeleo ya kimkakati na huduma za jamii, tumeimarisha demokrasia, tumeimarisha diplomasia, kujenga uchumi na kujenga mshikamano wa kitaifa. Hayo yote yametokana na uongozi imara wenye hekima wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***77.*** Hivyo nimalizie kwa kusema kuwa ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa Mwalimu wa subira, kielelezo cha ujasiri, ustahimilivu na alama ya matumaini kwa kizazi hiki na kijacho. Pia ninaomba nimnukuu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Awamu ya 4 alisema:***

***"Hapa Tanzania leo hakuna mwanasiasa maarufu kama Rais Samia iwe ndani ya Chama ama nje ya Chama Cha Mapinduzi".***

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** daima nitaendelea kumshukuru na ninamuombea ushindi mkubwa kwenye uchaguzi mkuu ujao. Vilevile, ninawaombea ushindi wa kishindo Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, mgombea mwenza wa nafasi ya Urais na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Mgombea wa Urais Zanzibar.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia, kukupongeza sana wewe binafsi kwa namna ulivyoendesha Bunge hili kwa weledi, busara na ujasiri wa hali ya juu. Katika kipindi cha uongozi wako katika Bunge hili, sote tumeshuhudia imani kubwa ya Dunia kwa nchi yetu kupitia wewe Spika wetu, pale ambapo Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) ulipoamua kukupa dhamana kubwa ya kuwa Rais wa Bunge hilo. Kuchaguliwa kwako sio tu kumeliheshimisha taifa letu pekee, bali kumeliheshimisha Bunge letu ambalo ndilo lilianza kuonesha imani kwako na tunajivunia kukupa imani hiyo.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** sote tunafahamu kuwa umefunga mkanda wa kazi na upo tayari katika kuwahudumia wananchi wa jimbo lako jipya la Uyole baada ya kufanya vizuri Jimbo la Mbeya Mjini. Sina shaka kuwa wananchi wanasubiri kwa hamu kubwa kukupa ridhaa ya kuwawakilisha katika chombo hiki. Niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kukutakia kila la kheri katika uchaguzi mkuu ujao. Ninaomba wana uyole mrudisheni Mheshimiwa wetu bungeni ili aje kuwawakilisha.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, niendelee kumpongeza Naibu Spika wa Bunge letu Mheshimiwa Mussa Azan Zungu Mbunge wa Ilala nawe tunakuombea kheri kwenye mchakato ujao upate ushindi wa kutosha. Ninawashukuru na kuwatakia ushindi mnono Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb); Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb); na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb). Tunawaomba wapiga kura wawape kura za kutosha ili warudi bungeni tena.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninamtakia kila la kheri Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ili wananchi wa Bukombe waweze kukupitisha na kukupa kura za kutosha kushinda. Umekuwa msaada sana kwangu katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Hongera na kila la kheri.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kutambua kazi kubwa iliyofanywa na Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu; Naibu Makatibu Wakuu na Wasaidizi wote. Kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri ninawaombea ushindi mwema na wa kishindo. Inshaalah mtashinda kwa ushindi mnono.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninarudia tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa mlionipa wakati wote nikitekeleza majukumu yangu. Nami ninawatakia ushindi wa kishindo kwenye kinyang'anyiro cha kura za maoni na uchaguzi mkuu ili mrudi bungeni.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, ninampongeza Ndugu Baraka Ildephonce Leonard, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa shughuli za bunge. Ninawapongeza pia watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kazi kubwa na nzuri ya kuandaa, kuratibu shughuli za bunge.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ninawapongeza wanahabari kwa kazi kubwa ya kuuhabarisha umma kwa uwazi, uaminifu na weledi wa hali ya juu katika kipindi chote cha mkutano. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawapongeza madereva ambao mmesimaia usalama wa Waheshimiwa Wabunge kuja na kurudi Dodoma. Hii ni pamoja na watoa huduma wengine waliotuhudumia katika kipindi chote cha bunge.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tukiwa tunaelekea kuhitimisha Mkutano huu wa 19 wa Bunge la 12, nikiri kuwa, Bunge hili limefanya kazi kwa bidii, tumetafakari hoja, tumejadili miswada, na tumetoa maazimio yenye tija kwa maendeleo ya nchi yetu. Ni wakati sasa wa kurejea

majimboni ili kujiandaa na Uchaguzi Mkuu, ni matumaini yangu wananchi watatupa ridhaa kwa mara nyingine.

***88. Mheshimiwa Spika,*** Baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mketi kwa sababu hoja hii ikiwasilishwa kwa ngazi hii hamuhojiwi wala hamuungi mkono, lakini ninawashukuru sana, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mnataka lazima muhojiwe? Siyo utaratibu wetu.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wasilisho hili ambalo pamoja na mambo mengine, lakini ameeleza kwa kirefu kazi ambazo zimefanyika katika Bunge letu hili la 12, lakini pia Bunge katika Mkutano huu wa 19. Baada ya kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge nami nizungumze nanyi kwa kifupi.

Nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya na kutuwezesha kushiriki katika Shughuli za Bunge letu Tukufu kwa kipindi cha miaka mitano na nikitaja hapa miaka mitano mnafahamu Bunge hili la 12 limepata fursa ya kuongozwa na Waheshimiwa Maspika wawili; lilianza kuongozwa na Mheshimiwa Spika wetu Mheshimiwa Job Yustino Ndugai. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana, kisha nikapata nafasi mimi ya kumpokea kijiti. *(Makofi)*

Leo ilikuwa apate fursa ya kuzungumza nanyi, lakini amesema kwa kuwa wewe utazungumza basi utazungumza utakayosema ya Bunge zima hili la 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ndugai tunakushukuru sana kwa utumishi wako kwa Bunge hili kwa sehemu ambayo uliweza kuhudumu kwenye nafasi ya Mheshimiwa Spika. Nawe tunakutakia kila la kheri katika yaliyo mbele yako, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge katika safari hii wapo wenzetu ambao hawapo nasi tena wametangulia mbele za haki. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awajalie pumziko la amani na sisi sote tuendelee kuilinda nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, mnamo tarehe 15 Juni, 2020 nilipata heshima ya kusimama mbele yenu kama Naibu Spika nikiwasilisha salamu zangu baada ya kuhitimishwa kwa mjadala wa Bajeti Kuu ya Serikali wa mwaka 2020/2021. Leo hii nimejaliwa fursa nyingine adhimu kabisa kuzungumza nanyi nikiwa Spika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaendelea kutoa shukrani za dhati kabisa kwa heshima kubwa mliyonipa ya kuwatumikia kama Spika kwa takribani miaka minne. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaelekea mwisho wa kipindi cha uhai wa Bunge la 12, hiki ni kipindi cha kutazama nyuma na kutafakari mambo mengi tuliyoyatekeleza kwa pamoja kama Bunge na kama wawakilishi wa wananchi katika majimbo yetu, katika mikoa yetu kwa wale wa Viti Maalum.

Katika kutafakari haya, ninaomba nianze kwa kutoa salamu maalum kabisa za shukrani za dhati kwa Chama Cha Mapinduzi hususan Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Chini ya uongozi wake, chama chetu kiliridhia jina langu liwasilishwe kwa Waheshimiwa Wabunge ili lipigiwe kura kufuatia kujiuzulu kwa aliyekuwa Spika wa wakati huo ambaye nimetoka kumleta kwenu muda si mrefu Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa imani kubwa mliyonipa. Hakika kipindi hiki kimekuwa ni darasa muhimu kwangu katika kukuza ujuzi na maarifa ya kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninapenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. *(Makofi)*

Kwa ujuzi wake, uzoefu wake na weledi wake amekuwa ni mtu ambaye ni Mwalimu bora lakini pia amekuwa ni mtu wa msaada sana kwangu kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. *(Makofi)*

Katika kipindi chote hiki amenipa ushauri, amenipa pia maarifa lakini pia amenipa msaada wa karibu katika kutekeleza majukumu yangu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Mheshimiwa Dkt. Biteko amemwakilisha vizuri sana Mheshimiwa Waziri Mkuu katika majukumu yake na ameyafanya hayo kwa ufanisi kama msaidizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Bungeni na hata nje ya Bunge. *(Makofi)*

Kwa upande wetu sisi kama Bunge ametusaidia sana katika utekelezaji wa majukumu yetu na yangu mimi pia kama Spika kwa nafasi yake kama Mheshimiwa Mbunge na pia kama sehemu ya viongozi.

Aidha, nitumie pia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huyu ni Mbunge wa Ilala, lakini pia ni Naibu Spika. Amepewa sifa nyingi nanyi Wabunge, lakini amepewa sifa nyingi na viongozi upande wa Serikali na hata leo amepewa sifa

nyingi na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sifa zote, mimi kama mtu ambaye ni kiongozi wake, zinamstahili. Ni mtu mwenye weledi, ni mtu mwenye ushirikiano mzuri, lakini pia ni mtu anayejishusha, amefanya kazi nzuri. Mheshimiwa Zungu, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia hapa wamepata nafasi ya kuzungumza nanyi Wenyeviti watatu wa Bunge. Nao nitumie fursa hii kuwashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kunisaidia hapa mbele. Wakati mwingine ratiba inakuwa ngumu sana kupanga na mtu anapigiwa simu muda huo huo ambao inabidi aingie hapa mbele, lakini wote wameonesha utayari. Ninawashukuru sana kwa ushirikiano wenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, upo usemi wa lugha yetu adhimu ya Kiswahili usemao, kidole kimoja hakivunji chawa. Inaweza kudhaniwa kwamba baada ya kupata fursa ya kuwa Naibu Spika kwa takribani miaka sita ningekuwa nimekamilika kwa ujuzi wa kuliongoza Bunge letu Tukufu, haikuwa hivyo. Nimeendelea kujifunza na kunufaika sana na weledi, uzoefu na maarifa kutoka kwenu ninyi Wabunge wenzangu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hakika nisingeweza kufanya kazi zangu kwa ufanisi bila ushirikiano mkubwa nilioupata kutoka kwenu. Nimepata ushirikiano wenu kwa ngazi ya mtu mmoja mmoja, ushirikiano wenu kama Wajumbe wa Kamati mbalimbali ambazo ninaziongoza, lakini ushirikiano wenu pale ambapo Bunge lilitakiwa kufanya maamuzi. Ninawashukuru sana kwa namna mlivyofanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa Wabunge wenzangu wa Chama Cha Mapinduzi, Chama Tawala, mmekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba ushirikiano wenu kwangu kama Spika umeleta ufanisi katika kutekeleza majukumu yetu ya pamoja kwa kuzingatia maslahi ya chama chetu na matarajio ya wananchi waliotukabidhi dhamana ya kuwatumikia kupitia Bunge hili. Kupitia usimamizi wenu mahiri tumeweza kuhakikisha kwamba tunaendelea kushikamana

na pia tunaendelea kufuatilia utekelezaji wa dira kuu ambayo ni Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia napenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao mnatoka vyama vingine vya siasa vyenye uwakilishi hapa Bungeni. Michango yenu mliyoitoa, hoja mbadala mlizozitoa na ushauri mlioutoa umeongeza ubora wa mijadala yetu hapa Bungeni. Tumetofautiana kwa hoja na hatimaye tukatoka na matokeo yaliyoonekana bora zaidi na yenye manufaa kwa nchi yetu sisi sote. Kwa hakika ada ya Bunge letu ni kupingana kwa hoja na siyo kupigana, ama unaweza kusema ni kupingana bila kupigana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sehemu kubwa ya uhai wa Bunge hili, shughuli zetu zimesikika na kuoneshwa mubashara na vyombo vya habari. Wananchi wamepata nafasi ya kufuatilia kwa umakini yaliyokuwa yakifanyika ndani ya Bunge. Wapo walioweza kutoa maoni yao kupitia mitandao ya kijamii na kwa njia hiyo wametusaidia kufahamu fikra zao na masuala ambayo walitamani yawekwe mbele kwenye ajenda za Bunge. Ushiriki wao kupitia njia hiyo umeniimarisha mimi kama Spika na pia nanyi mmetumia hayo katika michango yenu mbalimbali ambayo mmeweza kuileta hapa ndani kwa ujumla katika kuendesha shughuli zetu ndani ya Bunge hili. Ninawashukuru sana Watanzania wenzangu, ninawashukuru sana wananchi wote kwa michango yenu hiyo ambayo mmeitoa katika nafasi mbalimbali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimetaja hapa mitandao ya kijamii, lakini hiyo haikuwa pekee, mnafahamu kazi zetu hapa nyingi zinahusisha wadau na ninyi wananchi kama sehemu ya wadau mmekuwa mkijitokeza kwa wingi kabisa kuja kutoa maoni yenu na sisi tumewapokea na maoni yenu tumeyafanyia kazi. Kwa hiyo, tunawashukuru sana wananchi wote kwa ngazi mbalimbali kwa namna mlivyoshiriki kuliendesha Bunge hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili limetekeleza vyema majukumu yake ya Kikatiba ya kutunga sheria, kuidhinisha mipango

ya maendeleo na bajeti na kuridhia mikataba ya kimataifa kwa kuzingatia Katiba, Sheria na Kanuni za Bunge. Jumla ya miswada 60 imepitishwa na kuwa Sheria, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 ambayo imeletwa mbele yetu leo hapa na Waziri wetu wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na pia tumepata fursa ya kuutazama na kuupitisha Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, 2021/2022 mpaka 2025/2026.

Waheshimiwa Wabunge, bajeti zote za Serikali kwa kila mwaka zimepitishwa na Bunge hili, hatukupata changamoto ambapo bajeti ya Serikali ilirejeshwa, lakini mikataba, maazimio na itifaki takribani 16 za kimataifa zimeridhiwa na Bunge hili la 12. Vilevile, mmepata fursa ya kuuliza na kujibiwa maswali na Serikali. Maswali ya kawaida yalikuwa 5,057. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mmefanya kazi kubwa ya kuwawakilisha wananchi kwa kadri walivyowatuma na haya ni yale maswali ya msingi. Maswali ya nyongeza yalikuwa 10,005. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mjuavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu amepata nafasi pia ya kusikiliza maswali yenu na yeye kutoa majibu. Maswali aliyoulizwa Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Bunge la 12 ni maswali 260, sasa idadi hii ya maswali inaonesha namna ambavyo mmejishughulisha na hoja za wananchi mmezileta upande wa Serikali. Serikali imeweza kutoa majawabu kwa hoja hizo na yale ambayo yanahitaji majawabu ya muda mrefu basi Serikali imeyaweka kwenye mipango yake ili wananchi waweze kutatuliwa changamoto zao na ziweze kufanyiwa kazi.

Waheshimiwa Wabunge, haya yote ni mchango muhimu katika kuimarisha demokrasia, uwajibikaji na maendeleo ya Taifa letu. Pia hoja binafsi nne ambazo zililetwa na Waheshimiwa Wabunge zilijadiliwa na Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, mbali na kutekeleza majukumu ya Kikatiba, Bunge la 12 limepiga hatua kubwa katika kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma; kupitia Kamati zake za

Kudumu limeongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Kibunge, kama Bunge Mtandao, usambazaji wa nyaraka kidigitali na mambo kama haya. Pia limeboresha miundombinu na huduma kwa Wabunge na watumishi wa Bunge, limeshiriki kikamilifu katika vyama na taasisi za kimataifa ambapo baadhi yetu tumepata heshima ya kuwawakilisha huko nje aidha kwa kuchaguliwa ama kwa kuteuliwa. Kwa hiyo, tumepata nafasi nzuri ya kulitumikia Taifa letu.

Waheshimiwa Wabunge, vilevile Bunge limebuni matukio maalum kama vile *Bunge Bonanza, Bunge Marathon* na ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Kikombo Dodoma. Bunge la 11 lilijenga Shule ya Wasichana huko Kikombo na Bunge hili la 12 linajenga Shule ya Wavulana huko Kikombo. Hatua hizi zimeongeza mshikamano, afya na mchango wa Bunge katika maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya yasingewezekana bila mchango mkubwa na kujitolea sana kwa Katibu wetu wa Bunge, Ndugu Baraka Idelphonce. Katibu wa Bunge anaongoza kikosi cha watu wengi sana chini yake ambao wanamsaidia, kama Makatibu Kamati kama wasaidizi kule kwenye Kamati, na hata hapa ndani pia. Katibu wa Bunge, tunakushukuru sana kwa ushirikiano wako kwa kipindi chote ambacho wewe umekuja kuungana nasi katika Bunge hili. *(Makofi)*

Nikikushukuru wewe pia, natoa salamu hizi kwa niaba ya Wabunge wote, kuwashukuru watumishi wote wa Bunge kwa namna ambavyo mmeshirikiana nasi. Mmetupa utaalamu, uzoefu na pia mmejitoa sana kuhakikisha kazi za Bunge hazikwami. Wakati mwingine hata tukisema pengine kwa sura fulani, lakini mmekuwa wavumilivu. Tunawashukuru sana watumishi wote wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyokuwa kwa Bunge la 12 kwa upande wa Uspika, pia natumia fursa hii kutambua mchango mkubwa katika Bunge hili la 12 wa aliyekuwa Katibu wa Bunge,

Ndugu Nenelwa Mwihambi na yeye alifanya kazi kubwa sana. Alitusaidia sana na sasa amepata fursa ya kulitumikia Taifa sehemu nyingine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema hapo awali, tuko ukingoni mwa Bunge la 12, Mwenyezi Mungu akitujalia kesho tarehe 27 Juni, 2025, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atalihutubia Bunge hili Tukufu kabla ya kumaliza uhai wake. Sina shaka kwamba nyote mtakubaliana nami kwamba huu sasa ni wakati muafaka wa kutambua na kupongeza kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa kutambua kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu ameifanya. Sitaweza kusema mambo yote aliyoyafanya katika kipindi hiki cha miaka mitano kwa sababu tunazungumzia uhai wa Bunge letu, lakini ninyi ni mashahidi na Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelezo ya ziada kuhusu tuzo ambayo sisi Wabunge katika historia ya nchi hii tumetambua mchango huo wa kipekee kabisa ambao ameutoa kwa Taifa letu. Kwa sababu sitaweza kuorodhesha mambo yote aliyoyafanya ni muhimu kuyataja baadhi ya ambayo yalifanya tukampa tuzo Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wananchi wa Taifa hili.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu kwamba reli ya *SGR* kutoka Dar es Salaam, Morogoro mpaka Dodoma imekamilika na tumekuwa tukiitumia hiyo. Sasa taarifa nzuri zipo kwamba kutoka Dodoma mpaka Makutupora bado hatua chache tutafikia huko. Kwa hiyo hii ni sehemu tu ya hayo mambo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, juzi hapa ametoka kuzindua Daraja la Kigongo – Busisi la Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Hayo yote yanaonesha kwamba ilikuwa ni halali kabisa na ni sawasawa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumpa Tuzo Maalum Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere limekamilika, ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa, Waheshimiwa Wabunge wengine hasa wa Kanda ya Ziwa, ametoka huko amezindua hospitali. Pia tumeona namna ambavyo juhudi zake hizi zimesababisha kupungua kwa vifo vya mama na mtoto hata imesababisha kupewa tuzo ambayo imetolewa maelezo hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, amefanya kazi katika sekta nyingi, lakini kipekee sekta ya maji amemtua mama ndoo kichwani. Bado yako baadhi ya maeneo ambayo anaendelea kuyafanyia kazi, lakini ni lazima tutambue kwamba asilimia ya upatikanaji wa maji safi na salama imekuwa kubwa vijijini na pia mijini.

Waheshimiwa Wabunge, haya yote aliyoyafanya Mheshimiwa Rais amekuwa akisaidiwa na wasaidizi wake wakuu wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hapa ndani tunao wasaidizi wake wakuu pia wawili; yupo Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa - Waziri Mkuu na pia yupo Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko - Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba sisi sote ni mashahidi wa mambo makubwa yaliyofanyika katika sekta kadhaa, tumeona mambo makubwa yakifanyika kwenye eneo la elimu, eneo la afya, eneo la ujenzi, eneo la madini, eneo la kilimo, mifugo, uvuvi, biashara na viwanda, lakini sasa hili la nishati ni maalum kidogo kwa sababu nishati sisi kama wawakilishi wa wananchi tumeona umeme ukifika kule kwenye vijiji, tumeona umeme ukifika kwenye mitaa. Sasa pia eneo la nishati kuna hili ambalo limemletea Mheshimiwa Rais sifa kubwa sana na sisi kama Taifa, limetuletea sifa kubwa sana, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kinara wa nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sekta hizi zimetajwa kwa mifano tu, ziko nyingi ambazo kwa sababu ya muda hatuwezi kuzitaja hapa. Tungeweza kueleza mambo ya uwezeshaji wanawake kiuchumi,

tungeeleza hapa hata siku nzima, najaribu kueleza kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amelitendea haki Taifa hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kutaja sekta hizo na kazi kubwa aliyoifanya, sasa nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, mmewatendea haki Waheshimiwa Wabunge kwa kujibu maswali yao na mmewatendea haki kwa kusikiliza hoja zao wakati wa michango. Mmewatendea haki kwa kufanyia kazi maoni waliyoyatoa ambayo yameisaidia Serikali kupiga hatua katika nyanja mbalimbali.

Waheshimiwa Mawaziri, ahsanteni sana kwa nafasi hizo ambazo mmezitumikia vyema kabisa kila mmoja kwenye sekta yake. Tunawashukuru kwa sababu utumishi mlioufanya, mmeufanya kwetu sisi kama Wabunge na kama wawakilishi wa wananchi. Tumewaona huko mkienda ziara mnakuja kwenye majimbo yetu, tunawashukuru sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kutambua kwamba liko tangazo la mmoja atakayestaafu, wengine sijapata taarifa kwamba nani anakusudia kustaafu, natumia fursa hii kuwatakia kila la kheri kule ambako mnaenda ninyi kugombea. Mwenyezi Mungu awatangulie na *In Shaa Allah* mfanye vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu dhahiri wakitajwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, wako watendaji ambao wanafanya kazi nzuri chini yao kama wataalamu. Natumia fursa hii kuwashukuru watendaji wote kwenye Wizara zote kwa namna walivyotoa ushirikiano mkubwa kwa Shughuli za Bunge. Wakati mwingine maswali yanakuwa magumu sana, hoja zinakuwa za moto sana, lakini wamekuwa wavumilivu na wasikivu pia katika kuhakikisha tunapiga hatua, sisi kama wawakilishi wa wananchi na kama Taifa. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunafahamu katika hawa wataalam wapo wapanga mipango na wapo watafuta fedha, basi

natumia fursa hii kuwashukuru sana wapanga mipango na kuwatakia kila la heri katika mipango mnayoendelea kuipanga kwa sababu Dira ya 2050 imeshafikishwa hapa Bungeni. Tunaamini kwamba dira hii italipeleka Taifa letu mbele na wale waliokasimiwa kazi ya kupanga basi, watupangie vizuri sana nchi yetu iweze kupiga hatua.

Kwa wale ambao wanayo kazi ya kutafuta fedha basi nanyi tunawatakia heri huko. Kwa kweli, tunamuomba Mungu aendelee kufungua milango fedha ziendelee kuja nyingi ili mipango inayopangwa iweze kutekelezeka. Tunawashukuru sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya sote kukaa pamoja, kama Wabunge, tumejenga udugu na urafiki, tumejihisi kama wanachama wa klabu moja. Kwa sababu Yanga wametoka kushinda jana basi, inawezekana kila mmoja akajisikia kama Yanga hivi, lakini tathmini ya mara kwa mara inasema kwamba baada ya kila Bunge kumaliza uhai wake wanaofanikiwa kurejea katika Bunge jipya ni kama 50% hivi. Hali hii inaweza kutupa unyonge tukajiona tunaagana baada ya kama vile mahafali hivi, kama ingekuwa shuleni, lakini mimi nina matumaini makubwa kwamba wengi wetu tutarejea tena Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaamini tutarejea wengi siyo tu kwa matamanio binafsi, bali kwa kazi nzuri ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeifanya, mkiisimamia na kuishauri Serikali kwa uwezo, weledi na dhamira ya dhati kabisa. Mmetekeleza majukumu yenu kwa manufaa ya Watanzania wote na Watanzania wameona, wapiga kura wameona. Wananchi wameziona pia kazi zenu mkiwa hapa Bungeni na mnapokuwa kule majimboni, hivyo sina shaka kwamba wengi wetu tutarejea *In ShaaAllah*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo ninawatakia kila la kheri. Kama ningekuwa na fursa ningemtaja kila mmoja na kumtakia kheri kwa jimbo lake na kwa wale wa Viti Maalum kila mmoja na mkoa wake; na kwa wale wa Viti Maalum wanaopitia makundi

mbalimbali ningeataja na wao, na ningesema pia kule wanakoenda kugombea, lakini kwa ajili ya muda Waheshimiwa Wabunge wote ninawatakia kila la kheri kule mnakoenda kugombea. *(Makofi)*

Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa namna ya kipekee nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake shupavu na mahiri na wenye dira. Aidha, tunamshukuru pia baba yetu Mheshimiwa Hafidh Ameir kwa kuwa karibu na Mheshimiwa Rais wakati wote anapowatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunapoelekea kwenye mbio za uchaguzi tunawaombea Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na pia Mgombea Mwenza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi. Tunawaombea afya njema, nguvu na maarifa. Tunaahidi kuendelea kushirikiana kuhakikisha kwamba wanapata ushindi mnono, ushindi wa heshima. Sasa ushindi huu tutahakikisha wanashinda wao, lakini na chama chetu pia. *(Makofi)*

Pia nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdor Mpango kwa utumishi wake uliotukuka kwa nchi yetu. Tunamtakia yeye na Mheshimiwa Mama Mboni Mpaye Mpango afya njema na maisha ya utulivu watakapofikia hatua ya kustaafu katika siku zijazo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, itakumbukwa kwamba kwa mara ya kwanza niliingia katika Bunge hili Tukufu kama Mbunge wa Kuteuliwa na aliyekuwa Rais wa wakati huo Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Katika kipindi cha pili wananchi wa Mbeya Mjini walinipa heshima ya kuwa Mbunge wao. Tulifanya jitihada za pamoja kuliendeleza jiji letu la Mbeya kwa nguvu zetu zote tukiongozwa na kuungwa mkono na Serikali yetu. *(Makofi)*

Kwa nafasi yangu kama Spika sikuwa na uwezo wa kuiuliza Serikali maswali ama kusimama kwenye Kiti changu na kutoa mchango wa moja kwa moja, badala yake nilitumia njia nyingine kufuatilia masuala yaliyokuwa yanawahusu watu wa Mbeya Mjini na Wizara zinazohusika baada ya zile shukrani za awali basi wazichukue na hapa. Ninawashukuru sana kwa namna mlivyolihudumia Jimbo la Mbeya Mjini, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Leo hii ninafurahi kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetekeleza kikamilifu Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na ahadi ilizozitoa kwa Jiji letu la Mbeya. Wakati wa Ubunge wangu tumepata miradi kadhaa na yenyewe siwezi kuitaja hapa kwa sababu pia hapa mbele siyo kwamba ndiyo ninatakiwa nichangie nikiwa hapa; lakini iko miradi mikubwa ya kielelezo mniruhusu Waheshimiwa Wabunge wenzangu niitaje kwa kifupi. Upo Mradi Mkubwa wa Maji wa Kiwira, Mradi wa Barabara wa Njia Nne Mbeya Mjini. Pia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Igawilo, umeme kwenye kata 18 za pembezoni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yale tuliyoyasema Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya kwa nchi hii Mbeya Mjini hatujaachwa nyuma. Kwenye eneo la elimu tumepata shule mpya kabisa za msingi, shule mpya kabisa za sekondari, zahanati mpya kabisa na vituo vya afya vipya kabisa. Mambo mengi yamefanyika ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara za mitaa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninafurahi kwamba Wana-Mbeya tulisimama bega kwa bega katika kuchangia maendeleo ya jimbo letu na Mkoa wa Mbeya kwa ujumla. Hakuna sekta iliyoachwa nyuma. Sisi Wana-Mbeya tuna kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa maendeleo makubwa ambayo tumeyapata. Binafsi ninajivunia mshikamano wetu na kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa ushirikiano mzuri uliofanikisha azma yetu hii kutimia kwa pamoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mniruhusu kipekee kabisa kutambua mchango mkubwa ambao umetolewa na aliyekuwa Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Ndugu John John Nchimbi. Waheshimiwa Wabunge Mkurugenzi huyu amefanya kazi kubwa na hili mjue kwamba ninamtaja maalum kwa sababu maalum ili watu wa TAMISEMI waweze kuja kujifunza Mbeya juu ya mambo makubwa yaliyofanyika. *(Makofi)*

Sasa hivi Mbeya Mjini hakuna hoja wala hatuendi Serikali Kuu kuomba matundu ya vyoo, tatizo hilo limekwisha, tulikuwa na shida sasa limekwisha. Vyoo 540 vimejengwa vimekamilika; hatuna hoja hiyo Mbeya Mjini. Uchakavu wa shule; hapa huwa ninawasikia Wabunge wakisema shule imechakaa darasa limechakaa limefanya kitu gani, kule Mbeya Mjini tulikuwa na madarasa zaidi ya 900 yaliyokuwa yanahitaji ukarabati, lakini sasa madarasa 500 yamekwishakarabatiwa, bado 400. Kwa kuyataja hayo ambayo bado 400 ninamkaribisha sana Mkurugenzi ajaye wa Mbeya Mjini, ambaye ni Ndugu Justice Laurent Kijaji. Tunamkaribisha ili aje aendeleze yale ambayo John John Nchimbi aliyaanza. *(Makofi)*

Haya yasingewezekana bila ushirikiano mzuri na Baraza la Madiwani. Kwa hiyo, nitumie fursa kuwashukuru sana madiwani wenzangu wa Jiji la Mbeya kwa ushirikiano mzuri ambao wameutoa; na ninaamini na wao, ninawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya shukrani hizi pia nitambua mchango mkubwa ambao umetolewa na kiongozi ambaye sasa amepandishwa cheo. Sisi Wana-Mbeya Mjini tunamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumpandisha *DC* Beno Malisa kuwa Mkuu wa Mkoa mpya wa Mkoa wa Mbeya. Sasa kwa sababu sina uwezo wa kutaja kila mmoja aliyeshiriki katika maendeleo hayo viongozi wote wa Mkoa wa Mbeya wajue ninawashukuru, wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa anayeondoka sasa Mbeya Ndugu Juma Homera. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa Mbeya kuna majimbo mawili; Jimbo la Uyole na Jimbo la Mbeya Mjini. Niwatoe hofu wanajimbo la

Mbeya Mjini. Wakati nikichaguliwa mwaka 2020 nilichaguliwa kuwa Mbunge wa jimbo hili moja la Mbeya Mjini. Nitaendelea kutoa ushirikiano, hata nitakapokuwa Mbunge wa Uyole nitaendelea kutoa ushirikiano kwa Jimbo la Mbeya Mjini. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, sasa nitumie fursa hii kipekee kabisa kuishukuru familia yangu inayoongozwa na mume wangu Dkt. James Andilile Mwainyekule, lakini pia na watoto wetu, ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Ninawashukuru pia wazazi wetu, ndugu zetu wote, marafiki kwa ushirikiano na upendo wao wakati wote wamesimama nasi katika safari hii ambayo siyo rahisi sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutakiane kheri na afya njema. Twendeni tukaendeshe kampeni zetu kwa ari na kujiamini kwa sababu tumefanya kazi nzuri. Pamoja na kwenda huko tukijiamini tufuate yale maadili ambayo tunatakiwa kuwa nayo kama Wabunge. Sasa nimesema kama Wabunge kwa sababu sisi tulivyokuwa tunaapa kile kiapo tuliapa kuwa Wabunge. Kwa hiyo, umeshaitwa Mheshimiwa ukienda huko bado ukaendelee kujiheshimu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wale wa Chama Cha Mapinduzi basi tukakipiganie Chama Cha Mapinduzi kwa moyo wa dhati. Wakati huo huo nanyi pia ambao ni kundi la walio wachache tunawatakia kila la kheri kila mmoja katika mlango anaokwenda kupita ili aweze kurejea humu ndani tena. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika, Mungu atubariki sisi sote. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge si utaratibu wetu wa kawaida, lakini leo tumewaandalia jambo zuri, ninaamini mtafurahi. *(Makofi)*

Sasa tuikaribishe kwaya yetu ituimbie wimbo kisha tutaendelea na ratiba, karibuni sana Kwaya yetu ya Bunge ituimbie wimbo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, siyo Wimbo wa Taifa, Wimbo wa Taifa ni kesho huu ni wimbo maalum ndiyo maana nimesema mmeandaliwa kitu kizuri. Nani kasema wa Taifa? Siyo wa Taifa ni wimbo maalum, karibuni kwaya. *(Makofi)*

**Wimbo Maalum**

Ni jambo jema kumshukuru Mungu, kwa kutimiza miaka mitano, ya Bunge letu Bunge la Kumi Mbili, twawapongeza kumaliza salama

Hongera sana Spika wetu wa Bunge, Dkt. Tulia kwa uongozi bora wewe ni nahodha, shupavu na makini mwenye weledi kweli twakupogeza

Twawapongeza kweli Wabunge wote kwa kazi nzuri tena ya kutukuka kwa kupambana usiku hata mchana kwa lengo moja kujenga nchi yetu

Uwepo wenu Bunge la Kumi na Mbili umewezesha kutunga sheria nyingi  na kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika nchi yetu

Tukumbuke usemi ule wa wahenga, ukiona vyaelea jua vimeundwa, kila jambo lenye mwanzo huenda mwisho kwa herini twawaaga Wabunge wote

Tukumbuke usemi ule wa wahenga, ukiona vyaelea jua vimeundwa, kila jambo lenye mwanzo huenda mwisho kwaherini twawaaga Wabunge wote

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ngoja, ngoja, ngoja.

Waheshimiwa Wabunge, limetetwa pendekezo hapa kwamba kwa sababu tumeshatengua Kanuni kwa ajili ya wageni kuingia, waje waimbe hapa mbele. *(Makofi/Vigelegele)*

Haya washuke waje waimbe hapa mbele. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Once more, once more.*

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo kidogo.

**MBUNGE FULANI:** Weka kikapu.

**SPIKA:** Nani ameomba Mwongozo?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, niko hapa.

**SPIKA:** Ahaa, Mheshimiwa Kunti Majala.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru; nilikuwa ninatamani utupe mwongozo wako, kwa sababu wamefanya jambo jema kutukumbuka kwamba tumeishi nao vizuri. Sasa kuna ule utaratibu ambao haturuhusiwi kufika hapo kwenye Siwa, lakini wewe umetuambia watakuja hapo mbele tutamani na sisi angalau kuwapa hata zawadi shilingi 1000, 1000.

Kwa hiyo, tunaomba mwongozo wako tunaweza kufikaje hapo kwenye Siwa lako, nakushukuru.

**SPIKA:** Sawa, sasa Waheshimiwa Wabunge hii Siwa ina mambo mengi hebu nafikiri wale *Serjeant-at-Arms* angalau watatu waje hapa. *Serjeant-at-Arms* watatu waingie hapa ndani ili tuweze kuiruhusu kwaya.

Haya kwa hiyo hao watasimama hapo mbele nyinyi yaani kwaya itakuwa mbele ya hapo sawa jamani. Haya kwaya inakaribishwa sasa humu ndani, karibuni kwaya. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Kwaya ya Bunge iliingia ukumbini ili kutumbuiza)*

**MBUNGE FULANI:** Wamependeza sana.

**SPIKA:** Haya, karibuni sana. Jipangeni tu mistari kwa kadri muwezavyo.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, ili tuwe na utaratibu mzuri tukienda wote hapo mbele ninadhani kutakuwa na fujo hivi, kwa hiyo labda kila upande wanaweza kuzikusanya hizo pesa akaenda mtu mmoja badala ya wote, wengine tusimame maeneo yetu.

Karibu kwaya.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**Wimbo Maalum**

Ni jambo jema kumshukuru Mungu, kwa kutimiza miaka mitano, ya Bunge letu Bunge la Kumi Mbili, twawapongeza kumaliza salama

Hongera sana Spika wetu wa Bunge, Dkt. Tulia kwa uongozi bora wewe ni nahodha, shupavu na makini mwenye weledi kweli twakupogeza

Twawapongeza kweli Wabunge wote kwa kazi nzuri tena ya kutukuka kwa kupambana usiku hata mchana kwa lengo moja kujenga nchi yetu

Uwepo wenu Bunge la Kumi na Mbili umewezesha kutunga sheria nyingi na kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika nchi yetu

Tukumbuke usemi ule wa wahenga, ukiona vyaelea jua vimeundwa, kila jambo lenye mwanzo huenda mwisho kwa herini twawaaga Wabunge wote

Tukumbuke usemi ule wa wahenga, ukiona vyaelea jua vimeundwa, kila jambo lenye mwanzo huenda mwisho kwa herini twawaaga Wabunge wote

Mmerudisha huduma kwa jamii kwa kuanzisha miradi mbalimbali kama ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana pia na wavulana

Miundombinu mingi ya kiuchumi ya barabara, reli na madaraja imechochea ukuaji uchumi ni matokeo bora kwa nchi yetu

Kwenye michezo twawapeni kongole kwa uanzishab michezo mbalimbali na ikiwemo pia ile ya marathoni hongera sana Bunge tunalipongeza

Hongera sana Spika wetu wa Bunge Dkt. Tulia pia na Wabunge wote mmetuwezesha kwenda kifua mbele hongera sanakweli twawapongeza

Tukumbuke usemi ule wa wahenga, ukiona vyaelea jua vimeundwa, kila jambo lenye mwanzo huenda mwisho kwa herini twawaaga Wabunge wote

Tukumbuke usemi ule wa wahenga, ukiona vyaelea jua vimeundwa, kila jambo lenye mwanzo huenda mwisho kwa herini twawaaga Wabunge wote

Mwaliona Bunge letu
Mwaliona Bunge letu
Mwaliona Bunge letu
Mwaliona Bunge letu
Mwaliona Bunge letu
Eeeee
Mwaliona Bunge letu

Bunge letu kweli linapendeza
Linang'ara
La Watanzania wote
Linang'ara
Chini ya Spika
Linang'ara
Waziri Mkuu
Linang'ara
Katibu wa Bunge
Linang'ara
Na Wabunge wote
Linang'ara
Kwa kazi nzuri
Linang'ara
Zenye ufanisi
Linang'ara
Busara Weledi
Linang'ara
Kweli Bunge letu wee
Linang'ara
Bara, Visiwani
Linang'ara
Na Tanzania yote
Linang'ara
Njooni muone
Linang'ara
Bunge letu sote
Linang'ara
Mwaliona Bunge letu
Mwaliona Bunge letu
Mwaliona Bunge letu
Mwaliona Bunge letu
Mwaliona Bunge letu
Mwaliona Bunge letu
Eeeeh
Mwaliona Bunge letu *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** *Once more, once more, once more.*

**SPIKA:** Ahsanteni sana, sasa mnaweza kwenda.

*(Hapa Kwaya ya Bunge iliondoka ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**MBUNGE FULANI:** Na kesho tena, na kesho tena, na kesho tena. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, kwaya yetu tunawashukuru sana kwa wimbo huo mzuri kabisa, tunawashukuru sana, ahsante Katibu wa Bunge kwa maandalizi pia. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja hapa linatoka kwa Katibu wa Bunge. Mnatangaziwa Wabunge wote kwamba Ofisi ya Bunge imeandaa Jarida la Bunge Toleo la Kumi. Jarida hili linaeleza masuala mbalimbali ya Kibunge ikiwemo matukio yaliyojiri katika Bunge la 12 na baadhi ya matukio katika Mkutano huu wa 19. Jarida hili limekwishawekwa kwenye tovuti ya Bunge na kwenye vishikwambi vyenu Waheshimiwa Wabunge na nakala ngumu mtagawiwa. Hilo ndilo tangazo nililokuwa nalo hapa.

Sasa baada ya yote ambayo tumeweza kufanikiwa kuyafanya leo sasa tuko tayari kwa ajili ya shughuli moja ambayo *In Shaa Allah* Mwenyezi Mungu atuamshe salama kesho.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe kesho kuwahi kwa sababu anakuja Mheshimiwa Rais, usije ukajikuta umefungiwa mahali. Utaweza tu kuingia humu ndani akiwa ameshaingia na amekwishaketi, kwa sababu si tunaruhusiwa kuingia na kutoka, lakini muda fulani hivi utakaokuwa yeye ni wa kuja hapa wewe hutaruhusiwa tena kuja. Kwa hiyo, unaweza ukashikiliwa huko ukawa mkali, niwakumbushe kuwahi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*.

**SPIKA:** Ndiyo naenda kutaja. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 8.30 mchana.

*(Saa 7.29 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 27 Juni, 2025 Saa 8.30 Mchana)*